# Nipashe

Jumatano Agosti 14, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579996

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



ST.JOSEPH UNIVERSITY In Tanzania

"WHERE YOUR DREAMS ARE NURTURED"

Calling all Old Students of SJCET, SJCIT, SJCMC, SJCHS and SJUIT-ARUSHA

SJUIT invites its Alumnus for the Alumni meet from 4:00PM-9:00PM on 24th August, 2019, "Entrance is free". For details www.alumni.sjuit.ac.tz

For more information contact: +255 676 504 147 +255 745 281 505

215359802


## Waziri aahidi matumizi Kiswahili nchi za SADC

UKURASA 3

# Hali mbaya majeruhi ajali gari la mafuta

**WAGONJWA** 13 hoi ICU Muhimbili, waliopoteza maisha wafikia 76, dereva aliyekimbia lori lililoanguka Ruvuma mbaroni... *Endelea uk. 2*



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Ushirikiano wa Kimataifa na Uhusino wa Jamhuri ya Namibia na Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa SADC aliyemaliza muda wake, Netumbo Nandi Ndaitwah (kulia), akikabidhi kijiti cha uenyekiti kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi katika kikao cha Mawaziri wa Nchi za SADC, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: MAELEZO**

## Mamia wajitokeza upasuaji kupunguza ukubwa wa matiti

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### KANISA LAVUNJWA KWA AMRI YA DC

KANISA la EAGT katika Kijiji cha Lwang'a, Kata ya Kasanga wilayani Mufundi, limevunjwa kwa...

UKURASA WA 3

### SHEHENA YA PAMBA YA MAGENDO YAKAMATWA

GARI lenye zaidi ya tani 20 za pamba iliyonunuliwa kwa magendo na baadaye kusafirishwa bila kufuata...

UKURASA WA 4

### MALINZI AIELEZA KORTI TFF ILIVYOKUWA IKIDAIWA

RAIS wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi (59), amedai mahakamani kuwa wakati anaingia...

## Anayedaiwa kuua mke awatishia waandishi

UKURASA 4

**MICHEZO** KAKOLANYA ASHUSHA PRESHA YA AUSSEMS KWA MANULA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Hali mbaya majeruhi ajali ya lori la mafuta

**Na Waandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imesema majeruhi wanane kati ya 46 iliowapokea baada ya kujeruhiwa katika ajali ya lori la mafuta mkoani Morogoro, wamefariki dunia, huku 13 wakiwa kwenye hali mbaya.

Imesema majeruhi hao 13 wako kwenye chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU) na wote wamepoteza ufahamu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika hospitali hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma wa MNH, Aminiel Aligaesha, alisema kati ya hao waliofariki dunia, mmoja aliongezeka jana.

"Tangu tumepokea majeruhi wa ajali hiyo, waliofariki dunia ni Jackson Shao, Kulwa Dominic, Ismail Mwanga, Muhidin Mtingwa, Maige Hamisi, Issa Musa, Adinandi Khamis na Amani Urio," alisema.

Aligaesha alisema wamekumbana na changamoto kutoka kwa ndugu wa majeruhi ambao wameshindwa kuwatambua ndugu zao kutokana na majeraha ya moto yaliyosababisha ugumu katika kuwatambua.

Alisema wameshirikiana na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya utambuzi wa wagonjwa kwa kutumia vipimo vya vinasaba (DNA).

Alibainisha kuwa kati ya majeruhi 39 wa ajali hiyo waliobaki katika hospitali hiyo kubwa zaidi nchini, 25 wamepata ufahamu na 13 bado wako katika hali mbaya.

Katika mkutano huo na waandishi wa habari, Meneja wa Maabara ya Vinasaba kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Hadija Mwema, alisema: "Sampuli zitakazochukuliwa kutoka kwa majeruhi wa ajali hiyo ili kuwatambua ni kutoka kwa wazazi, watoto na ndugu wa karibu wa majeruhi hao."

Ajali hiyo ilitokea Jumamosi asubuhi eneo la Msamvu

INAENDELEA UK.8



Mwendesha guta akiwa amelisheheni vipande vya magodoro katika Mtaa wa Nyamwezi eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, na kumfanya ashindwe kuona nyuma kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Mamia wajitokeza upasuaji kupunguza ukubwa matiti

**Na Romana Mallya**

MADAKTARI bingwa kutoka Hospitali ya Aga Khan na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa kushirikiana na wenzao wa Marekani, Canada na nchi za Ulaya, wamefanya upasuaji wa kwanza Tanzania wa kupunguza ukubwa wa matiti.

Imeelezwa kuwa tayari wanawake 150 wamejitokeza kupatiwa matibabu hayo ya kibingwa, huku yakifanyika kwa mafanikio makubwa kwa mmoja wao.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Hospitali ya Aga Khan, Aidan Njau, alitangaza neema hiyo jijini Dar es Salaam jana alipozungumza na waandishi wa habari wakati kambi ya madaktari hao ikiwa Aga Khan kwa ajili ya upasuaji huo. Alisema timu ya wataalamu hao ilianza kambi yake Jumapili ikifanya upasuaji huo wa matiti makubwa na kurekebisha makovu yaliyotokana na ajali mbalimbali yakiwamo ya moto.

Dk. Njau alisema mpaka jana, walikuwa wamefanikiwa kufanya upasuaji huo kwa mwanamke aliyekuwa na matiti makubwa na kuyaweka matiti yake kwa kiwango alichotaka.

"Leo (jana) tumefanya upasuaji mkubwa, tangu saa moja asubuhi hadi wakati huo (saa sita mchana) tulikuwa tunamfanyia upasuaji mwanamke mwenye matiti makubwa kwa kiwango alichokitaka kwa sababu yanamtesa na kumuumiza mgongo na kukosa mwonekano mzuri," alisema.

Alisema mwitikio wa wanawake wanaotaka kufanyiwa upasuaji huo ni mkubwa, akibainisha kuwa wakati wanafanya uchunguzi, walijitokeza karibu wagonjwa 150.

"Kwa sasa tumemfanyia mwanamke mmoja, awamu nyingine inayotarajiwa kufanyika Novemba, tunatarajia kuwafanyia wanawake wengine wanne. Upasuaji huu siyo kazi ndogo kwa sababu unalenga kumremba mtu kwa mwonekano anaoutaka mhusika na unahitaji umakini wa hali ya juu ili kumridhisha mgonjwa kwa kile anachokihitaji," alisema.

Alisema hospitali hiyo kwa miaka mitano iliyopita imekuwa ikifanya upasuaji kwa wanawake wenye saratani ya matiti na baadaye kuwatengenezea mengine ya bandia.

"Tunafanya hivi ili akirudi kwenye jamii yake aendelee kuonekana kwa mwonekano wake wa awali badala ya kutengwa kwa kuwa na mwonekano tofauti, mwitikio ni mkubwa, tulikwenda hadi mikoani kuwaangalia wagonjwa, wengi wana matatizo," alisema.

Daktari Bingwa wa Upasuaji kutoka Marekani, Andrea Pusic, ambaye ni mkuu wa shirika la kimataifa lisilo la kiserikali la kusaidia wanawake, alisema changamoto walizokutana nazo ni pamoja na wingi wa wahitaji wa huduma hiyo na wamelazimika kuchukua wenye uhitaji mkubwa zaidi.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano, Olayce Lotha, alisema gharama iliyotumika katika awamu hiyo ya tano ya matibabu hayo ni Sh. milioni 285.6 ambazo zimepatikana kupitia wadau mbalimbali na wanufaika 56 wanaofanyiwa upasuaji wa makovu ya moto.

Mwanzilishi wa Mtandao wa Sadaka, Dk. Ibrahim Msengi, alisema wanashirikiana na serikali na taasisi mbalimbali kusaidia wagonjwa wanaohitaji kutibiwa makovu yanayotokana na ajali.

# Waliofariki dunia sasa wafikia 76

**Na Christina Haule,** MOROGORO

VIFO vya watu wa ajali ya moto vilivyosababishwa na lori la mafuta lililopinduka eneo la Msamvu mkoani Morogoro vimefikia 76, baada ya majeruhi mmoja wa Hospitali ya Muhimbili kufariki dunia juzi usiku.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Steven Kebwe, miili minane ipo chumba cha kuhifadhia maiti kwenye Hospitali ya Rufani mkoani Morogoro.

Alisema kati ya miili minane iliyopo chumba cha kuhifadhia maiti, sita imeshatambuliwa.

Dk. Kebwe alisema, juhudi za kupima vinasaba (DNA) kwa utambuzi wa wagonjwa na miili iliyobakia zinaendelea na kwamba jumla ya wagonjwa 38 wapo Hospitali ya Rufani Muhimbili wakiendelea na matibabu, huku 16 wakiwa Hospitali ya Rufani Morogoro.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenister Mhagama, alisema bado wanaendelea na suala la utambuzi, mazishi, tiba na tiba ya kisaikolojia.

Alisema, tayari wameshapokea wataalamu wa saikolojia kwa ajili ya kutoa tiba hiyo.

Vile vile, alisema timu ya maafa ya taifa imekabidhi rasmi kwa kamati ya maafa ya mkoa kuendelea na shughuli zilizobakia huku ikisimamia utekelezaji.

Alisema, shughuli mbalimbali bado zinaendelea ikiwamo mazishi kwa miili inayotambuliwa na serikali na hata wanaozikwa na ndugu zao.

Pia alisema kamati ya maafa itachukua muda mrefu kwa sababu wagonjwa bado wanaendelea kutibiwa huku wakihitaji uangalizi.

Akizungumzia tume ya wiki moja ya kuchunguza hali ya ajali iliyoundwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliwataka wananchi kuwa watulivu na kusubiri matokeo ya tume hiyo ambayo mpaka sasa ipo kazini.

Mmoja wa wataalamu wa saikolojia, Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Naftali Ng'ondi, alisema wamekuja kutoa msaada wa kisaikolojia kwa kuanzia na kufanya utambuzi wa familia zilizopoteza ndugu zao na kuangalia mahitaji kwa familia hizo, majeruhi na ndugu zao.

Dk. Ng'ondi alisema, mpaka sasa wameshapata taarifa ya vifo vya watu 76 na wagonjwa 56 waliopo hospitalini.

Alisema wameamua kutoa msaada wa kisaikolojia kwa wafiwa na wagonjwa kufuatia tukio lililotokea kuwa la kushtukiza ambalo linauwezekano mkubwa wa kuleta msongo wa mawazo na hivyo kurudishwa kwenye hali ya kawaida.

Misaada mbalimbali imeendelea kutolewa ikiwamo Benki ya CRDB Mkoa wa Morogoro na Ofisi ya Maji, Bonde la Wami Ruvu.

Watu, taasisi na makundi mbalimbali yameendelea kutoa damu katika Kituo cha Damu Salama na msimamizi wa kituo hicho, Angel Sengati, alisema mpaka sasa wamekusanya chupa 382 na wanaendelea kupokea makundi mengine ya watoa damu.

## HABARI KITAIFA

# Kabudi aahidi kukipaisha Kiswahili SADC

**Na Beatrice Moses**

MWENYEKITI mpya wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Profesa Palamagamba Kabudi, amesema nchi wanachama zinahitaji kuelekeza nguvu katika kufanikisha mapinduzi ya viwanda ili kuzalisha ajira nyingi.

Profesa Kabudi ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, alisema nguvu hizo pia zinahitajika kwenye uzalishaji mali na uboreshaji wa miundombinu, hatua ambayo itasaidia vijana wengi kupata ajira.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akihutubia baada ya kukabidhiwa uenyekiti wa Kamati ya Baraza hilo, nafasi ambayo atadumu nayo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Profesa Kapudi alisema ni wazi kwamba umoja unahitajika ili kufanikisha azima hiyo, kwa kuwa hakuna nchi inayoweza kujitegemea na kupata mafanikio kwa wakati badala yake itakuwa inajichelewesha.

"Ushirikiano huu utasaidia katika kuweka na kusimamia sera wezeshi kwenye uwekezaji na ujenzi wa viwanda nchi za SADC," Profesa Kabudi, alisema.

Kadhalika, alisema katika kutekeleza hilo, juhudi za dhati zinahitajika ikiwamo kuwa na sera wezeshi pamoja na kushughulikia na kuondoa vikwazo vya kibiashara katika maeneo yote ya nchi wanachama.

Akizungumzia wadhifa aliopewa, Profesa Kabudi alisema anaona fahari kupokea kijiti hicho cha uongozi kwa kuwa nafasi ya Tanzania katika SADC ni ya kipekee na ya kihistoria katika nchi hizo.

Alisema anapokea jukumu hilo kwa moyo mkunjufu, tena kwa heshima kubwa.

"Zaidi tunaishukuru Jamhuri ya Watu wa Namibia kwa kusimamia vyema nafasi hii kwa mwaka mzima uliopita," alisema Profesa Kabudi.

Profesa Kabudi anapokea nafasi hiyo kutoka kwa Naibu Waziri Mkuu wa Namibia anayeshughulikia Uhusiano na Ushirikiano wa Kimataifa, Netumbo Ndaitwah, aliyekuwa mwenyekiti baraza hilo mkutano wa 38 wa SADC, ambayo inamaliza muda wake rasmi wiki hii.

Alisema kwa kukabidhiwa nafasi hiyo anakumbuka jukumu zito la Tanzania katika mkutano huo wa 39 wa SADC ambalo Tanzania ililibeba katika ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika na kulifanikisha.

Alisema Tanzania ilitumika katika kuwahifadhi na kuwapa mafunzo wanaharakati wa ukombozi. Kambi zao zilikuwa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo Mazimbu, Kongwa, Nachingwea na Mgagao.

"Wakati huu tunapofanya mkutano huu wa 39 tunakumbuka pia miaka 20 ya kifo cha Mwalimu Julius Nyerere, kama kiongozi wa harakati za ukombozi na alichangia katika kuanzishwa kwa umoja huu," Profesa Kabudi alisema.

Aliahidi kuhakikisha anaongoza katika kusongesha mbele mambo manne, ikiwamo kampeni ya kufanikisha Kiswahili kuwa lugha rasmi ya SADC, wakizingatia historia kwamba ni lugha iliyotumika kwa ukombozi.

"Hatuna sababu ya kusema tunaleta Kiswahili kama jambo jipya. Tunalofanya sasa ni kwamba hii ni lugha ya ukombozi

**INAENDELEA UK.8**



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akiangalia vinyago alipotembelea maonyesho ya nne ya bidhaa za wajasiriamali katika makutano ya mtaa wa Samora na Shaaban Robert, jijini humo jana, ambayo ni fursa wakati wa mkutano wa SADC. Kushoto ni mjasiriamali kutoka Mwenge vinyago, Aika Pangani. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Kanisa lavunjwa kwa amri ya DC

**Na Beatrice Moses**

KANISA la EAGT katika Kijiji cha Lwang'a, Kata ya Kasanga wilayani Mufundi, limevunjwa kwa amri ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Jamhuri William.

Imedaiwa kuwa kanisa hilo lilijengwa kwa mabanzi likigharimu Sh. milioni 2.5 na lilianza kutumika Machi 27, mwaka huu.

Mmoja wa wazee wa kanisa hilo, aliyeomba hifadhi ya jina lake, alisema wamefadhaishwa na hatua hiyo kwa kuwa wamekosa mahali pa kuabudu.

Alidai eneo lilikokuwa limejengwa kanisa hilo, walilinunua Machi 20, mwaka huu kwa Sh. 500,000.

Mkuu wa Wilaya hiyo (William), aliliambia Nipashe juzi kuwa amelazimika kuchukua hatua hiyo kwa sababu za kiusalama, akieleza kuwa amekuwa akiwafuatilia kwa karibu wahusika wa kanisa hilo na kubaini ni 'waasi'. Kiongozi huyo wa serikali alikiri kuamuru jengo hilo la kanisa livunjwe kwa kuwa lilijengwa bila kibali cha serikali.

"Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, nilijiridhisha kwamba kikundi hicho kilikuwa ni cha waasi waliokuwa wamekusudia kuvuruga amani. "Ndiyo maana niliamuru jengo lile livunjwe, siamini kama lilikuwa kanisa maana halikusajiliwa," alisema.

Aliongeza kuwa uanzishwaji wa makanisa una utaratibu wake ambao upo kwa mujibu wa sheria, hivyo kila anayeanzisha huduma hiyo anapaswa kuuzingatia.

"Wamefanya majaribio kadhaa ili kuhujumu kanisa walilokuwa wakisali awali ikiwamo kutaka kulilipua, pia walikwenda kuvuna msitu, watu watatu wamekamatwa na wiki hii watapandishwa kizimbani," alisema.

Nipashe imebaini Mchungaji Mwakosya wa kanisa hilo aliandikiwa barua na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mufindi Agosti 5, mwaka huu, akitakiwa kuwasilisha nyaraka za usajili wa kanisa.

Barua hiyo ambayo ilitiwa saini na Mkuu wa Wilaya hiyo (William), akimtaka mchungaji huyo kuwasilisha nyaraka za usajili wa kanisa hilo saa tatu asubuhi Jumanne Agosti 6, mwaka huu bila kukosa. Mchungaji Mwakosya wa kanisa hilo aliliambia Nipashe kuwa hakutekeleza agizo la Mkuu wa Wilaya na ilipofika saa sita mchana, watu walivamia kanisani na kulivunja. Mchungaji huyo alidai anaamini hatua hiyo imechukuliwa kutokana na mgogoro ulioko kwenye ngazi ya kitaifa ya uongozi wa Kanisa la EAGT.

Alidai kanisa hilo ni tawi la Kanisa la EAGT, hivyo limesajiliwa, na viongozi wake akiwamo yeye wanafanya shughuli zao kihalali na wana vitambulisho vya kazi.

## Tani 20 pamba zakamatwa zikisafirishwa kwa magendo

**Na Happy Severine,** BARIADI

GARI lenye zaidi ya tani 20 za pamba iliyonunuliwa kwa magendo na baadaye kusafirishwa bila kufuata utaratibu, limekamatwa katika Kata ya Dutwa wilayani Bariadi mkoani Simiyu.

Imeelezwa kuwa gari hilo lenye namba za usajili T 917 BCN lilikamatwa juzi saa nne usiku likiwa limepakia iliyokuwa imekusanywa nyumbani kwa mtu katika Kata ya Gilya wilayani hapa kinyume na utaratibu.

Kwa mujibu wa utaratibu, pamba yote inatakiwa kununuliwa kupitia vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS).

Akizungumza katika eneo la tukio jana, Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, aliagiza gari hilo pamoja na dereva kushikiliwa na Jeshi la Polisi mpaka wanunuzi wa pamba hiyo watakaposakwa na kupatikana.

"Ninaliagiza Jeshi la Polisi kuendelea kulishikilia gari hilo pamoja na dereva, huku wakiwasaka wanunuzi wa pamba hiyo watafutwe ili waje kujibu kosa hilo la kununua na kusafirisha kimagendo," alisema Kiswaga na kuwaagiza wanunuzi hao wajitokeze mara moja na kujisalimisha wenyewe.

Dereva wa gari hilo, Lulyalya Deus, alieleza kutowafahamu wanunuzi wa pamba akidai kuwa yeye alilipwa malipo ya kazi ya kusafirisha.

Kadhalika, alikiri kushuhudia pamba hiyo kuanzia inapopakiwa kwenye gari, na kwamba watu hao walitoroka wakati gari liliposimamishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Katika kukabiliana na wizi wa pamba wilaya humo, Kiswaga amewataka watendaji wa mitaa na kata kuwa walinzi katika maeneo yao, na kuhakikisha hakuna pamba inayonunuliwa bila kufuata utaratibu.

# Anayedaiwa kuua mke atishia kuwafanya kitu kibaya waandishi

**Na Hellen Mwango**

MSHTAKIWA Khamis Luwonga maarufu kwa jina la Meshack (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe kwa kumchoma moto ameiambia mahakama kuwa atakuja kuwafanyia kitu kibaya waandishi wa habari wanaompiga picha.

Kadhalika, amedai atawafanyia kitu kibaya ambacho mahakama hiyo, haitatarajia kwa kuwa ameshachanganyikiwa na hajui mtoto wake yuko wapi, hivyo anahitaji amani ya moyo.

Mshtakiwa huyo alitoa madai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Salum Ally, jana kesi hiyo ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na upelelezi wake bado haujakamilika.

Mshtakiwa huyo aliomba ruhusa ya kuongea mahakamani na hakimu na alipomkubalia alidai kuwa anakerwa na waandishi wa habari kumpiga picha na kwamba ameshachanganyikiwa kwa kuwa hajui mtoto wake alipo.

"Mheshimiwa nina kitu ambacho nataka nikueleze kuhusu waandishi wa habari, wamekuwa wakinipiga picha kuanzia chini hadi ndani ya mahakama, sasa nakueleza hivi nitakuja kuishangaza mahakama nitafanya kitu kibaya sana, ninakabiliwa na kesi na sielewi hatima yangu, hapa nilipo kichwa changu kimevurugika, nina mawazo ya mtoto wangu na ninapofika hapa ili akili yangu itulie, wanakuja kunipiga picha sasa nawaeleza kuwa nitafanya kitu kibaya ambacho mahakama haitatarajia," alidai Luwongo.

Kufuatia kauli hiyo ya vitisho kwa waandishi wa habari, Wakili Wankyo alimweleza mshtakiwa kuwa, kupigwa picha ni hali ya kawaida kwa mshtakiwa yeyote anayefikishwa mahakamani, wote wanapigwa picha, hivyo amemtaka awape uhuru waandishi wa habari wafanye kazi yao.

Hakimu aliamuru mshtakiwa arudishwe rumande na kesi hiyo itatajwa Agosti 27, mwaka huu, itakapokuja kwa ajili ya kutajwa. Katika kesi hiyo, mshtakiwa anatuhumiwa kwa kosa moja la mauaji kinyume cha sheria ya kanuni ya adhabu namba 196 sura 16, kama kilichofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Katika kesi hiyo, mshtakiwa Luwonga ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam anadaiwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni, alimuua Naomi Marijani.

Mwanzoni mwa mwezi Julai, mwaka huu, mshtakiwa Meshack alisambaza tangazo magazetini na kwenye mitandao ya kijamii kuwa anamtafuta mke wake ambaye alitoweka ghafla, lakini baadaye Jeshi la Polisi kupitia Mkuu wa Upelelezi wa kanda hiyo, Camillius Wambura, alitangaza kumshikilia Luwonga akidaiwa kumuua na kisha aliuchoma moto mwili wa mkewe.



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Bariadi (Somanda), Mwanaidi Chura, akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani Simiyu jana, sehemu ambayo ilikuwa ikikaa mashine ya Utra Sound, kabla ya kuibwa na watu wasiojulikana. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Mashine ya 'utra sound' yaibwa hospitalini

**Na Happy Severine,**
BARIADI

KATIKA hali ya kushangaza mashine inayotumika kupima magonjwa kutambua taarifa mbalimbali katika mwili wa binadamu (utra sound) imeibwa na watu wasiojulikana kwenye wodi mpya ya wajawazito Hospitali ya Wilaya ya Bariadi.

Mashine hiyo pamoja na kifaa chake cha kudurufu karatasi (printer) na nyaya zake zote viliibwa Agosti 5, mwaka huu, majira ya mchana na mpaka sasa havijapatikana.

Akiongea na waandishi wa habari ofisini kwake, Mganga Mkuu wa halmashauri hiyo, Mike Mabimbi, alikiri kuibwa kwa mashine hiyo Agosti 5, mwaka huu.

Mabimbi alisema baada ya kutokea kwa tukio hilo walitoa taarifa polisi na watu 17 wakiwamo wauguzi walikamatwa kwa ajili ya mahojiano.

"Ni kweli mashine hiyo ambayo ilitolewa na wadau wa maendeleo wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), kwa ajili ya wodi ya kinamama pekee iliibiwa katika mazingira ya kutatanisha, tayari taarifa tulitoa polisi na wanaendelea na uchunguzi," alisema Mabimbi.

Aliongeza kuwa mashine hiyo inafanana na kompyuta mpakato (laptop), hivyo mtu yeyote mwenye nia ovu alikuwa na uwezo wa kuiba na kuweka kwenye begi na kutoweka nayo.

"Mashine hiyo ilitolewa kwa ajili ya wajawazito tu na ilikuwa humo kwenye wodi kwa ajili ya kurahisisha huduma na wodi hiyo, ilikuwa na vifaa vyote vinavyohitajika kwa mjamzito kikiwamo chumba cha upasuaji," alisema Mabimbi.

Alisema baada ya kuibwa kwa kifaa hicho wanalazimika kuwapeleka wajawazito kwenye mashine kama hiyo kubwa iliyoko chumba cha mionzi takribani mita 10 kutoka kwenye wodi hiyo na kueleza kuwa inasababisha usumbufu.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Mwanaidi Churu, alisema mazingira ya kuibwa kwa kifaa hicho yameendelea kuwa magumu kutokana na watoa huduma kwenye wodi hiyo kuwapo na kila mmoja kudai hajui.

Alisema baada ya mashine hiyo kuibwa wafanyakazi hao waliitwa na waliokuwa zamu usiku hadi asubuhi walieleza kuwa kifaa walikiacha, lakini walioingia mchana walidai kutokikuta.

"Kila siku hapa hospitali ni vikao na bado kifaa hakijapatikana, ingawa huduma zinaendelea, lakini kuna usumbufu maana kile kilikuwa humo humo ndani," alisema Churu.

Viongozi hao waliwaomba wananchi kutoa taarifa kwa polisi au kwa kiongozi wa serikali yeyote atakayeona kifaa kama hicho kinauzwa.

"Kifaa hiki kimeletwa hapa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wajawazito ambaye ameiba hakiwezi kumsaidia chochote, tunaomba waandishi wa habari na wananchi mtusaidie katika kupatikana kwa kifaa hiki ni muhimu sana," alisema Mabimbi.

# Malinzi aeleza TFF ilivyodaiwa

**Na Hellen Mwango**

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Jamal Malinzi (59), amedai mahakamani kuwa wakati anaingia madarakani shirikisho hilo lilikuwa na hali ngumu kiuchumi iliyosababisha madeni makubwa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kusababisha akaunti zake kufungwa kila wakati.

Malinzi alitoa madai hayo jana wakati akijitetea dhidi ya mashtaka ya kughushi na kutakatisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Richard Rweyongeza, Malinzi alidai hali hiyo ilikuwa ikimlazimu kuikopesha TFF fedha zake binafsi na alikuwa akifanya hivyo kupitia akaunti waliyoifungua kati yake na shirikisho hilo.

Malinzi alidai kuikopesha TFF kutokana na hali ngumu ya kifedha iliyokuwa ikiikabili na hivyo kulazimika kutumia fedha zake binafsi, kukopa kwa watu binafsi ama kamati ya utendaji ili kunusuru hali hiyo hasa katika matukio muhimu yanayoikuta TFF na timu ya Taifa Stars.

Akitaja baadhi ya matukio ambayo alilazimika kutoa fedha zake na kuikopesha TFF, ni kuilipa Kampuni ya Pachi Line iliyokuwa ikitoa huduma za tiketi ambayo iliwahi kukamata basi la shirikisho hilo kupitia hati waliyopewa mahakamani, lakini ili kunusuru hilo alilazimika kutoa fedha zake kuilipa kampuni hiyo.

Tukio lingine ni kuilipa Sh. milioni 20 kampuni ya udalali ya Yono, ambazo TFF ilikuwa ikidaiwa na walitaka kukamata basi la shirikisho hilo ambalo lilitolewa na wafadhili ambao walikuwa kampuni ya bia (TBL), pia alilipia Sh. milioni 40 za tiketi za ndege Kampuni ya Ethiopia Airline za wachezaji wa Taifa Stars, waliokuwa wanakwenda nchini Nigeria katika mashindano ya Afrika.

"Mheshimiwa mimi niliwahi kuikopesha TFF Dola za Kimarekani 7,000 nikiwa Harare, Zimbabwe baada ya wachezaji wa Taifa Stars kutolewa mizigo yao nje ya hoteli tuliyofikia kwa sababu shirikisho la mpira Zimbabwe lilikuwa likidaiwa na hoteli hiyo, hata baadhi ya mashahidi waliowa kutoa ushahidi wao hapa mahakamani walithibitisha hilo akiwamo Kaimu Mkurugenzi wa Fedha wa TFF, Daniel Maangi," alidai Malinzi.

Alidai deni la mwisho analokumbuka kuikopesha TFF ni Sh. milioni 15 alizolipa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ili wakalipie Kampuni ya Azam mwaka 2017, ikiwa ni takwa la mfadhili Kampuni ya Serengeti kutaka mechi za Taifa Stars zionyeshe bure na Taifa Stars ilikuwa ikicheza dhidi ya Lesotho.

Alidai wakati anaingia madarakani alikuta shirikisho hilo likiwa na madeni makubwa kutoka TRA na hiyo ilisababisha TFF kufungiwa akaunti zake mara kwa mara na wakati mwingine kuletewa hati za kuitwa mahakamani.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Agosti 15, mwaka huu kwa ajili ya kutoa uamuzi wa nyaraka za taarifa ya madeni kati ya Malinzi na TFF.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga, Karani Flora Rauya na Selestine Mwesigwa.

## HABARI KITAIFA



Meneja wa Benki ya CRDB Mkoa wa Morogoro, Steven Mapunda (wa pili kushoto), akikabidhi hundi ya Sh. milioni mbili kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana na Walemavu), Jenister Mhagama, mkoani Morogoro jana, ili kusaidia matibabu kwa majeruhi wa ajali ya moto, ambao bado wapo hospitalini. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Waziri Mahiga ataka Watanzania kujisajili

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustine Mahiga, amewataka wananchi kujisajili na kuwa na vyeti vya matukio muhimu ya kibinadamu kama vyeti vya kuzaliwa, vifo, ndoa na talaka.

Waziri Mahiga alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya pili ya Siku ya Usajili wa Matukio Muhimu kwa Binadamu na Takwimu Barani Afrika yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema usajili wa matukio muhimu ni suala ambalo linafanyika duniani kote na ni muhimu kwa mujibu wa sheria.

"Usajili ulikuwapo tangu enzi za ukoloni japo kulikuwa hakuna mfumo wa sheria, kwa sasa mfumo huo upo, hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kujisajili ili taarifa zake zihifadhiwe," Mahiga alisema.

"Nimefurahi kwa maboresho ambayo yamekuwa yakifanywa na Rita (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini) hasa kuhusisha na masuala ya teknolojia kwani kwa sasa dunia ipo katika mfumo wa kidigitali."

Balozi Mahiga pia aliwataka viongozi wa dini kuweka sawa taarifa za vyeti vya matukio ambayo ni vya kuzaliwa, kifo, ndoa na talaka ili kuisaidia serikali pindi zinapohitaji.

"Zamani tulikuwa tunahifadhi taarifa kama hizi kwa viongozi wa dini na ukienda kutaka kupata taarifa, unapata hadi za babu wa babu yako, kuanzia mwaka aliozaliwa, aliokufa na taarifa za familia yake, hili ni jambo muhimu sana kwa viongozi wetu wa dini," Balozi Mahiga alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Rita, Emmy Hudson, alisema kuwa katika kuadhimisha siku hiyo, wametoa huduma za usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa bure kama mchango katika jamii kwa wanafunzi 150 wa Shule ya Sekondari Wama Nakayama, iliyoko wilayani Kibiti mkoani Pwani na wanafunzi 102 wa Shule ya Sekondari ya Wama Sharaf iliyoko wilayani Lindi.

# Mtuhumiwa ujambazi afariki dunia hospitalini

**Na Timothy Itembe,** MARA

MKAZI wa Kijiji cha Kitenga wilayani Tarime mkoani Mara, Mwita Magori, maarufu Otieno 45, aliyekuwa akitafutwa kwa tuhuma za makosa ya uporaji wa mifugo na ujambazi, amefariki dunia muda mfupi baada ya kukamatwa mkoani Shinyanga akipelekwa Tarime kwa mahojiano.

Kamanda Mkoa wa Kipolisi Tarime na Rorya, Henry Mwaibambe, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa kwa tuhuma zilizokuwa zikimkabili za uporaji wa mifugo maeneo ya Rorya, Tarime na Kahama, akidaiwa kuwa na mtandao mkubwa.

"Kabla ya kufariki dunia katika mahojiano na polisi alitoa ushirikiano wa kutosha wa mtandao wake wa wizi wa mifugo na ujambazi ambao tunaufanyiwa kazi," aliongeza Mwaibambe. "Kwa muda mrefu Jeshi la Polisi lilikuwa linamtafuta Mwita Marwa Magori maarufu kwa jina la Otieno 45, ghafla akiwa katika mahojiano aliugua tumbo la kuhara na kupelekwa hospitali ya wilaya na kufariki dunia," alisema Mwaibambe.

Alisema alifariki Agosti 11 katika hospitali ya wilaya inayomilikiwa na Halmashauri ya Mji wa Tarime, wakati akiwa anapatiwa matibabu.

# Waombwa taarifa ajali magari mafuta

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kutoa taarifa katika vyombo vya ulinzi na usalama wanapoona magari ya mafuta yameanguka ili kuzuia vifo ambavyo vinaweza kujitokeza baadhi wanapovamia na kuchukua mafuta.

Ushauri huo ulitolewa na Mwakilishi wa Jumuiya ya Kiislamu ya Istiqama International kutoka Msikiti wa Al-wahaab, Ahmad Haroon, wakati wa Swala ya Eid Haji iliyofanyika katika msikiti huo na kusema, ajali iliyokea Morogoro inatokana na wananchi kutotoa taarifa mapema badala yake walikimbilia kuchukua mafuta bila kuangali uhai wao.

Alisema kuwa kila mwananchi anatakiwa kutafuta riziki zilizo za halali na itasaidia kuondokana na kuingia kwenye madhambi na badala yake linapokea gari la mafuta limeanguka, watoe taarifa ili vyombo vya ulinzi viangalie namna gani wanaweza kuzuia majanga yasitokee.

"Waislamu tujifunze kwa tukio lililotokea mjini Morogoro, ndugu zetu walitamani kula Sikukuu ya Eid pamoja nasi, lakini hawakuweza kutokana na ajali iliyotokea, tukumbuke kutoa taarifa kwenye vyombo vya sheria tunapoona gari la mafuta limeanguka na sio kuwaacha wananchi wakijichotea mafuta," alisema Haroon.

Aidha, Haroon alisema majanga ya wananchi kuungua kwenye moto wa mafuta wakati wakichukua mafuta kwenye magari yaliyoanguka yaliwahi kutokea katika mkoa wa Mbeya eneo la Isongole, Mdaula Chalinze, Manyoni, Mbagala na Msamvu na yote ni kutokana na kutotoa taarifa mapema.

Ashura Hamisi, aliwataka kinamama kuacha mara moja tabia ya kuyavamia magari ya mafuta yaliyoanguka na kujichotea mafuta ili kuepukana na vifo visivyo vya lazima na kuwaacha wanaume na watoto wanateseka wanapopoteza maisha.

Naye Hawa Kasimu, alisema vifo vilivyokea mjini Mororogo ni vyema Watanzania wakajifunza na kuacha tamaa za kupata mali kwa njia rahisi, badala yake wafanye kazi halali ambazo zitaweza kuwaingizia kipato.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uhuru kupindukia ni chanzo cha ajali

**POLE** tena Watanzania wenzetu mliojeruhiwa na wote mliopoteza wapendwa wenu katika ajali ya gari la mafuta lililowaka moto hivi karibuni mkoani Morogoro.

Tunafahamu kuwa ajali za barabarani na vifo vinavyohusiana na vyombo vya usafiri ni jambo ambalo kila wakati linaipasua kichwa serikali na wadau wengine wa usafiri na usafirishaji.

Tunatambua kuwa mikakati mingi imeibuliwa ikiwamo kutumia GPS au ving'amuzi kupunguza kasi ya magari ya abiria ili kuondoa ajali zisizo na sababu.

Aidha, tochi na kamera za kurekodi kasi barabarani na faini za papo kwa papo kwa madereva nazo zinatumiwa kuwadhibiti wasio na nidhamu na kuhakikisha usalama na amani vinakuwapo. Lakini yote hayo hayakudhibiti au kuepusha ajali iliyotokea Morogoro mwishoni mwa juma lililopita.

Ndiyo maana tunaona kuwa kuna haja pamoja na kutumia GPS, faini za papo kwa papo na tochi kudhibiti uhuru wa kupindukia wa kutumia barabara unaotishia usalama nchini.

Uhuru wa kupindukia unapatikana kwa waendesha bodaboda, toyo na hata maguta ambao kuna haja ya kuwaangalia upya na kuwatungia sharia ili kudhibiti.

Kwa mfano iwapo itathibitika kuwa chanzo cha ajali ya Morogoro juzi ni dereva wa tangi la mafuta kumkwepa dereva wa bodaboda ni dhahiri pikipiki inahusika moja kwa moja. Mara nyingi madereva wa pikipiki wamekuwa na uhuru mkubwa wa kufanya wapendalo wakiwa barabarani.

Mathalani jijini Dar es Salaam, bodaboda huingilia magari ya mwendokasi na kusababisha ajali na usumbufu. Aidha, hujitumbukiza hata kwenye reli na kubughudhi treni.

Ni kero kwa watembea kwa miguu ambao kwa ujumla hawana njia kwa vile njia zao sasa zimechukuliwa na pikipiki.

Licha ya kusababisha usumbufu mkubwa barabarani vyombo hivyo hubeba shehena kubwa ya mkaa inayoingizwa barabarani bila kujali kuwa mzigo uliobebwa unamzuia dereva wake kuona popote mbali na walioko mbele yake.

Si hivyo tu, mara kadhaa maguta na pikipiki hubeba mizigo kama magodoro na kutembea barabarani kwa uhuru bila kujali kuwa vyombo hivyo vinatishia usalama wa watumiaji wengine na utaratibu mzima wa usafiri na usafirishaji.

Pamoja na kuwa na uhuru huo mkubwa wa kutumia barabara wapendavyo kwenye pikipiki, bajaji na maguta, tatizo jingine la uhuru kupindukia upo kwa wafanyabiashara walio kando ya barabara kuu. Mara nyingi watu huuza bidhaa pembeni ya barabara na hata kuweka migongo na miguu barabarani bila hofu hata nyakati za usiku. Uhuru wa kupindukia unaonekana Mbezi, Ubungo maeneo ya Riverside, Kimara na maeneo kama Msavu ambako ajali imetokea. Lakini, pia kuna uhuru huo kwenye stesheni za treni ndani na hifadhi ya reli watu wakifanyabiashara bila kuogopa vyombo vya moto.

Ndiyo maana tunaona kuna kwa kuangalia na kutafakari kilichotokea Morogoro kuna haja kutumia somo hilo kuwakumbusha wananchi na mamlaka za kusimamia barabara kupunguza uhuru huo.

Watu wengi wamejisahau wanafanya biashara karibu na barabara wakitandika bidhaa kila mahali na kujiachia bila hofu kwa hilo ni eneo la hatari. Ujenzi wa barabara unaoendelea kote nchini unahaja ya kuangalia namna ya kuwa na njia za pikipiki, toyo na maguta pekee ili kupunguza ajali.

Kuna uwezekano wa kupata hasara ikiwamo ya mali na maisha iwapo watu wataachiliwa kufanya wapendalo ndani ya hifadhi ya barabara na reli. Wakala wa Barabara Tanroads na Tarura pamoja na Shirika la Reli (TRC) fuatilieni mienendo inayokiuka matumizi ya reli na barabara ili kuepusha ajali zinazoweza kuepukika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ni muhimu Waziri Lukuvi akalindwa

Na Salome Kitomari

**UPO** usemi usemao mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Msemo huu hauna ubishi kwa Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kwani ni miongoni mwa viongozi walioweza kidhati kusimamia maeneo waliokabidhiwa.

Kila nikifungua mitandao ya kijamii na hasa YouTube nakutana na video za Lukuvi akifafanua mambo mbalimbali ya ardhi yanayogusa maisha ya watu, hasa walioporwa haki zao na wenye nguvu ya kifedha na mamlaka.

Kwa muda mrefu, ardhi imekuwa ni sekta iliyojaa dhuluma na uonevu hali iliyosababisha watu kudai haki zao mahakamani na njia zingine walizoona zinastahili.

Dhuluma mojawapo ni mchezo mchafu baina ya madalali na taasisi za mikopo au watu binafsi ambao hukimbilia kuuza mali ya mtu na kubadilisha umiliki kwa haraka, huku wakimwacha mwingine katika maumivu makali.

Mathalani, wiki iliyopita vyombo vya habari vilitawaliwa na kisa cha mtu mmoja aliyeporwa haki yake kwa kuchukuliwa ghorofa lake na rafiki yake ambaye alishirikiana na watumishi wa idara ya ardhi kutengeneza hati 'feki.'

Kama siyo Waziri Lukuvi ambaye ameamua kujitolea, hakika mtu huyo angekufa bila kurejeshewa mali yake hiyo.

Tukio jingine ni mkoani Arusha ambako kikongwe alinyang'anywa mali yake na kwa zaidi ya miaka 30 ameidai mahakamani bila kufanikiwa.

Lakini kwa sababu Waziri Lukuvi amejitoa sadaka, bibi huyo amerejeshewa mali yake.

Hakuna eneo gumu kama la ardhi ambalo limejaa wajanja wanaoshirikiana na baadhi ya madalali ambao miaka yote wamekula kwa jasho la watu, wakishirikiana na baadhi ya watumishi wa idara ya ardhi ambao huuza maeneo kwa zaidi ya mtu mmoja, wote wakipewa hati moja.

Hatua hii imesababisha waathirika kutumia gharama kubwa wakisaka haki zao kwenye mabaraza ya ardhi.

Hata hivyo imekuwa ngumu kupata haki kwa sababu walio kwenye mfumo ni watu ambao wanashirikiana na magenge ya 'kijinai' kunyanyasa raia.

Kwenye miji na majiji kuna kesi nyingi za watu kuporwa ardhi zao, wamiliki wawili kuwa na hati moja, na wengine kujeruhiwa au kufanyiwa ubaya licha ya kuwa ni haki yao.

Tangu aingie madarakani, siku zote Waziri Lukuvi amekuwa akitembea huku na kule kupambana na uhalifu huo na kimsingi amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuhakikisha wenye haki zao wanazipata.

Kwa sasa eneo la ardhi linaogopeka kufanya vinginevyo kwa sababu wajanja wanajua kwamba iwapo itajulikana, hatua zitachukuliwa dhidi ya mhusika.

Kila siku yanaibuka mapya katika eneo hilo na yote yamevaa sura ya uonevu dhidi ya watu, hasa wanyonge.

Na uonevu huu unapofuatiliwa kwa kina katika sekta hii ya ardhi ambayo ni muhimu sana kiuchumi, unakuta watu wenye nguvu ya fedha ambazo wamezitumia kujihalalishia maeneo hayo kinyemela.

Naamini waziri huyu akiendelea kuwapo katika kipindi chote cha awamu ya tano, Tanzania itapiga hatua kubwa katika suala zima la kumaliza migogoro ya ardhi ambayo mingi inatengenezwa kwa manufaa ya watu fulani.

Kwa kuwa mipango miji mingi ni ya zamani na ilipangwa kabla ya ongezeko la watu na mabadiliko makubwa ya kimaendeleo, ipo haja ya kufanyika kwa mipango mipya ya kupanga miji na majiji na hasa kwenye maeneo mapya ambayo bado hayajaendelezwa.

Kwa kazi kubwa anayofanya Waziri Lukuvi ni wazi kuwa amejitengenezea maadui ambao walipora haki za watu, na kwa kuwa wana fedha wanaweza kufanya lolote wakati wowote.

Kwa misingi hiyo ni vyema zikafanyika jitihada za kumlinda Waziri huyu kwa namna yoyote ili aendelee kutetea wanyonge ambao wameporwa haki zao.

Kikubwa kinachotakiwa ni kutenda haki kwa kila anayestahili pasipo kumwonea yeyote.

## BARUA & MJADALA

# Hili Dawasco Boko si sahihi

**Ndugu Mhariri**

*TAFADHALI naomba nafasi katika gazeti lako linalotupa sisi wananchi ya kutoa malalamiko yetu, dukuduku na kero mbalimbali zinazotukabili katika mihangaiko yetu ya kila siku na dhima nzima ya kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.*

*Ninajitokeza leo ili niweze kuibainisha kero ambayo haikubaliki kwa namna yoyote ile, hasa inapofanywa na shirika la umma kama Dawasco ambalo linapaswa kuwa msitari wa mbele kulinda miundombinu mbalimbali ya serikali kama barabara.*

*Katika eneo ninaloishi la Wazo Mafuriko, lililoko Serikali ya Mtaa wa Kisanga, Kata ya Wazo, Manispaa ya Ubungo kwa hivi sasa, Dawasco walichimba mtaro kwa minajili ya kupeleka maji ya bomba kwenye Shule ya Sekondari ya Twiga.*

*Ni mtaro ambao umechimbwa na kupitishwa kwenye barabara ya mtaa inayotokea kwenye kiungo cha maji kilicho jirani na fensi za nyumba zilizo mkabala na kiwanda cha Wazo kuelekea Zahanati ya Serikali ya Mafuriko au Kisanga.*

*Kinachonifanya nilalamikie kero hii ni kwamba tangu Dawasco walipochimba mtaro huo sasa ni miezi miwili, umeachwa bila ya kufukiwa, hali ambayo sasa imeanza kuiharibu barabara ya mtaa ambapo mtaro huo umepitishwa.*

*Hatujui ni lini Dawasco Boko ambao ndio inayolimiliki eneo hilo kwa huduma ya maji watakuja kuufukia mtaro huo ambao unatishia kuharibu hata maeneo ya wakazi walio jirani na barabara hiyo.*

*Kuna madai yanayotolewa kwa wakazi wa maeneo hayo ulipopita mtaro huo kwamba huwa ni kawaida kwa Dawasco kuchimba mtaro wa kupitisha bomba na siyo kazi yao kufukia mtaro huo.*

*Sasa hapo swali ni kwamba kama siyo kazi yao kufukia mitaro wanayochimba kwa ajili ya kupitisha mabomba ya maji, ni kazi ya nani sasa kufanya kazi hiyo?*

*Haijafukiwa kwa sababu wakazi wanasema hiyo ni kazi ya Dawasco Boko, ambayo ndiyo waliochimba mtaro huo. Wasiwasi wangu ni kwamba endapo mvua zitanyesha kabla ya Dawasco kufukia mtaro huo waliouchimba, ni wazi utaharibu barabara hiyo pamoja na makazi ya watu wa eneo hilo.*


*Ninaomba kupitia barua hii Dawasco Boko ambao ndio waliochimba mtaro huo waje kuufukia.*

*Si vizuri shirika la umma likawa ndio haribifu la miundombinu ya umma.*

**Mkazi- Wazo Mafuriko, DSM**

**WASILIANA NASI:**
TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Elimu ya kujikinga dhidi ya majanga ndiyo mwarobaini




**Na Sabato Kasika**

KABLA ya yote, nianze kwa kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu zao kwenye tukio la ajali ya moto, lililotokea Jumamosi ya Agosti 10, mjini Morogoro ambalo limesababisha watu zaidi ya 70 hadi sasa kupoteza maisha.

Taifa limepoteza nguvukazi, lakini pia inawezekana baadhi ya Watanzania wamebaki yatima, wajane, wagane na wengine kubaki na ulemaavu wa kudumu uliosababishwa na tukio hilo la kusikitisha.

Baada ya tukio hilo, yapo mengi yamesemwa, wengine wakiyanyooshea mkono majeshi ya polisi na yale ya Zimamoto na Uokozi na vyombo vingine vya serikali kwa ujumla kwamba vilipaswa kuzuia na kudhibiti ajali hiyo.

Kimsingi kila mtu ana haki ya kusema, lakini binafsi sidhani kwamba ni wakati wa kulaumiana, ila ni wakati wa kutafuta njia ya sahihi ya kukabiliana na majanga kama hayo ili yasiendelee kujirudia.

Kama sikosei, tukio la Morogoro linafanana na lile lililotokea Oktoba mwaka 2002 eneo la Idweli mkoani Mbeya na kusababisha vifo vya Watanzania zaidi ya 30 na wengine 100 wakijeruhiwa.

Katika tukio la mwaka 2002, watu walikuwa wakichota mafuta baada ya gari kupata ajali kama ilivyokuwa kwa lile la Jumamosi iliyopita.

Kwamba chanzo ni kile kile, gari linapinduka kisha watu wakaenda kuchota mafuta. Ingawa kuna ajali nyingi za aina hiyo zimeshatokea, lakini ya Idweli ya mwaka 2002 na hii ya Morogoro zimesababisha vifo vingi, hali inayoonyesha kuwa kuna haja kubwa ya kutoa elimu ya kujiepusha na majanga ya moto.

Elimu hiyo ya kujifunza athari za majanga moto ikienezwa kiasi cha kutosha, jamii itakuwa na uelewa mpana na hata itakapotokea ajali ya aina hiyo watu hawataisogelea na badala yake watatoa taarifa kwa vyombo husika.

Ninaamini kwamba pamoja na mambo mengine, tatizo kubwa miongoni mwa Watanzania ni elimu duni au uelewa mdogo kuhusu jinsi ya kujikinga na majanga ya moto.

Ikumbukwe kuwa kuna magari yanabeba kemikali za sumu, milipuko na mengine mafuta ya petroli, hayo yote ni hatari na hayatakiwi kusogelewa yanapopata ajali.

Kwamba wananchi tuachane na tabia ya kusogelea ajali kwa ajili ya kushangaa au kujipatia chochote, kwa sababu moto ukilipuka unawakumba wote, hivyo ni muhimu jamii ielimishwe kutambua hilo na kuliepuka.

Ninatambua elimu ambayo imekuwa ikitolewa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuanzia ngazi mbalimbali ili kuwajengea Watanzania uwezo wa kukabiliana na majanga ikiwamo moto.

Elimu ya jeshi hilo pia imekuwa ikilenga kuwahamasisha wananchi kujilinda na kujikinga na majanga ya moto yanapotokea kama hilo lilitokea Morogoro, ambalo pia limeacha watu wengi wakiwa wamejeruhiwa.

Kwa mtu aliyeelimishwa na akaelewa, hawezi kwenda kwenye ajali ya gari la mafuta ya petroli, milipuko au kemikali na kuwasha sigara au kutoa betri ya gari, kwani mwisho wake ni kusababisha madhara makubwa.

Watu walioelimishwa na wakaelewa, ajali inapotokea kama hiyo ya Morogoro hawawezi kuikimbilia kwenda kuchota mafuta, kwa sababu watakuwa wanajua madhara, ambayo wanaweza kuyapata.

Vilevile elimu ikitolewa ya kutosha, wale wenye nia ya kutoa msaada inapotokea ajali watajiridhisha kwanza kuhusu usalama wao kabla ya kwenda kutoa msaada ili wasijikute wakiangamia.

Lakini raia kufika kwenye tukio na kuanza kuchota mafuta huku wengine wakipiga picha kutumia kamera zao bila kutoa taarifa kwa vyombo husika ili kudhibiti athari, huo ni ukosefu wa elimu ya kujinga na majanga.

Alichokaririwa na vyombo vya habari akisema, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Willbroad Mutafungwa kinaonyesha wazi kuwa elimu ya kujikinga na majanga ya moto kama hilo ni ya muhimu kwa Watanzania.

"Gari lililokuwa limebeba petroli lilipinduka, baada ya kupinduka mafuta yalimwagika watu katika eneo hilo walijitokeza kuchota mafuta, moto ukalipuka takriban watu zaidi ya 57 wamefariki," anasema Kamanda Mutafungwa.

Kwa maana hiyo kama tukio la mwaka 2002 lilikuwa limeshasahaulika, basi hili la Morogoro litukumbushe kutambua umuhimu wa kuzingatia elimu ya majanga ingawa ajali haina kinga.

Ajali haina kinga, lakini ajali husababishwa, hivyo kinachotakiwa ni kujifunza na kutambua visababishi vya ajali na kuviepuka kuliko kufanya mambo kienyeji na mwisho wa siku ni kupata madhara makubwa.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Bashungwa ashtukia mikataba ya kahawa

**Na Daniel Limbe,**
KARAGWE

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, ameliagiza Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe mkoani Kagera, kuchunguza mikataba ya ubanguaji kahawa kwenye Chama cha Ushirika cha Karagwe (KDCU). Bashungwa amesema kwa taarifa alizonazo, kumefanyika mikataba ya kinyonyaji kwenye ushirika huo kwa lengo la watu wachache kujinufaisha badala ya fedha hizo kuwaongezea wakulima kama malipo ya pili.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa kwenye Jubilei ya kutimiza miaka 25 ya kuanzishwa kwa shirika lisilokuwa la kiserikali la Mavuno sambamba na mahafali ya kwanza ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Mavuno ambayo imefadhiliwa na wadau wa maendeleo wakiwamo wahandisi wasiokuwa na mipaka kutoka Sweden na Ujerumani.

"Haiwezekani tukaendelea kuingia mikataba ya kihuni isiyokuwa na faida kwa wakulima wetu wa zao la kahawa...ninazo taarifa kuwa mikataba ya ubanguaji wa kahawa kwenye KDCU inafanywa kwa siri...wahusika hawataki kuiweka wazi," alisema.

"Ninawaagiza Baraza la Madiwani kupitia kamati ya fedha na mipango, kachukueni mikataba hiyo ya ukoboaji kahawa pale KDCU muipitie na kujiridhisha...kama kuna vipengele ambavyo havina maslahi kwa wakulima wetu virekebishwe haraka maana chama hicho siyo mali ya mtu ispokuwa ni cha wakulima wetu...kwa hiyo lazima tusimamie." Mbali na kulipongeza Shirika la Mavuno kwa kuhamasisha maendeleo ya kilimo, elimu, maji na utunzaji wa mazingira kwa wananchi wa Wilaya ya Karagwe na Kyerwa, akatumia fursa hiyo kuwaonya viongozi wa mkoa huo ambao wamekuwa kikwazo cha wakulima kuuza mazao yao nje ya nchi.

"Zao lililozuiliwa na serikali kuuzwa nje ya nchi bila utaratibu maalumu ni kahawa pekee... hivyo natoa wito kwa viongozi wote kwenye mkoa huu kuwa ni marufuku kuwazuia wakulima kutafuta masoko ya mazao yao nje ya nchi, na katika hili nitakuwa tayari kupambana na viongozi wanaoweka vikwazo."

Alisema serikali imedhamiria kuwakomboa wakulima kupitia kilimo cha kibiashara ili waweze kuinua vipato vyao hali itakayosaidia kuwa na familia zenye uwezo wa kuwagharimia watoto wao kupata elimu bora kwa kuwa ndiyo msingi wa maisha.

Mkurugenzi wa Shirika la Mavuno, Charles Bahati, alisema wamefanikiwa kuwahudumia wananchi wa vijiji 13 kwenye wilaya za Karagwe na Kyerwa ambapo zaidi ya wakulima 1,667, shule za msingi na sekondari 23 zimenufaika na fursa za kilimo mseto.

Aidha, zaidi ya visima 582 vyenye ujazo wa zaidi ya lita 16,000 hadi 22,000 vimejengwa na kuwanufaisha zaidi ya wananchi 13,960 pamoja na kuielimisha jamii kuvuna maji ya mvua kwenye kaya zao badala ya kuyaacha yakapotea bure.

# JPM ateua mwenyekiti wa maadili viongozi umma

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli ameemteua Jaji mstaafu Ibrahim Sayida Mipawa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma.

Jaji Mstaafu Mipawa anachukua nafasi Jaji Mstaafu Januari Msofe, ambaye ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria.

Taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilieleza jana kwamba uteuzi wa Jaji mstaafu Mipawa ulianza tarehe Agosti 7, mwaka huu.



Waziri wa Madini, Dotto Biteko (wa tatu kulia), akiangalia mchanga wenye madini ya chuma katika eneo la Michiga, wilayani Nanyumbu, mkoani Mtwara juzi, akiwa katika ziara ya kukagua shughuli mbalimbali za sekta ya madini. **PICHA: WM**

# Hali mbaya majeruhi ajali ya lori la mafuta

**INATOKA UK. 2**

mkoani Morogoro baada ya lori lililokuwa limebeba tangi la mafuta ya petroli, kuanguka na baadaye kulipuka wakati baadhi ya wananchi wakichota mafuta yaliyokuwa yanamwagika kutoka kwenye tangi hilo.

**DEREVA ALIYEKIMBIA LORI RUVUMA MBARONI**

Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma linamshikilia Hubert Mpete (51), mkazi wa Njombe ambaye pia ni dereva wa gari lililokuwa limesheheni petroli likitokea mkoani Njombe kwenda Songea ambalo liliacha njia kisha kugonga mti na kuwaka moto.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Jumapili saa nne usiku katika Kijiji cha Hanga Ngandinda wilayani Songea.

Alisema gari lenye namba za usajili T 243 DCU na tera mali ya mfanyabiashara James Mwinuka, mkazi wa Njombe ambaye pia ni mmiliki wa kituo cha mafuta cha Njombe Filling Station.

Alisema siku ya tukio, Mpete alikuwa akiendesha gari hilo kwa mwendokasi, hivyo kumshinda, kuacha njia kisha kuelekea porini na kugonga mti kulikosababisha kichwa cha gari kuwaka moto na kuteketea.

Alisema baada ya kupata taarifa ya ajali hiyo, Jeshi la Polisi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walifika katika eneo hilo na kukuta gari likiwaka moto na kufanikiwa kuokoa mafuta yenye ujazo wa lita 33,000 na kuuzima moto huo kabla ya kutokea madhara.

Kamanda Maigwa alisema dereva huyo amelazwa katika Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma akiendelea kupatiwa matibabu chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi na hali yake ya kiafya ikitengamaa, utaratibu wa kumhoji utaendelea ili baadaye afikishwe mahakamani.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Magafu Majura, alithibitisha kuwapo kwa majeruhi huyo katika hospitali yake, akieleza kuwa anasumbuliwa na maumivu ya kifua na paja la mguu wa kulia.

■ **Imeandikwa na Philip Nyiti na Mariam Magili, DAR, Gideon Mwakanosya, SONGEA**

# Kabudi aahidi kukipaisha Kiswahili SADC

**INATOKA UK. 3**

waliyoitumia wakati wa kupigania uhuru, sasa iwe moja ya lugha rasmi SADC," alisema.

Alisema kuna mwitikio kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa tayari imeanza kutumika katika kufundishwa kwenye zaidi ya vyuo 58 duniani, pia ni miongoni mwa lugha kumi zinazozungumzwa duniani na watu wengi.

"Hivyo Tanzania itatilia mkazo isiwe lugha ya Afrika Mashariki pekee, bali iwe ya SADC na hatimaye lugha unganishi na jumuishi ya bara lote," alisema.

Profesa Kabudi alisema pia wapo kwenye harakati za kutaka jumuiya ya kimataifa kuondoa vikwazo vya kiuchumi kwa Zimbabwe.

"Uongozi uliopo Zimbabwe umechaguliwa kwa demokrasia, hivyo kuna haja ya kuiondolea vikwazo vya kiuchumi ili ipate fursa ya kushiriki kikamilifu katika kujitafutia maendeleo," alisema.

Alitaja mambo mengine kuwa ni pamoja na kusisitiza kuongeza ajira kwa vijana, kuhamasisha masuala ya afya na maendeleo kwa wanawake, watoto pamoja na kuongeza kasi ya biashara ya kikanda. Alisema pia katika mkutano huo wanatarajia kujadili namna ambavyo nchi ya Burundi inaweza kuruhusiwa kujiunga kuwa mwanachama wa SADC.

Awali, akizungumza aliyekuwa mwenyekiti wa kamati hiyo, Ndaitwah, alitoa pole kwa serikali na kueleza kusikitishwa kwa ajali ya mlipuko wa lori la mafuta mkoani Morogoro iliyosababisha vifo vya watu zaidi ya 75 na wengine kadhaa kujeruhiwa kwa moto.

Alisema yeye ni mwenyeji nchini kwa kuwa anakumbuka ameishi miaka ya 1980 na alijulikana kwa jina la 'Mama Swapo' hivyo kuwa Dar es Salaam anajiona kama yupo nyumbani kwake.

Alisema anashukuru kwa hatua zilizofikiwa katika kutekeleza malengo ya mkutano wa 38, ambao ulikusudia kuangalia maboresho na ujenzi wa miundombinu na uwezeshaji wa vijana.

Alieleza jinsi ambavyo SADC inashukuru uchaguzi uliofanyika katika nchi sita ambazo ni ESwatini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Jamhuri ya Madagascar, Muungano wa Comoros, Malawi na Afrika Kusini.

"Nazipongeza serikali na wananchi katika nchi nilizotaja kutokana na kufuata misingi ya demokrasia na kumaliza uchaguzi kwa amani," alisema.

HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka (katikati), akizungumza na wataalamu elekezi baada ya kumalizika kwa semina ya mafunzo ya siku tano iliyolenga kuwajengea uwezo wataalamu hao, kuhusu namna ya kufanya tathmini ya athari kwa mazingira (EIA), iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wa pili kushoto ni Meneja wa Tathmini ya athari kwa mazingira ( EIA) kutoka NEMC, Glory Kombe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ang'aka wabunge kukimbia wapigakura

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWENYEKITI wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, amesikitishwa na baadhi ya wabunge mkoani humo kushindwa kufanya mikutano ya hadhara ya kusikiliza kero za wapigakura wao na kuwaeleza wanavyotekeleza ahadi walizotoa uchaguzi mkuu uliopita wa mwaka 2015.

Alisema kuna baadhi ya wabunge mkoani humo wamekuwa akihangaika nao kila kukicha kuwaambia wakafanye mikutano ya hadhara ya kusikiliza kero za wapigakura wao.

Mlolwa alizungumza hayo juzi Kata ya Tinde, Shinyanga Vijijini, kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Jimbo la Solwa, Ahmed Salum wa kusikiliza kero za wananchi na kuwaelezea alivyotekeleza ahadi zake.

Alisema anampongeza mbunge huyo wa Jimbo la Solwakwa kufanya mikutano mingi ya hadhara jimboni kwake na amekuwa akiifanya mara kwa mara kwa kusikiliza kero za wapigakura wake na kuzitatua tofauti na wabunge wengine mkoani humo ambao wamekuwa hawafanyi mikutano na kukimbia wapigakura wao.

"Wananchi wa Tinde nimekuja kwenye mkutano huu kuangalia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na tuliowapa ilani ni madiwani, wabunge na rais, sasa tunaangalia je, wanafanya mikutano ya kusikiliza kero za waliotupa dhamana kwa Ahmed siyo mara yake ya kwanza ndiyo CCM tunataka wabunge wa aina hii," alisema Mlolwa.

"Wapo wabunge mkoani Shinyanga mpaka leo nahangaika nao ukiwaambia nenda ukafanye mikutano ya hadhara ya kusikiliza kero za wapigakura wako wanaogopa, hatutaki wabunge wa namna hii kwa serikali ya awamu ya tano, bali tunataka wabunge ambao wanashughulika na matatizo ya wananchi," aliongeza.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo hilo la Solwa, akiwa kwenye ziara yake ya siku tano jimboni humo, alisema mpaka sasa ameshatekeleza ahadi zake nyingi na kati ya vijiji 126 vya jimboni humo 18 tu ndiyo vilivyosalia kupata maji ya Ziwa Victoria.

Alisema kwa upande wa umeme wa REA, vijiji 78 vimeshavutiwa umeme kwa awamu ya kwanza na kusalia 48 ambavyo vitaingia kwenye awamu ya pili na kubainisha miradi mingine ikiwamo ya upauaji wa madarasa 50 kwa jimbo zima, miundombinu ya afya, barabara kwa sehemu zilizosalia hadi 2020 atakuwa amekamilisha.

# Zaidi ya wakulima 80,000 kunufaika mradi PASS

**Na Zuwena Shame**

WAKULIMA wadogo na wafanyabiashara nchini watafaidika na mikopo kutoka mradi mpya ulizinduliwa na taasisi ya kilimo ya PASS na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB).

Mradi huo mpya unaojulikana kama 'de-risk agricultural financing for smallholder farmers' (DAFS), unakusudia kuwawezesha wakulima wadogo kifedha na kuwekeza sekta ya kilimo kupitia mikopo ya miradi ya dhamana na malipo ya bima kwa kuzingatia mfumo wa kuhatarisha.

Katika mkataba uliotiwa saini kati ya PASS na AFDB, PASS inajukumu la kuangalia na utekelezaji wa mradi huo nchini na nchi zingine za kiafrika ikiwamo Ghana, Uganda na Zimbabwe.

Meneja wa AFDB nchini, Alex Mubiru na Mkurugenzi Mkuu wa PASS, walisema kuwa dhumuni la mradi huo hasa ni kukuza uhakika wa mazao kwa wakulima wadogo nchini na kupunguza masuala yanayotokana na mnyororo unaotokana na mabadiliko ya hali ya hewa na vile vile kukuza mikopo na uwekezaji katika sekta ya kilimo kupitia miradi ya dhamana.

Mradi huo utawezesha wakulima wadogo kupata mikopo ya kilimo. "Huu ni ukuaji mkubwa kwetu sisi PASS na pia tunashukuru kwa kupewa nafasi kuongoza mradi huu, tutafanya kazi pamoja na kushirikiana kwenye matokeo yetu mazuri na nchi zingine," alisema Bohay.

Mradi huo wenye thamani ya Dola za Kimarekani 980,000 unakadiriwa kudumu kwa muda wa miaka miwili na nusu.

PASS itakuwa inafanyakazi na taasisi mbalimbali ikiwamo kampuni ya bima na taasisi za mikopo ili kuwezesha uchukuaji kilimo na kupunguza upotevu wa mazao na kupunguza matatizo yanayosababishwa na mnyororo wa hali ya hewa.

Kwa upande wake Eric Chavez kutoka chuo cha Imperial cha Uingereza, alisema PASS inajukumu kubwa nchini kwenye sekta ya kilimo na inahusika na utoaji wa mikopo ya kilimo nchini, hivyo ni kazi kubwa kwao na vilevile ina uhakika itatimiza majukumu mradi chini ya uongozi wake.

Mradi huo unalenga wakulima wadogo na taasisi za wakulima katika nchi zilizokusudiwa.

"Hadi mwisho wa mradi huu, tunataka kuwa na wakulima 80,000 watakaonufaika," aliongeza Chavez.

"Mradi huu umeanzishwa ili kuwezesha wakulima wadogo kupata mikopo na kuwawezesha kujikita kikamilifu kwenye masuala ya kuongeza minyoro ya thamani mazao yao," alisema Mubiru.

Wadau wengine wakubwa katika mradi huo ni Benki ya Dunia (WB), Umoja wa Ulaya (EU) na Serikali ya Japani.

# Wafanyabiashara watakiwa kumchangamkia Wiki ya Kagera

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WAFANYABIASHARA wametakiwa kutumia fursa zinazopatikana katika nchi zilizozunguka Mkoa wa Kagera ili kusaidia ukuaji wa uchumi katika mkoa huo.

Ushauri huo umetolewa na mabalozi wa nchi tano zilizopakana na mkoa huo wanaowakilisha Tanzania kwenye mwanzo wa utambuzi wa fursa zinazopatikana mkoani humo katika Wiki ya Kagera.

Mabalozi hao ni Ernest Mangu anayewakilisha Tanzania nchini Rwanda, Luten Jenerali Paulo Meela (Congo), Dk. Azizi Mlima (Uganda), Dk. Pindi Chana (Kenya) na Dk. Edmund Kitokezi, kaimu balozi (Burundi).

Balozi Mangu anayewakilisha Tanzania nchini Rwanda, alisema wafanyabiashara waishio Mkoa wa Kagera wanatakiwa kuzitumia fursa zinazokosekana kuwa changamoto ya ukosefu wa bidhaa katika nchi nyingine.

Alisema Rwanda kuna uhitaji wa bidhaa za vyakula kwa sababu ya ufinyu wa ardhi ya kilimo nchini humo.

"Uhitaji wa bidhaa zinazotokana na kilimo kama ndizi, mchele, makopa na mahindi una fursa kubwa kwa kuwa nchi nyingine hazina maeneo ya kilimo," alisema Balozi Mangu.

Kwa upande wake balozi anayewakilisha Tanzania nchini Congo, Luteni Jenerali Meela, alisema bidhaa za viwandani kama chumvi, saruji na vifaa vya ujenzi ambavyo nchi zingine hupata changamoto kuvipata, zina fursa kubwa.

"Nitumie nafasi hii kuwaomba wafanyabiashara kujenga tabia ya kutoka kutembea mkaone fursa zilizopo Kivu pamoja na Goma ili kujifunza jinsi watu wanavyofanya biashara na kupata mawazo mapya ya kujiendeleza kiuchumi," alisema Meela.

Dk. Chana anayeiwakilisha Tanzania nchini Kenya, alisema ili kufanikiwa katika biashara ni muhimu kutumia mitandao ambayo inaweza kusaidia kupata taarifa ya bei ya bidhaa pamoja na wateja.

"Wafanyabiashara wa Kagera katika masoko ya mipakani ambayo ni ya kimataifa mnatakiwa kufuata taratibu za kuwa na vibali sio kwenda tu, vinginevyo mtajikuta mnakwenda katika biashara halafu mnarudi na bidhaa hizo, cha msingi tumieni mabalozi wa nchi husika ili msikwame katika biashara," alisema Chana.

## Waturuki waitwa kuwekeza Singida

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

SERIKALI imetoa wito kwa wawekezaji kutoka Uturuki kuwekeza kwenye sekta ya kilimo na ufugaji wilayani Singida ili kuwezesha upatikanaji wa ng'ombe na mbuzi wengi kutoka kwenye mashamba yaliyopo.

Akizindua kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Singida, Pascas Muragiri katika ugawaji kitoweo cha wanyama waliochinjwa kwa ajili ya kutolewa sadaka kusherehekea Sikukuu ya Eid-Elhaji, Katibu Tawala wa Wilaya ya Singida, Wilson Shimo, alisisitiza kwamba ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na Uturuki haukuanza leo, bali ulianza tangu uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Shimo alitumia uzinduzi huo kuwakaribisha wawekezaji hao kuja kuwekeza katika fursa zingine za kiuchumi na kiuwekezaji katika Wilaya ya Singida.

Akitoa taarifa fupi ya shughuli ya kuchinja iliyofanyika katika Msikiti wa Alshababu, Mtaa wa Unyakindi, Manispaa ya Singida, Mudiri wa Jimbo la Singida, Zuberi Saidi Mkoko, alifafanua kwamba katika siku ya kwanza ya zoezi hilo walichinja jumla ya wanyama 1,410 wakiwamo ng'ombe 160 na mbuzi 1,250, wakati kwenye msikiti wa Mtaa wa Misuna uliopo kituo kipya cha mabasi yaendayo mikoani walichinja wanyama 1,310 wakiwamo ng'ombe 60 na mbuzi 1,250.

Amiri wa Jumuiya ya Answari Suna Tanzania (JASUTA) Mkoa wa Singida, Yahaya Mohamed, alisema shughuli za uchinjaji na ugawaji wa kitoweo hicho wamekuwa wakiifanya kwa kuzingatia zaidi ubinadamu, na siyo masuala ya itikadi na kwamba watu watakaopata bahati ya kitoweo ni watu wa aina zote, wa dini zote, wa rangi zote na wa makabila yote.

# Rai kwa wanahabari kuelimisha jamii uvamizi malori ya mafuta

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

KUWAPO kwa matukio mengi ya ajali za malori nchini, vyombo vya habari vimeombwa kuwa na vipindi maalumu vya kuelimisha jamii athari za kuvamia malori ya mafuta yanapopata ajali pamoja na kuchota mafuta.

Wito huo umetolewa jijini hapa na Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza (MPC), Edwin Soko, na kusema kumbukumbu zinaonyesha kuwapo kwa matukio mengi ya ajali za malori kupata ajali na wananchi kufariki walipokuwa wanachota mafuta. Alisema, matukio kama hayo yalitokea mwaka 1998 lori la mafuta lilipata ajali eneo la Isongole Mbeya na watu walifariki dunia wakiwa kwenye harakati za kuchota mafuta, 2008 eneo la Mdaula Chalinze karibu na Morogoro, 2010 eneo la Manyoni 2013, eneo la Mbagala jijiji Dar es Salaam na la Jumamosi eneo la Msamvu mkoani Morogoro.

"Mtiririko wa matukio haya unatia shaka na kutuaminisha kuwa hakuna elimu ya kutosha juu ya athari za vitendo vya kuvamia malori na kuchota mafuta yanapopata ajali, hivyo ni muda mwafaka kwa vyombo vya habari kutoa uchechemushi na kuelimisha jamii juu ya jambo hili, pia tunato pole kwa ndugu zetu, Watanzania wenzetu waliopoteza maisha katika ajali ya Msamvu na majeruhi wapone na kurejea katika shughuli zao za kila siku," alisema Soko.

Pia alivitaka vyombo vya habari kuacha mara moja kuchapisha picha zenye ukakasi (kutumia picha ya maiti iliyo haribika) kwani kwa kufanya hivyo ni kuvunja misingi ya uandishi wa habari na kuchochea maumivu kwa msomaji.

"MPC inawakumbusha waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini hasa wanaofanya kazi ya kuchapisha, kutangaza na kurusha habari katika mitandao ya kijamii (Online Journalism) kuzingatia weledi na taaluma katika kupiga picha za miili ya marehemu walio ungua katika ajali," alisema.

Aidha, baada ya kutokea kwa tukio la ajali hiyo MPC imefanya tathimini ya namna vyombo vya habari vilivyochapisha habari hiyo ikiwamo magazeti, radio, runinga na mitandao ya kijamii na kushuhudia picha za watu waliofariki kwa kuungua moto zikirushwa kwenye vyombo ovyo, jambo ambalo ni kinyume cha maadili ya taaluma ya uandishi wa habari na upashaji habari kwa njia ya picha.

"Kwa kufanya hivyo ni kosa la kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Mawasiliano na Posta (maudhui ya mtandaoni) Epoca 2018 kifungu cha 5(1) A, B, C, D, E, na F, endapo utakiuka vifungu vilivyoainishwa katika sheria hiyo basi utakuwa umetenda kosa na unaweza kutozwa faini sio chini ya shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi kumi na miwili," alisema.

Aliwataka waandishi wa habari kutimiza vyema majukumu yao ya msingi ya kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha, kuonya sanjali na kufanya ukosoaji jengefu bila kuvunja maadili pamoja na kuwa mabalozi wa kuielimisha jamii kutumia vyema mitandao ya kijamii hasa uandishi wa kiraia.



Msamaria mwema Zuberi Fadhili (kushoto), akikabidhi msaada wa matofali 1000 na mifuko ya saruji 20 kwa Diwani wa Kata ya Misozwe, wilayani Muheza Mkoa wa Tanga, Jestina Mntangi, kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa madarasa katika Shule ya Sekondari ya Kata ya Misozwe wilayani hapa juzi. Kulia ni Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Judithi Madudu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wadau wa elimu wajadili shule kuongeza kidato 6

**Na Sabato Kasika**

WADAU wa elimu wa Wilaya ya Musoma mkoani Mara, wameanza vikao vya kuangalia uwezekano wa kutekeleza mradi wa kuongeza kidato cha sita kwa shule za jimbo la Musoma Vijijini.

Mchakato huo ambao unalenga kuwa mchepuo wa masomo ya sayansi, unashirikisha Mkuu wa Wilaya, Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo na Madiwani wa Halmashauri ya Musoma Vijijini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Musoma, John Kayombo, alisema mbali na shule za serikali, wanakaribishwa uanzishwaji wa kidato cha sita kwa shule binafsi mkazo mkubwa ikiwa kwenye masomo ya sayansi.

Alisema ameshafanya vikao na wananchi na viongozi mbalimbali akiwashawishi kuboresha miundombinu kama maabara, ujenzi wa mabweni ya baadhi ya sekondari na kupendekeza zipanuliwe na kuanza kutoa elimu ya kidato cha tano na cha sita ya masomo ya Sayansi.

"Tunasisitiza kuboresha elimu ya Sayansi kwani taifa litakalokuwa na ubunifu mkubwa kwenye teknolojia na Sayansi ndilo linatawala uchumi wa dunia yetu kwenye karne hii na zijazo," alisema Kayombo.

Kayombo alizitaja sekondari za Bugwema, Mtiro, Mugango na Mkirira kwamba ziko juu kwenye orodha ya kuweza kuanzisha kidato cha sita zikiwa na mchepuo wa masomo ya Sayansi.

"Sekondari nyingine pia zina nafasi sawa na hizo iwapo miundombinu ya elimu ya kuanzisha kidato cha sita itakuwapo, hivyo kinachotakiwa ni miundombinu inayohitajika kukidhi vigezo vya elimu ya juu," alisema.

Alifafanua kuwa Musoma Vijijini ina shule za sekondari 18 za serikali na mbili za binafsi, lakini za kidato cha sita mbili tu ambazo ni Kasoma ambayo ni ya serikali na Nyegina inayomilikiwa na Kanisa Katoliki.

"Wananchi, madiwani na viongozi wao wengine, kwa kushirikiana na serikali na mbunge wao wa jimbo wanajenga sekondari mpya nane, lengo kuu likiwa ni kuboresha elimu lakini bado kuna haja ya kuwa na shule nyingi zenye kidato cha sita," alisema.

# DC awasifu viongozi kuhamasisha maendeleo

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

MKUU wa wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, amewashukuru viongozi wa dini kwa kusaidia serikali kuhamasisha maendeleo kwa haraka kwenye jamii wanazoziongoza.

Hayo alisema jana Kitundu katika Baraza la Idd, lililofanyika mjini Babati katika uwanja wa Kwaraa.

"Hakika bila ninyi viongozi wa dini kufanya kazi nzuri ya kuwaambia wananchi kuhusu maendeleo , kazi yetu sisi viongozi wa serikali ingekuwa ngumu sana maana tusingeweza kufanikisha wala kutawala kwa amani,"alisema Kitundu

Aidha, aliwataka viongozi wa Kiislamu kuendelea kuwahimiza vijana kuepuka kufanya vitendo viovu kama vile wizi na kucheza kamari, bali wafanye kazi zilizo halali kwa kufuata sheria na kutumia vitambulisho vya wajasiriamali.

Mkuu wa wilaya aliwaomba kuendelea kuwahamasisha wananchi kumuunga mkono Rais John Magufuli, katika jitihada zake za kuiletea nchi maendeleo na pia kuhimiza waumini wao kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji. "Kwani Rais wetu anastahili kuungwa mkono kwa sababu ni mchapakazi na hivyo tumchague na kumpa wasaidizi wake uchaguzi wa mwaka huu wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani,"alisema

Shekhe wa Mkoa wa Manyara, Mohamed Kadidi, aliwataka waislamu kujitathimini wamefanya nini kwa mwaka mzima na wajikite kwenye mipango ya maendeleo na si vinginevyo. Shekhe Kadidi aliwaambia kuwa misikitini siyo ni sehemu ya kufanya migogoro au fitina, bali wanatakiwa kupendana na kuchapa kazi kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao na taifa pia.

Katibu wa Baraza la Waislamu (Bakwata) Wilaya ya Babati , Abdi Issuja, akisoma risala alisema miongoni mwa changamoto inayowakabili ni ukosefu wa usafiri na kuwaomba wadau kuchangia, ili waweze kuwafikia waumini kiurahisi. Baada ya risala hiyo viongozi wa serikali na wa dini walichangia fedha taslimu Shilingi 460,000 na ahadi zaidi ya Shilingi 2,000,000 kwa ajili ya kumaliza deni la 5,000,000 la gari waliyonunua kwa ajili ya kufanya huduma kwa waumini wao.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Daniel Ole Materi, akizungumza kwenye kikao cha viongozi wa tarafa ya Terrat, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wafugaji wahimizwa kusomesha watoto

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAFUGAJI katika mikoa mbalimbali wameshauriwa kuwekeza zaidi katika elimu kwa watoto wao bila kujali jinsia kwani wote wana haki sawa ya kuondokana na ujinga.

Aidha, wamekumbushwa kuachana na mfumo dume wa kuwapeleka watoto wa kike machungani na kuwapendelea zaidi watoto wa kiume. Hayo yalisemwa jana na mdau wa elimu ,Paulo Ndari, wakati akizungumza katika sherehe za kimila za kumsimika kiongozi wa boma katika Kijiji cha Engaroji Kata ya Lepuko Wilayani Monduli mkoani Arusha.

Alisema kuwa,jamii nyingi za wafugaji wamekuwa wakiendekeza mfumo dume, kwa kuwabagua watoto katika utoaji wa elimu, ambapo wamekuwa wakiwapendelea watoto wa kiume, huku watoto wa kike wakiishia kuchunga na kubaki majumbani. Alisema umefika wakati sasa wa jamii hiyo kuachana na mifumo dume, badala yake waweke katika elimu kwa watoto wote bila ubaguzi, kwani zawadi pekee wanayotakiwa kupewa watoto hao ni elimu na sio vinginevyo.

"Sisi viongozi katika jamii yetu tuna majukumu makubwa sana ya kuhakikisha watoto wote wanapata haki sawa, huku tukiweka sheria zetu za kuwabana wale wote wanaokiuka sheria hizo, ikiwemo suala zima la elimu na tumepiga marufuku kwa mtoto yoyote kwenda machungani, hivyo watoto wote lazima waende shuleni na akitokea mtu yeyote amekiuka anapigwa faini,"alisema Paulo.

Alifafanua kuwa, bado kuna changamoto kubwa ya elimu katika jamii hiyo ya kifugaji kutokana na wengi wao kutojua umuhimu wa kuwekeza katika elimu, ambapo wamekuwa wakiendelea kuelimisha jamii yao kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali wa kimila .

Kwa upande wake kiongozi wa kimila Laigwanani wa kijiji hicho, Bukula Narida, alisema kuwa,wamekuwa wakichagua viongozi hao katika jamii zao, kwani wana wajibu mkubwa na mchango katika kuleta mabadiliko ndani ya jamii.

Aidha, alisema kwa kutumia sheria zao ndogo ndogo walizojiwekea viongozi hao wanahusika kudhibiti mila zisizo rafiki na kuhimiza masuala ya serikali yanayosimamia maendeleo ya jamii.

Narida aliongeza kuwa,kupitia viongozi hao jamii hiyo ya wafugaji imeweza kuelimika na kupeleka watoto shuleni, japo bado kuna changamoto katika kuwepo kwa haki sawa kwa watoto wote bila kuwepo kwa ubaguzi wowote.

"Tumejiwekea sheria ndogondogo za kuwabana wote wanaokwenda tofauti na makubaliano yetu na zimekuwa zikisaidia sana, kwani yoyote anayeenda kinyume huwa anapigwa faini, kulingana na sheria zetu na wengi wao wamekuwa wakijirekebisha sana,"alisema.

Mwananchi mwingine, Sanare Mollel, alisema kuwa, uwepo wa viongozi hao katika jamii unasaidia kushawishi watu katika suala zima la maendeleo, pamoja na kutatua migogoro mbalimbali inayotokea ndani ya jamii kabla ya kwenda kwenye ngazi za juu, kwani viongozi kama hao ndio wanaaminika zaidi tofauti na wengine hasa katika jamii za kifugaji.

Kiongozi mwingine wa kimila Laigwanani, Loshiro Mollel, alizitaka jamii mbalimbali kuendelea kuzienzi na kuzithamini mila na desturi zao, kuhakikisha zinadumishwa ili ziendelee kutumiwa na vizazi vijavyo kwa lengo la kujiletea maendeleo katika jamii yao.

## Wananchi waiomba serikali umeme

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WAKAZI wa Kata ya Terrat wilayani Simanjiro mkoa wa Manyara, wameiomba serikali kufikisha umeme kwani viwanda na miradi ya maendeleo inakwama.

Waliomba kupitia awamu ya tatu ya mpango wa usambazaji wa nishati ya umeme vijijini wapate nishati hiyo, ili visima na viwanda vidogo viweze kukamilika na kuwanufaisha kiuchumi.

Wananchi hao waliyasema hayo juzi wakati wakizungumza kwenye kijiji cha Terrat wakati wa kikao cha kuzungumzia uchaguzi wa serikali za mitaa na kumpongeza Rais John Magufuli kwa kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo ya kimkakati.

Katika kikao hicho kilichohusisha viongozi wa CCM wa Kata za Komolo, Terrat na Oljoro namba tano za Tarafa ya Terrat, walisema umeme ukiwafikia watanufaika zaidi tofauti na sasa wanapotumia nishati ya umeme wa juaa -sola na jenereta.

Diwani wa Kata ya Terrat, Jackson Ole Materi, alisema katika mpango wa visima 20 vya wilaya hiyo, kata hiyo ilifanikiwa kupata visima viwili ila wanashindwa kuviendesha kutokana na ukosefu wa nishati ya umeme.

"Rais John Magufuli kupitia ilani ya CCM anatekeleza jukumu la kumtua mwanamke ndoo kichwani lakini tunashidwa kutekeleza hilo kwa ukosefu wa umeme, ila tuna matarajio utafika na maji yatakuwepo kwa wingi," alisema Ole Materi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa wa Wilaya ya Simanjiro Daniel Ole Materi alisema, kiwanda cha maziwa kimeshidwa kufanya kazi kutokana na kutowepo kwa nishati ya umeme. "Gharama za umeme wa jua na jenereta ni ghali mno katika kuendesha viwanda, tunaiomba serikali ifanikishe hili suala la umeme wa vijijini Rea kwani ni hitaji kubwa kwa jamii," alisema Ole Materi.

Ofisa Tarafa ya Terrat, Lekshon Kiruswa alisema suala la mradi wa Rea awamu ya tatu kwenye eneo hilo unaendelea vizuri, kwani vijiji vingi katika tarafa hiyo vimepata umeme.

Kiruswa alisema kata za Oljoro namba tano na Komolo zimeshapata nishati ya umeme na hivi sasa unaelekea Kijiji cha Nadonjukin, kisha utaingia Kata ya Terrat na kuendelea kusambazwa katika vijiji vya eneo hilo.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha hadi ifikapo mwaka 2021 vijiji vyote nchini viwe vimefikiwa na nishati ya umeme wa Rea na kutokana na kasi kubwa inavyokwenda utekelezaji wake utafanikiwa.

Mkazi wa Kijiji cha Terrat Jacob Laizer alisema endapo umeme ungefika katika eneo hilo hivi sasa kungekuwa na maendeleo makubwa mno.

"Kuna wafugaji wana uwezo wa kufungua viwanda vidogo ili kumuunga mkono Rais John Magufuli katika dhana ya Tanzania ya viwanda, ila wanashindwa kutokana na ukosefu wa nishati ya umeme," alisema Laizer.

## Magugu maji kuwa historia

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

WAKATI serikali ikiwa inaendelea na mkakati wake wa kutekeleza mradi wa kuyahifadhi maziwa madogo, Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, inakusudia kuanzisha mradi wa kuyaangamiza magugu maji yanayozuia shughuli za kiuchumi katika Ziwa Jipe.

Uthibitisho rasmi wa kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo wa kuzuia magugu maji katika ziwa hilo, umetolewa na halmashauri ya wilaya hiyo kupitia tovuti ya serikali.

Jana, alipotafutwa kwa njia ya simu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Zefrin Lubuva, kufafanua kuhusu mkakati huo, simu yake ilikuwa ikiita bila majibu.

Tovuti hiyo inaonyesha kuwa katika ziwa hilo linalotoa fursa ya uvuvi kwa wakazi wanaoishi kando kando mwa Ziwa Jipe, shughuli za kiuchumi hasa uvuvi zimepungua kwa sababu ya magugu maji ambayo yamesababisha pia kupungua kwa kina na upana wa ziwa.

Mbali na changamoto hiyo, halmashauri hiyo imeanza kuwakaribisha wazawa na wageni kutoka nje ya nchi kwenda kuwekeza kwenye shughuli za uvuvi kama kuvua kwa kutumia vifaa vya kisasa, kujenga masoko ya kisasa ya samaki na kujenga viwanda vya kusindika samaki.

Maeneo mengine inayovutia uwekezaji ni uanzishaji wa mabwawa ya samaki kwenye maeneo yenye maji kama Kata za Kileo, Kivulini, Kirya, Lang'ata na baadhi ya maeneo ya ukanda wa milimani.

Kutokana na mpango huo, baadhi ya wavuvi waliozungumza na Nipashe, Aziz Mshana alisema kwa kuwa ziwa hilo ni rasilimali muhimu na hivyo ni lazima kuwe na mpango wa muda mfupi na ule wa muda mrefu wa kulinusuru.

Aidha, mkazi wa Jipe, Natujwa Alli, alisema Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, inapaswa kuja na mpango maalum wa kuitangaza Jipe kuwa eneo mahsusi ama nyeti la kimazingira.

Alisema ni vyema ofisi hiyo ikaliweka ziwa hilo chini ya uangalizi maalumu na kuweka masharti ya matumizi bora ya eneo hilo.

# Wataka utafiti wa kina Ziwa Chala

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

BAADHI ya wadau wa sekta ya utalii mkoani Kilimanjaro, wameishauri Wizara ya Maliasili na Utalii, itenge fungu maalum kwa ajili ya kufanya utafiti wa kisayansi utakaothibitisha kina halisi cha Ziwa Chala ambalo linatembelewa na idadi kubwa ya wageni kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Ziwa hilo liko mpakani mwa nchi ya Kenya na Tanzania, takribani kilomita 45 kutoka barabara kuu ya Moshi-Taveta.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana baada ya kufanya utalii wa ndani, wakati wa maadhimisho ya Sikukuu ya Eid el Hajj, akiwamo mwongoza watalii Vallerian Mboya, walisema licha ya ziwa hilo kudaiwa kuwa na muunganiko wa kijiolojia na Mlima Kilimanjaro, iko haja kwa serikali kuwa na kanzi data inayoonyesha kina halisi cha ziwa hilo ili kutoa fursa ya watalii kupata taarifa sahihi.

"Ukiangalia karibu asilimia 60 ya watalii wanaotembelea Ziwa Chala kwa upande wa wilaya ya Rombo wanatuuliza maswali kuhusu kina cha ziwa hili lakini hatuna majibu. Tunaishia kuwaeleza kwamba bado hakujafanyika utafiti kujua ukubwa wake kwenda chini," alisema Mboya.

Hata hivyo, inaelezwa kwamba ziwa hilo lina takribani kina cha mita 3,000 lakini hakuna utafiti wa kisayansi unaothibitisha urefu wa ziwa hilo ambalo lina mvuto wa kipekee kwa kuwa hakuna mto unaoingiza wala kutoa maji. Ni ziwa lenye maji baridi na samaki wa maji baridi.

Naye Isaack Nuru maarufu kama Zedane, ambaye ni mwongoza watalii katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, akiwa katika ziwa hilo, alisema pamoja na kwamba uko mwamko mkubwa wa wananchi kutembelea vivutio vya utalii, ni vyema serikali ikafanya utafiti huo kujiridhisha.

Katika tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, taarifa iliyowekwa inaeleza kuwa eneo la Ziwa Chala kuna hekta zipatazo 23 kwa upande wa Tanzania ambazo ni mashamba yanayomilikiwa na watu binafsi ambako kunaweza kutumika kwa ujenzi wa hoteli na 'campsite'.

Moja ya maajabu ya Ziwa Chala ambalo ndilo kivutio kikuu cha utalii katika Wilaya ya Rombo, ni uwezo wake wa kutopungua maji, wala kuongezeka kipindi cha mvua au ukame, huku kukiwa hakuna mto unaoingiza maji katika ziwa hilo.

Ziwa hilo lililoko katika Kijiji Malowa, lina ukubwa wa hekta 421, huku utafiti mbalimbali wa kitaalamu ukieleza chanzo chake ni kimetokana na mlipuko wa volkano uliosababisha ardhi kudidimia na hatimaye kuwa na bonde kubwa la maji yakitokea chini kwa chini kwenye miamba.



Mwonekana wa sehemu ya ujenzi unaoendelea wa barabara za mpishano (Ubungo Interchange), katika eneo la mataa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Hai yatenga eneo la uwekezaji

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro imetenga eneo la ukanda maalum wa viwanda (EPZ) lenye ukubwa wa hekta 463 kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vikubwa.

Taarifa iliyothibitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Hai na kuwekwa katika tovuti ya serikali, inaeleza kuwa eneo hilo liko katika barabara kuu ya Moshi- Kilimanjaro. Kutokana na taarifa hiyo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, alipoulizwa na Nipashe ni eneo gani ambalo ni mahususi kwa ajili ya uwekezaji huo, alisema katika eneo la Mashine Tools, njia panda ya Machame. Eneo hilo limetengwa hekta 430 kati ya 463.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, eneo hilo hivi sasa limewekwa wazi kwa ajili ya uwekezaji wa bidhaa za viwandani.

Kuhusu uwekezaji katika sekta ya utalii, alisema wilaya hiyo ina vivutio muhimu ambavyo ni pamoja na chemuchem ya Chekimaji inayotoa maji ya moto.

"Hai yako pia maeneo ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji wa hoteli za kitalii hasa ukizingatia ni eneo lililo karibu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Hivi sasa tunahangaika kutafuta wawekezaji ndani na nje ya nchi ambao watakuja kuwekeza hapa kwa ajili ya kuchochea sekta ya utalii," alisema.

Kuhusu mchakato wa utekelezaji wa mradi mkubwa wa kimkakati wa ujenzi wa soko la kimataifa la nafaka ambalo uwekezaji wake utagharimu Sh. bilioni 11 katika eneo la Kwa Sadala, Ole Sabaya alisema unaendelea kwa kasi na wakati wowote atatangaza kuanza kwa ujenzi wake. Soko hilo ambalo limepewa jina la 'The Magufuli International Complex Centre' (MICC-Hai), litajengwa karibu na kiwanda cha Arsho au mkabala na njia panda ya kwenda Masama. Inaelezwa kuwa soko hilo ambalo litakuwa na kazi ya kuongeza thamani ya mazao, kuchochea pato la mkulima na kuingizia serikali kodi, litakuwa na eneo maalum la viwanda vya usindikaji, eneo la utalii zikiwamo hoteli, kituo cha habari za utalii, migahawa ya kisasa na maeneo ya huduma za kibenki.

Pia litakuwa na ofisi za bima, kumbi za kisasa za mikutano na maduka makubwa. Muda ambao mradi huo utatekelezwa ni miaka miwili na utagawanyika katika awamu tatu.

Ukurasa 18



BETTY BIGOMBE; Mwanamke aliyemshawishi Kony kukutana na Museveni Uganda

Magufuli na safari ya kuiongoza SADC



Ukurasa 15


Kimataifa



Wanajeshi, waandamanaji Sudan waafiki kutekeleza makubaliano

Ukurasa 17

siasa
JUMATANO AGOSTI 14, 2019
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe



Mwaka unakatika, DRC waanza kujadiliana orodha ya mawaziri

Ukurasa 14

## BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-9

PIUS Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa Serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Pia Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu na kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa na leo hii tunaendelea kutokea tulipoishia wiki iliyopita. Endelea na sehemu hii ya tisa ya kitabu hicho inayoanzia na 'Kuhusu Madai ya Tume ya Nyalali'...

(ii) Kuhusu madai ya Tume ya Nyalali

Mwalimu Nyerere aliyapuuzilia mbali kwa maneno aliyoyaandika katika kitabu chake kiitwacho "Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania:"

- "Lakini, ukweli wa jambo hili unabaki palepale. Wananchi wa Tanzania hawadai serikali ya Tanganyika. Na mimi nasema, ukifufua Tanganyika, utaua Tanzania. Fahari wawili hawakai zizi moja. 'Yeltsin' wa Tanganyika ataua Muungano.

(ii) Kuhusu madai ya Azimio la Bunge la kutaka iundwe

Endelea 16



Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

Hiki ndicho mwenyekiti mpya wa SADC anachoingia nacho Ukurasa 20

# Mwaka unakatika, DRC waanza kujadiliana orodha ya mawaziri

Na Anil Kija



Rais wa zamani wa DRC, Joseph Kabila (aliyenyoosha mkono), anadaiwa kuchangia ucheleweshaji wa kuundwa kwa Baraza la Mawaziri nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

KIELELEZO cha msingi kuwa uchaguzi mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ulivurugwa na kutoa matokeo yasiyo sahihi ni kushindwa kwa Rais Felix Tshisekedi kuunda serikali tangu achaguliwe au atangazwe mshindi mwezi Januari mwaka huu.

Ilitazamiwa kuwa hadi Machi angekuwa ameunda serikali lakini alikwama kabisa, na hadi kufikia mwezi Mei akawa ameafikiana na rais aliyestaafu kidogo tu, Joseph Kabila, kuwa msaidizi wa karibu wa Kabila ndiye achukue nafasi ya uwaziri mkuu.

Mwishoni mwa Julai walikubaliana idadi ya mawaziri watakaokuwako serikalini, na wakati Agosti inaanza wanajadili majina ya mawaziri.

Taarifa kutoka Kinshasa zinaonyesha kuwa majadiliano ya kuunda serikali tangu mwanzo yanafanywa na Tshisekedi na Kabila moja kwa moja, siyo kupitia umoja wa upinzani na hata makundi ya vyama bungeni.

Ila mwafaka wowote unaopendekezwa lazima ufikishwe bungeni uthibitishwe, na ndiyo Tshisekedi alipoanza kukwama, kwani kundi la Kabila lina wabunge wengi.

Halafu isitoshe wabunge wa uliokuwa upinzani wakati wa Kabila wamegawanyika kutokana na kutangazwa Tshisekedi kuwa mshindi, badala ya Martin Fayulu aliyeonekana na makundi tofauti ya waangalizi wa kura ndani na nje ya DRC waliokuwapo kuwa alishinda.

Hali ya kushindwa kuunda serikali na mparaganyiko wa utii bungeni ambako kuna kambi kadhaa hasimu ni ushindi kwa Kabila ambaye ameondoka Ikulu, lakini hakuna kitu kilichobadilishwa hadi sasa, na saini yake inatakiwa ili chochote kifanyike.

Bila wabunge wake kumuunga mkono Tshisekedi, Rais anakuwa hana uwezo wa kupitisha chochote, wakati ambapo kuna kila ishara kuwa kuna anazo hitilafu si ndogo siyo tu na Kabila mwenyewe bali zaidi tu na wasaidizi wake, hasa mawaziri waliokuwapo, au wanaoendelea kubakia hadi wengine watangazwe.

Ingekuwa ni miaka ya zamani, jeshi tayari lingekuwa limeshapindua kuondoa mkwamo serikalini, si siku hizi.

Katika ishara kuwa Kabila anahakikisha anashika nchi kama mwanzo hata kama itachukua mwaka mzima kuunda serikali, taarifa zinasema kuwa amekazania kuwa kundi lake la wabunge litashika nafasi tatu kati ya nne za wizara muhimu zaidi, yaani ulinzi, fedha na sheria.

Ina maana wizara nyingine muhimu itakayokwenda kwa kundi la Tshisekedi ni mambo ya ndani na mambo ya nje, licha ya kuwa nafasi ya waziri mkuu pia itakwenda kwa kundi la Kabila.

Ni gharama kubwa ya kuviliwa madaraka halisi ya urais kwa Tshisekedi, anayolipa kwa kupewa nafasi hiyo.

Nguvu kubwa ya Kabila inaonekana iko serikalini ambako ameisimamia kwa miaka 18 kama rais, hivyo ameteua wakuu wa taasisi zote nchini na watangulizi wao, 'kuanzia vizazi vya tatu na vya nne.'

Kwa maana hiyo bila rais aliyechaguliwa kwa nguvu na wananchi, achukue madaraka kamili, haitakuwa rahisi kupangua 'le systeme Kabila,' kama ambavyo inaitwa kwa Kifaransa.

Isitoshe, akishateuliwa waziri mkuu itakuwa lazima kwa rais kumshirikisha kwa kila atakalotaka kufanya hasa katika kubadili washika madaraka maeneo tofauti, pale ambapo hawajafikia umri wa kustaafu, au pale anapotaka kutumia madaraka yake kuwastaafisha.

Na kama ilivyokuwa Sudan Kusini, katika mvurugano wa makundi yenye nguvu, upande wa kundi la mshindani-rais wanamsikiliza kiongozi wao, kwa maana hiyo Kabila, kwa uamuzi wowote ule; rais hawatishii...

Fununu zinasema kuwa Kabila ametaka pia wafuasi wake wapewe wadhifa wa wizara inayosimamia hisa za serikali, inayoshika kampuni za madini ambako kampuni kubwa ya shaba na 'cobalt' Gecamines, ina ubia na Glencore na Molybdenum ya China.

Pamoja na mambo ya nje na mambo ya ndani, bajeti na uchumi pia vitashikwa na kundi la Tshisekedi, ambao ina maana mgao wa ruzuku majimboni na sera za uwekezaji, wakati masuala ya fedha, benki na Benki Kuu, yanabaki chini ya kundi la Kabila.

Kundi la Kabila lilifurahia matokeo ya mazungumzo hayo na azma ya kuunda baraza jipya la mawaziri ambako ndio watakaotawala.

Jumla ya nafasi za uwaziri zinazotazamiwa ni 65, wakiwa ni 42 kutoka kundi la Kabila na 21 kutoka kundi la Tshisekedi, idadi ambayo inazidi ukubwa wa mabaraza ya mawaziri wakati wa Kabila.

> Katika ishara kuwa Kabila anahakikisha anashika nchi kama mwanzo hata kama itachukua mwaka mzima kuunda serikali, taarifa zinasema kuwa amekazania kuwa kundi lake la wabunge litashika nafasi tatu kati ya nne za wizara muhimu zaidi, yaani ulinzi, fedha na sheria.

Tayari Tshisekedi alishamtangaza Sylvestre Ilunga, swahiba wa Kabila kuwa waziri mkuu na makundi hayo mawili yakaunda umoja bungeni.

Tatizo limekuwa kutokana na hali ya kutokuaminiana kuhusu nani achukue wizara gani, kwani Tshisekedi amewahi kuwakosoa mawaziri wa Kabila kuwa wana tabia ya umila na ni wala rushwa, ina maana hana nia ya kuwatupa.

Mkwamo huo wa kuunda serikali na nguvu ya Kabila inayoonekana wazi imezua vurugu za hapa na pale lakini bado siyo za kina, kwani kuna shauku maeneo tofauti ya nchi nini ambacho serikali mpya inaweza kufanya.

Lakini historia inaonyesha kuwa mwelekeo wa kundi la Kabila hautabadilika na watataka wafanye watakavyo kwani bado ndio wenye wingi wa viti bungeni, na pande tofauti za upinzani hazielewani kutokana na 'usaliti' wa kukubali kuvuruga kura na kuteua mshindi asiye na wingi wa viti bungeni au idadi ya kura za wananchi.

Ina maana kuna uwezekano mkubwa wa serikali hiyo kushindwa kufanya kazi, au kukwama uchaguzi baadaye.

Inawezekana hali ya mkwamo ikaendelea kufukiwa fukiwa hadi uchaguzi mkuu miaka mitano baada ya ule wa Januari 2019, kwa sababu uwezekano wa ushindi wa Tshisekedi endapo akiamua kuitisha uchaguzi mwingine sasa, iwe ni kwa urais au kwa wabunge ni mdogo sana.

Itakuwa imeeleweka kuwa hakuwa mpinzani halisi bali mshirika msiri wa utawala ulioko madarakani.

Na isitoshe ushawishi wa wale waliovuna wakati wa Kabila utakuwa umepungua, pale wananchi watakapoelewa kuwa suala siyo kuwa na rais mwingine endapo hana wingi wa viti bungeni.

Ni kiashiria kuwa serikali ya Kabila kwa kivuli na ushirika wa Tshisekedi inaweza kudumu kwa miaka kadhaa kama itajitahidi, lakini inaweza kuvurugwa na maandamano ambayo hata sasa yanatokea lakini hayajashika kasi.

Ila kwa vile DRC ina tatizo la kuwepo kwa mwelekeo halisi wa kitaifa katika suala lolote lile, haitakuwa rahisi wananchi kujipanga nyuma ya Fayulu kama mgombea aliyepokonywa ushindi, kwani hata hivyo wingi wake wa viti bungeni ungesuasua.

Ila angeweza kuunda serikali na mojawapo ya makundi ya upinzani, hivyo tatizo ni kuwa licha ya 'maandamano yasiyoisha' wakati ule, wapigakura wa DRC walikuwa bado hawajaiva kuchagua serikali mpya kwa maana ya rais pamoja na wabunge.

Kabila ana viti vingi bungeni, hali halisi inayomwezesha apokonye au aelekeze nini kifanyike katika ngazi ya urais, kwani haina mizizi.

# Magufuli na safari ya kuiongoza SADC

• Changamoto na mafanikio yake

**Na Mashaka Mgeta**

AGOSTI 18 mwaka huu, Rais John Magufuli, atakabidhiwa ki'rungu' kinachoashiria kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Hii itakuwa ni mara ya pili kwa Rais Magufuli kuongoza jumuiya ya kikanda katika wadhifa huo, ikirejea Machi 2016 alipochaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Hii ni fursa inayoashiria bahati kwa kiongozi wa nchi kushika wadhifa huo katika kanda tofauti katika awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi.

Kwa maana mathalani kati ya nchi 16 wanachama wa SADC, kila Rais anashika wadhifa wa uenyekiti kwa mwaka mmoja na hivyo kufanya, ikiwa vigezo vitakidhi kwa mataifa yao na pasipo kuwapo mwanachama mpya, kila nchi kushika wadhifa huo baada ya miaka 15.

Ni dhahiri kwamba kwa nchi kama Tanzania yenye ukomo wa urais wa miaka 10, inawezekana Rais akamaliza muda wake pasipokuwa sehemu ya walioshika wadhifa huo.

Safari hii Rais Magufuli anakuwa Mwenyekiti wa SADC, je, ni mambo gani anayokabiliana nayo kwa kipindi hicho cha mwaka mmoja?




Baadhi ya marais wa nchi wanachama wa SADC, Rais Felix Tshisekedi wa DRC (wa kwanza kulia), Rais John Magufuli wa Tanzania (wa pili kulia), Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini (mbele aliyekunja mikono), Rais Emerson Mnangagwa wa Zimbabwe (kushoto), Rais wa Malawi, Peter Mutharika (nyuma kushoto) na Rais wa Namibia Hage Geingob (katikati nyuma). **PICHA: MTANDSAO**

**FURSA ZA KIKANDA**

Moja ya hoja iliyoshamiri kwa muda mrefu katika uendeshaji wa SADC na ambayo Rais Magufuli atakutana nayo, ni namna ya kuziwezesha nchi wanachama kuwa washirika wakuu wa biashara na shughuli nyingine miongoni mwao.

Hata hivyo, tayari Rais Magufuli ameshaonyesha mwelekeo wa uongozi wake kupitia hotuba aliyoitoa wakati akizindua wiki ya maonyesho ya viwanda kwa nchi za SADC yaliyofanyika jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

Rais Magufuli anagusia umuhimu wa masoko kwa ajili ya bidhaa zinazochagiza biashara na kukuza uchumi kwa wakazi na nchi za SADC, ili kuepuka hatari ya 'kukimbilia' masoko ya nje yenye masharti, ushindani na gharama kubwa.

Ingawa hoja hii imewahi kutajwa na marais waliowahi kushika wadhifa huo kwa nyakati tofauti, lakini Rais Magufuli amezitaka nchi hizo kupeana fursa zenyewe kwa zenyewe, hasa kwa masuala ya biashara.

Akasema moja ya njia bora za kuyafikisha mataifa hayo katika ushirikiano wenye tija ni kuwekeza katika ushirikiano wa uchumi wa viwanda.

Tayari serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais Magufuli imeweka kipaumbele cha kuubadili muundo wa uchumi kutoka unaotegemea kilimo kuwa wa viwanda ili taifa liweze kuwa lenye uchumi wa kati.

Rais Magufuli akasema ili kuufikia uchumi wa viwanda kwa mataifa yaliyo wanachama wa SADC, ipo haja ya kuweka kipaumbele kwenye utumiaji wa teknolojia ya viwanda ndani ya mipaka ya jumuiya yenye idadi ya watu wanaokadiriwa kuwa milioni 350.

Hata hivyo, Rais Magufuli anaingia katika uongozi huo akitambua kwamba sekta ya viwanda imeanza kuleta mafanikio katika ukanda wa SADC kwa kuhusisha zaidi ongezeko la viwanda, akitoa mfano kwamba Tanzania imeanzisha viwanda takribani 4000 kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

**VIKWAZO**

Kuwapo kwa vikwazo vya biashara na visivyokuwa vya kibiashara kumetajwa mara kadhaa kuwa miongoni mwa sababu zinazokwamisha ama kufifisha ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi wanachama wa SADC.

Rais Magufuli anasema miongoni mwa mambo yanayopaswa kufanywa ili kufanikisha azma ya ukanda wa SADC uweze kujenga uchumi wa viwanda ni pamoja na kuondoa vikwazo vya kibiashara katika nchi za jumuiya hiyo.

Amezitaka nchi wanachama wa SADC kushughulikia vikwazo vinavyochelewesha maendeleo ya viwanda kwenye ukanda huo, akisema vipo vikwazo visivyo na maana ikiwemo utitiri wa taasisi za udhibiti, kodi, tozo, urasimu wa taratibu za uwekezaji na vikwazo vya mipakani.

Rais Magufuli anasema uchumi wa viwanda hauwezi kuepukika ikiwa nchi wanachama wa SADC zinataka kuufikia ukombozi na kukuza uchumi wa nchi wanachama na bara la Afrika kwa ujumla.

**MAUZO NA BIASHARA**

Akiwa Mwenyekiti wa SADC, Rais Magufuli anatarajiwa kukutana na changamoto inayohusu ongezeko la mauzo ya bidhaa nje ya Afrika ambamo SADC imo ndani yake.

Lakini katika hotuba yake ya hivi karibuni, Rais Magufuli anasema ukuzaji wa teknolojia ya viwanda na matumizi ya malighafi unapaswa kufanyika katika nchi wanachama wa SADC ili kuzalisha bidhaa zenye ubora zitakazouzwa ndani na nje ya Afrika. Rais Magufuli anaamini kuwa pamoja na kujielekeza katika soko la nje ya Afrika, nchi za SADC zinapaswa kuimarisha biashara na mauzo ya bidhaa na malighafi miongoni mwao, hali itakayochochea kukuza mitaji na kuendeleza viwanda vyao.

**UKOSEFU WA AJIRA**

Suala la ukosefu wa ajira ni kero inayozungumzwa katika nchi wanachama wa SADC, kiasi kwamba baadhi yao, wananchi wake walifikia hatua ya kuwafukuza wafanyabiashara wasiokuwa raia wa mataifa hayo.

Lengo la kuwafukuza wasiokuwa raia hao kama ilivyotokea kwa nchi kama Malawi na Afrika Kusini, ilikuwa ni kulinda ajira na soko la ndani.

Mtazamo wa Rais Magufuli kuhusu nchi za SADC kuendeleza ubunifu wa watu na kuhamasisha matumizi ya teknolojia rahisi katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji inaweza kuwa kichocheo cha kukabiliana na changamoto hiyo.

Rais Magufuli anasema nchi za SADC zina vijana wengi wenye vipaji vikubwa katika sayansi na teknolojia visivyotumika vizuri kwenye nchi hizo.

"Badala ya kutumia sayansi na teknolojia hii, tunakimbilia kwenye mataifa mbalimbali na kununua teknolojia kwa gharama kubwa, wakati mwingine isiyosawili na mazingira yetu," Rais Magufuli amekaririwa akisema.

**MKAKATI WA VIWANDA**

Inawezekana, uzoefu alioupata Rais Magufuli katika utekelezaji wa ujenzi wa viwanda, mafanikio na changamoto katika Tanzania, vinaweza kumsaidia katika utekelezaji wa mkakati wa viwanda wa SADC.

Aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa wizara mbalimbali hapa nchini, Uledi Mussa anasema, mkakati wa maendeleo ya viwanda wa SADC unafanana kwa kiwango kikubwa na ule wa Tanzania, akigusia pia miundombinu, hivyo kuimarisha maendeleo na kukuza uchumi na ustawi wa wananchi.

Tanzania ina kumbukumbu ya kushiriki katika harakati za kutafuta ukombozi na uhuru kwa mataifa mengi yaliyo wanachama wa SADC, wakati huo ikiongozwa na Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Mkuu wa Operesheni na Mafunzo, Brigedi ya Magharibi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Kanali Wilbert Ibuge, amekaririwa akisema Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi za mwanzo barani Afrika zilizotoa mchango mkubwa na kuratibu kuanzishwa kwa mtengamano wa SADC.

Mbali na SADC, barani Afrika kuna jumuiya nyinginezo za utengamano kama Jumuiya ya Uchumi kwa Nchi za Magharibi mwa Afrika (ECOWAS), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Soko la Pamoja Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA).

**UMASKINI**

Pamoja na azma ya nchi moja moja na jumuiya nzima ya SADC kujielekeza katika uchumi wa viwanda, ukweli unabaki kuwa sehemu kubwa ya raia wake wanakabakiliwa na umaskini.

Lakini katika miaka ya karibuni, SADC imerekodi mafanikio kadhaa ya kufikia malengo yake, lakini ikikabiliwa na changamoto zinazoonekana 'kuyafunika' mafanikio husika.

Miongoni mwa changamoto hizo uwapo wa mipango mingi inayowekwa kama njia ya kufikia malengo ya kiuchumi.

Pia ipo changamoto ya nchi wanachama kuwa na uanachama katika jumuiya nyingine na uwapo wa malengo mengi yenye utekelezaji duni.

Hali hiyo inawiana na ripoti ya mbobezi wa masuala ya ukanda huo, Pete Hancock anaposema, imejiwekea malengo mengi lakini utekelezaji umekuwa duni na hivyo kuzidi kupanua wigo wa tofauti kati ya malengo na utekelezaji.

Pia kuna changamoto inayohusu wanachama wanaotofautiana kwa asili ya ukanda wanapotoka, mchanganyiko wa asili ya uchumi unaosababisha tofauti ya mazingira na ukuaji uchumi usiolingana kwa nchi wanachama.

Miongoni mwa maeneo yanayotajwa kuzorota ni utekelezaji wa itifaki ya biashara iliyosaini mwaka 2000 na nchi wanachama 11 kati ya 15 waliokuwapo wakati huo.

Pia ukanda huo ulipanga kuanzisha soko la pamoja ifikapo mwaka 2012 na fedha moja ifikapo 2016, lakini yote mawili hayajafikiwa.

Kwa kutambua udhaifu huo, SADC iliahirisha ukomo wa kufikia malengo hayo na kutoa mwanya wa kufanya utafiti zaidi kuhusu athari za utengamano wa kiuchumi kwa nchi wanachama.

**MAFANIKIO**

Pamoja na changamoto zake, SADC imefikia mafanikio kadhaa ikiwamo uthibitisho kuwa utengamano na ushirikiano wa kikanda ni jambo linalowezekana na lenye manufaa.

Kupitia msaada wa SADC, miradi mbalimbali ya miundombinu imetekelezwa kwa sekta za barabara, reli, bandari ikiwa ni njia ya kuboresha mawasiliano, usafirishaji na uchukuzi katika ukanda huo.

Yapo mafanikio na changamoto nyingi kwa SADC na ambazo hazitoshi kuwekwa kwenye makala haya, lakini jambo la msingi ni kuiunga mkono jumuiya hiyo hasa wakati huu ambao Tanzania inachukua uenyekiti, ili ile azma ya awali ya uundwaji wake iendelee kutimizwa katika awamu hii, kuyaendeleza mafanikio na kuzikabili changamoto zilizopo.

NIPASHE inamtakia kila la heri Rais Magufuli katika uongozi wake wa SADC, ili aweze kuivusha salama katika kipindi cha mwaka mmoja kwa kuleta mageuzi yenye kufikia malengo ya jumuiya hiyo.

***Mwandishi wa makala haya anapatikana kwa simu namba +255 754 691540 ama barua pepe: mgeta2000@yahoo.com.***

UCHAMBUZI

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-9

Inatoka Uk. 13

serikali ya Tanganyika

Nguvu kubwa ya Mwalimu Nyerere katika kupinga muundo wa serikali tatu ilidhihirika katika jitihada zake za kupinga Azimio la Bunge la kutaka serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano. Madai hayo yaliibuliwa wakati Mwalimu Nyerere alipokuwa tayari amekwishakustaafu Uenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Lakini, bado aliweza kutumia nguvu kubwa na uwezo wake mkubwa aliokuwa nao wa kushawishi watu, katika kupinga azimio hilo la Bunge. Alifanya hivyo katika vikao vyake vya faragha na viongozi wakuu wa chama na serikali ngazi ya taifa, alifanya hivyo katika vikao vya Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ambavyo alihudhuria kwa kualikwa, na alifanya hivyo hadharani katika mkutano wake na waandishi wa habari. Kwa sababu hakuwa madarakani, haikuwa rahisi kwake kupata mafanikio. Kitabu chake cha "Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania" kinaeleza kwa kirefu jinsi alivyovunjwa moyo kutokana na Wakuu wa Chama na Serikali kutokuthamini ushauri wake kwao.

Hatimaye, alipochoshwa na usugu wa viongozi hao wa kutokuwa tayari kukubali ushauri wake, Mwalimu Nyerere aliamua kuelekeza mashambulizi yake kwa viongozi hao, yaani, Rais Ali Hassan Mwinyi, Waziri Mkuu John Malechela na Katibu Mkuu wa Chama, Horace Kolimba.

Mwalimu aliandika hivi katika kitabu chake cha 'Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania':

- "Washauri wake (Rais Mwinyi) walipomshauri akubali hoja ya kufufua Tanganyika na kuipatia serikali yake, badala ya kukataa na kumfukuza Waziri Mkuu, Rais wetu alikubali! Alifanya hivyo akijua athari za kufufua Utanganyika, na baada ya yeye mwenyewe kusimama mbele ya wabunge siku chache tu zilizopita na kupinga hoja ya serikali tatu."

Hatimaye, mnamo mwezi Desemba 1994, Rais Mwinyi alimwondoa madarakani Waziri Mkuu John Malechela na kumteua Cleopa Msuya kushika nafasi hiyo; na pia alimwondoa madarakani Katibu Mkuu wa Chama Horace Kolimba na kumteua Lawrence Gama kushika nafasi hiyo.

(iv) Kuhusu Madai ya Tume ya Jaji Kisanga

Mwalimu Nyerere hakupata nafasi ya kupinga pendekezo la serikali tatu ambalo lilitolewa na Tume ya Jaji Kisanga, kwa sababu taarifa ya tume hiyo iliwasilishwa kwa Rais Benjamin Mkapa kwa barua liyoandikwa tarehe 20 Agosti, 1999, wakati ambapo Mwalimu Nyerere alikuwa ameanza kusumbuliwa na maradhi ambayo hatimaye yalimwondoa duniani mwezi Oktoba mwaka huohuo.



Moja ya manjonjo ya sherehe za Muungano wa Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

"Hatukutunga mfumo huu kama wapumbavu. Tulitazama hali yetu halisi ilivyokuwa, na tukabuni mfumo uliotufaa zaidi katika hali hiyo" Na "hali halisi" iliyozingatiwa wakati huo ilikuwa ni 'udogo wa Zanzibar na ukubwa wa Tanganyika';

**6.4 Majadiliano katika Bunge Maalum la Katiba**

Majadiliano yalivyokuwa katika Bunge Maalum la Katiba yaliweka wazi sababu zinazotolewa na wale wanaodai muundo wa serikali tatu na sababu zinazotolewa na watetezi wa muundo wa serikali mbili. Kwa hakika, hii ilikuwa chemsha bongo ya aina yake.

Uchambuzi unaonesha kwamba sababu kubwa kwa pande zote mbili ni kuzuia Muungano usivunjike. Kila upande ulikuwa unadai kuwa, muundo wa Muungano wanaoutetea wao, ndio utakaookoa Muungano usivunjike. Hii ni chemsha bongo ya aina yake, kwani siyo rahisi kuelewa kwamba, pande mbili zinazotetea miundo tofauti kabisa, eti zinakuwa na lengo lilelile moja la kuokoa Muungano usivunjike!

Tuliweza kuisikia chemshabongo hii katika mjadala uliokuwa ukiendelea katika Bunge Maalum la Katiba (2013), na jinsi kila upande ulivyokuwa ukitetea hoja zake kwa nguvu kubwa. Hatuna haja ya kurudia kuzitaja hoja zote hizo hapa. Lakini, kwa muhtasari, zilikuwa kama ifuatavyo:

- Watetezi wa serikali mbili walidai kwamba, muundo huu umekuwapo kwa miaka hamsini iliyopita. Matatizo mengi yaliyojitokeza yameweza kutatuliwa, na kero nyingi zimeondolewa. Wanadai kwamba, muundo wa serikali tatu utaleta mzozo mkubwa baina ya Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar katika suala la kuchangia fedha za kuendesha Serikali ya Muungano. Kwa kuwa Zanzibar haina uwezo wa kuchangia kiasi kikubwa, katika muundo wa serikali tatu, Tanganyika nayo itakataa kubeba mzigo huo peke yake, na mzozo huo lazima utasababisha kuvunjika kwa Muungano.



Rais wa pili wa Zanzibar, Aboud Jumbe. **PICHA: MTANDAO**

- Kwa upande wao, wale wanaodai muundo wa serikali tatu walidai kwamba, muundo wa serikali mbili umesababisha kuwapo kwa malalamiko na kero nyingi kwa pande zote mbili za Muungano, kero ambazo zimeshindikana kutatuliwa kwa muda mrefu wa miaka hamsini iliyopita. Wanaendelea kudai kwamba, hatimaye, malalamiko haya yatazaa hasira kali ambazo zitasababisha kuvunjika kwa Muungano. Lakini, katika muundo wa Serikali tatu, kila upande utakuwa na Serikali yake, ambazo zitakuwa zikishauriana katika hali ya usawa juu ya namna ya kutatua matatizo yoyote yatakayokuwa yanajitokeza. Hali hiyo ya usawa ndiyo itakayoimarisha Muungano na kuzuia usivunjike.

Lakini, zaidi ya hayo ni kwamba, kurejeshwa kwa Serikali ya Tanganyika kutaiondoa Tanganyika katika hali ya kuwa 'imevaa koti la Muungano', na kudhihirisha usawa baina ya nchi mbili zilizoungana.

**6.5 Hoja ya kutetea Muundo wa Serikali mbili**

Pamoja na sababu zilizotolewa katika Bunge Maalum la Katiba za kutetea muundo wa Muungano wa serikali mbili, ni vizuri vilevile kujielekeza kwenye sababu halisi zilizowafanya waasisi wa Muungano kuweka muundo huo, kwa kujikumbusha maelezo ya Mwalimu Nyerere kwamba, "Hatukutunga mfumo huu kama wapumbavu. Tulitazama hali yetu halisi ilivyokuwa, na tukabuni mfumo uliotufaa zaidi katika hali hiyo" na "hali halisi" iliyozingatiwa wakati huo ilikuwa ni 'udogo wa Zanzibar na ukubwa wa Tanganyika'; kwa maana idadi ya watu wa kila upande. Swali muhimu hapa ni je, hali hiyo sasa imebadilika? Jibu lake ni dhahiri kabisa kwamba hali hiyo bado haijabadilika. Kwa hiyo, mantiki ya muundo wa serikali mbili bado iko palepale.

**6.5.1 Hofu kwamba, muundo wa serikali tatu utavunja Muungano**

Kwa uchambuzi wangu: Idadi ya serikali siyo kinga dhidi ya Muungano kuvunjika. Idadi yoyote ya serikali, (ziwe ni mbili au ni tatu) siyo kinga ya uhakika ya kuzuia Muungano usivunjike, kwani upo uzoefu wa nchi nyingine zilizowahi kuungana, lakini, muungano wao ukavunjika bila kusababishwa na idadi ya serikali katika Muungano wao, mfano, Misri (Egypt) Syria, Senegali na Gambia.

"Washauri wake (Rais Mwinyi) walipomshauri akubali hoja ya kufufua Tanganyika na kuipatia serikali yake, badala ya kukataa na kumfukuza Waziri Mkuu, Rais wetu alikubali! Alifanya hivyo akijua athari za kufufua Utanganyika, na baada ya yeye mwenyewe kusimama mbele ya Wabunge siku chache tu zilizopita na kupinga hoja ya serikali tatu."

**6.5.2 Mifano ya Miungano iliyovunjika na sababu zake**

Mfano mmoja ni ule wa nchi ya Egypt na Syria. Nchi hizo mbili ziliungana rasmi mwezi Februari 1958 na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Kiarabu, iliyopewa jina la United Arab Republic (U.A.R.). Muungano huo ulidumu kwa kipindi cha miaka minne tu hadi Septemba 1961, ulipovunjika. Sababu ya kuvunjika kwake ni kujitoa kwa Syria kwenye Muungano huo baada ya mapinduzi ya kijeshi yaliyotokea katika nchi hiyo.

Hapa tunaona kwamba, kilichosababisha kuvunjika kwa Muungano huo ni mabadiliko ya Serikali ya Syria, ambapo serikali ya kijeshi iliyotwaa madaraka huko haikuwa na utashi wa kisiasa wa kuendelea kubaki ndani ya Muungano huo.

Mfano mwingine ni nchi ya Senegali na Gambia, zilizoungana katika muundo wa 'Confederation" kuanzia tarahe 1 Februari, 1982, na kujulikana kwa jina la Senegambia. Muungano huo ulivunjika tarehe 30 Septemba, 1989, siyo kwa sababu ya idadi ya Serikali katika muundo wao, bali ni kwa sababu ya utashi wa kisiasa wa nchi hizo na kubaki kwenye Muungano, ulitoweka.

Vilevile, kuna mfano wa "Central African Federation" iliyoundwa na wakoloni ikiunganisha nchi zilizokuwapo wakati huo za Southern Rhodesia, Northern Rhodesia na Nyasaland. Wapigania uhuru wa nchi hizo waliupinga sana muungano huo wa kulazimishwa na wakoloni, na walifanikiwa kuuvunja walipopata uhuru.

Sababu ya kuvunjika kwa Muungano huo ni kutokuwapo kwa utashi wa kisiasa wa viongozi walioshika madaraka katika nchi hizo baada ya uhuru.

**ITAENDELEA WIKI IJAYO**



Kiongozi wa Baraza la Kijeshi Sudan, Jenerali Abdel Fattah al- Burhan. **PICHA: MTANDAO**

## Wanajeshi, waandamanaji Sudan waafiki kutekeleza makubaliano

NAIBU Waziri wa Masuala ya Kisiasa wa Marekani, David Hale, amesema majenerali wa kijeshi na viongozi wa waandamanaji nchini Sudan wameahidi kuingia katika kipindi cha mpito kurejesha utawala wa kiraia.

Naibu Waziri wa Masuala ya Kisiasa nchini Marekani, David Hale, anasema kuwa majenerali wa kijeshi wanaoongoza nchini Sudan pamoja na viongozi wa waandamanaji wametoa ahadi thabiti za kuingia katika kipindi cha mpito kurejesha mamlaka kwa uongozi wa kiraia.

Hale anasema hayo baada ya kukutana na kiongozi wa baraza la kijeshi; Abdel Fattah al- Burhan, viongozi wa waandamanaji na maofisa wa vyama vya kijamii.

Baraza la kijeshi linaloongoza na viongozi wa vuguvugu la maandamano nchini humo walitia saini maazimio Jumapili iliyopita yanayotoa njia ya kurejeshwa kwa mamlaka kwa uongozi wa kiraia baada ya zaidi ya miezi saba ya maandamano na ghasia.

Akiwahutubia wanahabari wakati wa mkutano jijini Khartoum, alipongeza mkataba huo, ulioongozwa na Ethiopia na Muungano wa Afrika na kuutaja kuwa wakihistoria.

**DW**

UCHAMBUZI

# BETTY BIGOMBE; Mwanamke aliyemshawishi Kony kukutana na Museveni Uganda

BETTY Bigombe alikulia Kaskazini mwa Uganda mwishoni mwa miaka ya 1950 na alikuwa akitembea maili nne kila siku kwenda shuleni.

Alijua kuwa kupata elimu ndio njia pekee itakayobadilisha maisha yake binafsi na ya jamii nzima kwa ujumla.

Miaka 30 baadaye "jukumu" lake lilikuwa la kuamua hatima ya siku zijazo za eneo hilo, kupitia jaribio la kushauriana na mbabe hatari wa kivita Joseph Kony, kiongozi wa kundi la waasi wa Lord's Resistance Army (LRA).

Betty alikuwa mtoto wa nane kati ya watoto 11 na alikulia katika jamii yenye utamaduni ambao unaendelea kushuhudiwa hadi leo.

"Bila elimu, pengine huenda nisingekuwa hapa…huenda saa hii ningekuwa na watoto 20 nikiishi vijijini, huku nikifanya kazi ya malezi na zingine ngumu," anasema na kuongeza:

"Kazi kama vile kukuza chakula cha familia kwa kulima, kupalilia na kuvuna na muda huo wote pengine nikiwa nimebeba mtoto mgongoni, huku mwingine akitambaa…pengine ningelikuwa mmoja wa wake wenza."

Familia yake ilipata msaada wa kifedha kutoka katika kanisa, wakati alipokuwa akiendelea na masomo yake.

Nafasi hiyo ilimsaidia kupata ufadhili wa elimu uliomwezesha kujiunga na Chuo Kikuu cha Harvard.

Mapema miaka ya 1980, alirejea nyumbani akiwa ameolewa na tayari akiwa amepata watoto wawili.

Taifa lake lilikuwa limetumbukia kwenye vita ambapo vikosi vya Rais Milton Obote vilikuwa vikikabiliana na vuguvugu lililokuwa likiongozwa na Yoweri Museveni.

"Wakati huo, nilikuwa nikiwaficha baadhi ya watu waliokuwa wakimuunga mkono Museveni. Nilifanya kazi na mwanamke mmoja raia wa Ujerumani aliyekuwa akihudumu katika Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia wakimbizi (UNHCR)," anasema na kuongeza:

"Na tulisaidia kuwapeleka watu waliokuwa hatarini nchini Kenya… ukiwa na bendera ya UN, ni rahisi… tuliweza kupita vizuizi vya barabarani na kuwafikisha mahali salama, hali iliyowafanya watu kupigania haki zao."

Mwaka 1986, Museveni alikuwa rais, wadhifa anaoshikilia hadi wa leo. Alimzawadia Bigombe kwa kumfanya waziri wa serikali.

"Nilipata usumbufu sana nilipoteuliwa katika wadhifa wa uwaziri kwa sababu mawaziri wengine walikuwa wanaume. Kile walichoniagiza kufanya ni kusoma makaratasi… kwa hiyo nilimfahamisha rais kuwa nataka kujiuzulu kwa sababu sikuona chochote cha msingi ambacho ningelifanya, isipokuwa kusoma vitabu wakati nilitaka kufanya kazi," anasema.

Anabainisha kwamba Rais alishangaa sana kusikia kuwa alitaka kujiuzulu kwa kuwa mawaziri wa Afrika hawajiuzulu, hususani wanawake.

Kwa hiyo Betty alikuja na pendekezo la kukutana na waasi kaskazini mwa nchi, baada ya mapigano kuzuka ili kufahamu walichokuwa wakipigania na mahali walipoweka silaha zao.

Rais Museveni alikubaliana na pendekezo hilo, lakini akamwomba Betty kuwashawishi waasi waache mapigano.

Ndugu jamaa na marafiki zake walihofia mpango huo ulikuwa hatari kwa maisha yake.

"Watu wengi waliniambia niachane na mpango huo, 'unataka ufariki' marafiki waliniambia, "Hiyo si kazi ya wanawake, kwanini amekupatia jukumu hilo wakati hujawahi kuifanya," anasema.

Bila shaka ni wazi kuwa hakuna mtu aliyekuwa jasiri wa kutosha kuzungumza na Joseph Kony, kiongozi wa kundi hatari la LRA.

WATUMA UJUMBE

Waasi wa LRA walimtumia Betty barua wakisema Rais Museveni, amewatukana kwa kumtuma mwanamke kujadiliana nao.

Walitishia kumuua, lakini hakutishika na alijitolea kuhakikisha mapigano yanakomeshwa.

Baadaye walimtuma mtu aliyetekwa na kundi la Kony kuwasilisha barua ya pili ana kwa ana.

"Mtu huyo alijitokeza na sijui aliponea vipi kifo… hakuwa na chanjo ya ukambi, alikuwa amekatwa sehemu ya mdomo na viungo vyake na alikuwa ameloa damu…barua inayosemekana imetumwa kwangu ilikuwa imejaa damu, kwa kweli hata sikuweza kuigusa," anasema.

Bila uoga, Betty aliamua kumwandikia barua Kony. alimtaja kama "mwanangu" na kutumia njia za kidini kuwasiliana naye na kuomba wakutane.

Hatimaye Kony alikubali kukutana naye. Alihofia huenda akaamua kumtesa na kumuua badala ya kukubali atumiwe kama chambo cha kumkamata.

Kwa mara ya kwanza walikutana ndani ya kichaka kikubwa cha kuogofya.

"Alikuwa chini ya ulinzi mkali, muziki wa kidini ulikuwa ukicheza, kulikuwa na wanaume waliovalia nguo za watawa na walikuwa wamejihami kwa bunduki," anasema na kuongeza:

" Walikuwa wakiimba muziki wa kidini, [unaosema] kwamba ushetani unakaribia kuwatoka. Mandhari hayo yalikuwa ya kushangaza. Alikuwa amevalia sare za kijeshi, tayari kuniogofya."

Miezi 18 baada ya wao kukutana ana kwa ana mara kadhaa, Kony alianza kumuita Betty "Mummy Bigombe."

Na hatimaye alikubali kutoka mwituni kufanya mazungumzo ya amani na Rais Museveni.

Betty alienda kukutana na rais ili wakubaliane masharti yatakayoongoza mazungumzo hayo ya amani.



Betty Bigombe akiwa na mwakilishi wa LRA Brigedia Sam Kolo (kulia). **PICHA: MTANDAO**

Badala ya kufanya hivyo, Rais Museveni alimtishia Kony hadharani na kutangaza katika mkutano wa hadhara kuwa ajitokeze mara moja la sivyo akabiliwe vikali na vikosi vya serikali.

Kony na vikosi vyake walijibu kwa kutekeleza mashambulizi mabaya katika kituo kimoja karibu na mpaka wa Uganda na Sudan, ambapo watu 300 waliuawa kinyama. Betty alijiuzulu jukumu lake na kuelekea Marekani.

"Nilisikitika sana, nikalia kwa machungu ndani ya ndege…sikuamini tulivyoshindwa kufikia amani… lakini yote haikuwa kwa ajili yangu, nilikuwa nawahurumia watu waliokuwa wakiteseka bila sababu," anasema.

Alirejea tena kwa masomo Chuo Kikuu cha Harvard na baadaye kuajiriwa na Benki ya Dunia (WB) mjini Washington.

Asubuhi moja mwaka 2004, alifungulia runinga kutazama yanayojiri lakini ghafla alikumbana na taarifa iliyobadilisha kila kitu.

Kulikuwa na taarifa katika kituo cha habari cha CNN, kwamba waasi wa Lord's Resistance Army walivamia kambi moja ya wakimbizi na kuua zaidi ya watu 300.

"Na baada ya hapo niliona picha yangu ikiandamana na maandishi… mtu pekee aliyekaribia kukomesha mapigano… mtu pekee aliyekutana na kiongozi wa waasi. Ujumbe huo nilihisi ni mwito kwangu," anasema.

Betty alirejea Uganda na kujaribu kupanga tena mkutano baina yake na kiongozi wa waasi wa LRA, Kony.

Hata hivyo, alihofia hatua ya serikali ya Uganda kufadhili mpango huo utaathiri msimamo wake, kwa hiyo aliamua kutumia pesa zake binafsi.

Alitumia fedha za masomo alizokuwa amemtengea binti yake kulipa bili ya simu yake ya satellite.

Kufikia wakati huo, Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Jinai (ICC), ilikuwa imemfungulia Kony mashtaka ya uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu.

Kazi ya Betty ilikuwa msingi wa mazungumzo ya amani nchini Sudan Kusini mwaka 2006, japo yalivunjika dakika za mwisho, baada ya Kony kukataa kutia saini mkataba wa amani.

Kony na washirika wake katika kundi la Lord's Resistance Army, kutokea wakati huo walipunguza shughuli zao.

Sasa imeripotiwa kuwa afya yake imezorota na jeshi lake limepungua hadi chini ya askari 100.

Leo hii Betty ni Mkurugenzi wa kitengo cha kushughulikia mizozo katika WB.

Anazuru maeneo tofauti duniani kutoa mafunzo kwa wapatanishi na kuwafahamisha alichojifunza alipokutana na waasi wa LRA mwituni.

"Hivi karibuni nilikutana na mmoja wa wapiganaji…wao hunitafuta, inashangaza lakini wanafanya hivyo," anasema na kuongeza:

"Miezi kadhaa iliyopita mmoja wao aliwasiliana nami na kusema, mara hii Kony anataka kukutana na wewe…nikasema, 'naomba uache utani, kama kweli anamaanisha alichosema mwambie anipigie simu, naweza kung'amua sauti yake."

**BBC**

UCHAMBUZI

# Mathew, Mwenyekiti Chadema Lindi anayelimezea mate Jimbo la Mtama

**Na Sabato Kasika**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mkoa wa Lindi, Suleiman Mathew, anasema hajakata tamaa kuwania ubunge wa Jimbo la Mtama mkoani humo.

Mathew ambaye aliwania ubunge wa jimbo hilo katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, anasema figisu alizokutana nazo katika uchaguzi huo haziwezi kumkatisha tamaa, badala yake anajipanga kukabiliana nazo.

Katika mazungumzo yake na mwandishi wa makala haya anasema kwenye kampeni za uchaguzi huo alikuwa hakamatiki lakini alijikuta akifanyiwa figisu na kukoseshwa ubunge na watu wenye mbinu za 'goli la mkono.'

"Lakini nikuhakikishie kuwa sijakata tamaa ya kuwania ubunge wa Jimbo la Mtama kwani wananchi wengi wako nyuma yangu na wananitia moyo, hivyo sitaki kuwaangusha... nitawania ubunge 2020," anasema.

Mwanasiasa huyo anasema, watu waliokuwa wakifuatilia kampeni za mwaka 2015, wanajua kwamba alikuwa hakamatiki, lakini mbinu za goli la mkono zilizotumika zilimfanya akose ubunge.

"Ninaposema goli la mkono ninaamini wanasiasa watakuwa wanalijua, hivyo sioni sababu ya kulitolea ufafanuzi... lakini jambo la msingi ni kwamba hilo na mengine mengi niliyofanyiwa havijanikatisha tamaa," anasema.

Anawataka wapinzani wake jimboni kupunguza maneno na kwamba bado anaendelea kupiga jaramba vitongojini mpaka kieleweke, na kwamba wanaotaka kupambana naye, wakutane mwaka 2020 hapo Mtama.



Suleiman Mathew (aliyebebwa), akiwa katika moja ya mikutano ya siasa jimboni Mtama. **PICHA: SABATO KASIKA**

### ANACHOJIVUNIA

Mathew anasema yeye ni mtu wa kawaida katika jamii, amekuwa akishirikiana na wakazi wa Mtama katika shughuli mbalimbali zikiwamo za kijamii na hata wakati wa shida na raha.

Anasema mazingira hayo yamemfanya awe rafiki wa watu wengi wakubwa kwa wadogo wakiwamo, ambao hadi sasa wanaendelea kumuunga mkono wakimtaka asikate tamaa badala yake agombee ubunge mwaka ujao.

"Sitaki kuwaangusha wana Mtama ambao waliumia wakati ninapigwa goli la mkono kwenye uchaguzi uliopita, kwani bado hawajakata tamaa kunipigania, hivyo nami niko pamoja nao," anasema.

Mathew au 'Messi' kama anavyojulikana jimboni Mtama anadai kwamba anakubalika kwa watu wa kada zote kutokana na umaarufu wa siku nyingi alioupata wakati akichezea timu mbalimbali za soka nchini.

"Kabla na baada ya kuwania ubunge nimekuwa nikitoa vifaa vya michezo ikiwamo mipira na jezi kwa timu mbalimbali na kushiriki shughuli za kijamii, hivyo huwezi kunisema kinyume watu wa Mtama wakakuelewa," anasema.

Anasema nafasi yake ya kutwaa jimbo la Mtama bado ipo hivyo hawezi kukata tamaa, kwa vile mtaji wa wapigakura anao na wanaendelea kumuomba awanie nafasi hiyo mwaka 2020.

### ASICHOSAHAU

Mathew anasema baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, alikumbana na tukio ambalo katika maisha yake hatalisahau la kifungo cha miezi nane jela baada ya kupatikana na hatia ya kufanya mkusanyiko bila ya kibali.

Anasema, Januari 18 mwaka 2017, alihukumiwa kifungo cha miezi nane jela bila faini na mahakama ya wilaya ya Lindi, lakini akatoka kwa dhamana baada ya kukata rufaa kwa hati ya dharura.

"Baadaye mahakama kuu kanda ya Mtwara iliniachia nikiwa tayari nimeshakaa jela kwa siku 40 baada ya kuniona sina kosa. Kwa kweli tukio hili ambalo linatokana na siasa sitalisahau," anasema.

Mwanasiasa huyo, ambaye amewahi kuwa diwani wa Kata ya Vijibweni kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), anaamini kwamba siasa zina changamoto zake zikiwamo hizo za kufungwa jela, ambazo anadai zinamkomaza kiasa.

Anasema, hatua yake ya kujiondoa CCM baada ya kura za maoni kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, ndiyo iliyosababisha uhasama kati yake na baadhi ya wana CCM hadi kufikia kufunguliwa kesi.

> "Kama unakumbuka, baadhi ya wanachama wa CCM waliandamana kupinga ushindi wangu kuporwa kwenye kura za maoni, hivyo kukawa na mgawanyiko miongoni mwao huku wengine wakinichukia," anasema.

"Kama unakumbuka, baadhi ya wanachama wa CCM waliandamana kupinga ushindi wangu kuporwa kwenye kura za maoni, hivyo kukawa na mgawanyiko miongoni mwao huku wengine wakinichukia," anasema.

Mathew anasema wananchi walibeba mabango yenye jumbe mbalimbali wakishinikiza chama kutengua matokeo ya kura maoni wakitaka arejeshewe ushindi wake lakini halikuwezekana.

"Cha ajabu ni kwamba baada ya uchaguzi kumalizika, wale wasionipenda waliibuka na kunifungulia kesi... lakini nirudie kusema kuwa wameniimarisha na tukutane mwaka 2020," anasema.

### ALIKOANZIA

Mwanasiasa huyo alipata umaarufu mkubwa alipokuwa mchezaji soka na hata alipostaafu soka, alianzisha kituo cha kuendeleza michezo cha Tanzania alichokipa jina la Sports Catalyst na pia shule ya sekondari ya Tanzania Sports Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Baadaye aliamua kujitosa kwenye siasa na kuwania udiwani wa Kata ya Vijibweni kupitia CCM katika uchaguzi wa marudio mwaka 2012 na kuchaguliwa kuwa diwani.

"Kata ya Vijibweni ilikuwa chini ya CUF, lakini bahati mbaya diwani wao akafariki dunia ndipo CCM wakaniomba kuwania nafasi hiyo nikaibuka na ushindi kwa kuwabwaga wagombea wa Chadema na CUF," anasema.

Anafafanua kuwa aliongoza kata hiyo hadi alipoacha na kwenda kuwania ubunge nyumbani kwao Mtama, lakini hakufanikiwa kutwaa jimbo kutokana na kile anachodai ni goli la mkono.

"Kama ambavyo nilikuwa nikifanya kazi ya kuhamasiasha vijana kujiajiri kupitia michezo, ndivyo ninavyofanya hata Mtama kwani nina haki ya kufanya hivyo kama mzaliwa wa jimbo hilo," anasema.

Anasema vijana wengi wanajishughulisha na kilimo, na biashara ya nazi na matunda kulingana na msimu, lakini pia wamejiongezea fani nyingine ya kusaidia kujiajiri ambayo ni michezo ukiwamo wa soka.

Anasema, kwa sasa Mtama kuna timu mbalimbali za vijana na kwamba hana budi kusaidia kuibua vipaji ambavyo baadaye vinaweza kuitangaza Mtama na hata taifa kwa ujumla kupitia soka na hata netboli.

# Hiki ndicho mwenyekiti mpya wa SADC anachoingia nacho

Na Gaudensia Mngumi

WIKI hii Tanzania inakuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Uchumi ya Kusini mwa Afrika (SADC), baada ya Rais John Magufuli, kukabidhiwa kijiti cha uongozi na Mwenyekiti anayemaliza muda wake, Rais Hage Geingob wa Namibia.

Kwa wana SADC Mwenyekiti Magufuli, ni kiongozi ambaye huenda akatofautiana na wengine kwa jinsi alivyojipambanua kwenye misimamo ya kiuongozi, akisimamia uzalendo, utaifa, uadilifu, kufanyakazi kwa bidii na kujiamini.

Ndani ya jumuiya ya SADC mambo muhimu yanayoambatana na ujio wa Rais Magufuli kwenye kazi hiyo ni mengi na baadhi ni kama haya:

**MPINZANI WA UMASKINI**

Jambo kubwa linalomtofautisha mwenyekiti mpya pengine na viongozi wengine wa Afrika ni upinzani mkubwa alionao dhidi ya kuitwa maskini.

Pengine ni Rais wa Afrika ambaye anasimama tofauti na simulizi za kimazoea za kudhalilisha ambazo ndizo msingi wa kuizungumzia Afrika na Tanzania, kuwa ni bara na taifa maskini.

Hilo analipinga kwa dhati. Rais Magufuli alipoingia madarakani kuiingoza Tanzania kwa mara ya kwanza 2015, alitamka bayana kuwa nchi anayoiongoza ni tajiri tena ni taifa lenye hadhi ya kufadhili wengine wanaohitaji misaada na kushikwa mkono ili waendelee.

Ni kiongozi asiyeamini kwenye fedha za misaada ili kujiletea maendeleo, kwa vile anaona fedha nyingi ndani ya rasilimali zilizomo nchini na wala si nje ya mipaka.

Kwa imani hiyo hafungamani sana na kuombaomba misaada kwa kuzitembelea kaya za matajiri wanaoishi huko Washington, London, Paris, Tokyo na hata Beijing kunakoelezwa kuwa ni kimbilio la viongozi wa Afrika.

Rais Magufuli anapochukua uongozi wa SADC ni fursa kwa wakuu wenzake kujifunza kuwa walichonacho ni utajiri mkubwa na Ukanda wa Kusini mwa Afrika, ndilo eneo linaloweza kuwa namba moja kwa utajiri duniani.

Ni fursa kwa viongozi hao kujinasibu kuwa si maskini tena kwani wana maliasili nyingi.

Hizi ni pamoja na maporomoko ya Victoria yaliyoko Zambia na Zimbabwe, Mto Inga ulioko Congo ambao sasa unatumiwa kuzalisha umeme wa Afrika nzima kwenye mradi wa Pan Africa Power Project.

SADC ni eneo tajiri lenye shaba, dhahabu, misitu, tena kuna mabwawa makubwa ya umeme kama Stiegler's Gorge Tanzania na la Cahora Bassa nchini Msumbiji yote yenye uwezo wa kuzalisha megawati za umeme zaidi ya 2,000.

**ULINZI WA MALIASILI**

Mwenyekiti mpya anaamini kwenye ulinzi wa mali za taifa. Ni 'championi' wa ulinzi wa rasilimali zote za taifa ili zitumike kwa maendeleo ya nchi.

Kwa viongozi wa SADC ni vyema wakatembelea machimbo ya Tanzanite huko Mererani na kuona kile mwenyekiti wao alichofanya kudhibiti wizi, ufisadi na ulaji wa madini pekee duniani yanayopatikana Tanzania.

Ameweka ukuta madhubuti ambao kwa waliokuwa mafisadi wa madini hayo wakiwamo baadhi ya mataifa yaliyojenga vituo vya kukata, kuchonga na kuuza Tanzanite duniani na kujidai kuwa ni mali yao leo hawana lao.

**UTHUBUTU/KUJITEGEMEA**

Mwenyekiti mpya anaongozwa na roho ya uthubutu. Ni wazi kuwa mara kadhaa Watanzania wamemsikia Rais akisisitiza kuwa hakuna taifa lolote lililoendelea kwa mkono wa wageni.

Ni lazima maendeleo yatoke ndani ya nchi yenyewe kwa kuthubutu, kujituma na kufanya kila jambo kwa bidii.

Rais anaongozwa na misimamo ya kujiamini kuwa 'anaweza, ana nguvu (I am strong) na lazima afanikiwe'.

Ni nguvu mpya anayoingia nayo SADC katika kutekeleza majukumu yake.

Pengine ni wakati muafaka kwa viongozi wengine kuungana na mwenyekiti wao kuyaambia mataifa na raia wao kuwa wana nguvu, wanaweza na wana kila sababu ya kujiletea maendeleo kwa nguvu zao wenyewe.

**VIWANDA**

Ari ya Mwenyekiti wa SADC anayeingia madarakani ni kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Mara nyingi anasisitiza kuwa kila kinachozalishwa Tanzania kiongezewe thamani si kukiuza kama malighafi.

Rais anapokwenda kuiongoza SADC anaingia kwenye uenyekiti na msimamo kuwa ni lazima ukanda huu wa Afrika ujitegemee kiviwanda na usiendelee kuwa kituo cha kuuza malighafi ng'ambo.

Tena uachane na kupokea bidhaa za kisasa zilizozalishwa kwa malighafi walizouza. Na mbaya zaidia wakiuziwa bidhaa na huduma hizo kwa bei ghali.



Mwenyekiti mpya wa SADC, Rais John Magufuli wa Tanzania (kushoto), akiwa na Mwenyekiti wa SADC anayemaliza muda wake, Rais Hage Geingob wa Namibia. **PICHA: MTANDAO**

> Rais Magufuli anapochukua uongozi wa SADC ni fursa kwa wakuu wenzake kujifunza kuwa walichonacho ni utajiri mkubwa na Ukanda wa Kusini mwa Afrika, ndilo eneo linaloweza kuwa namba moja kwa utajiri duniani.

**KUHOJI MIKATABA**

Ujasiri mwingine alionao mwenyekiti ajaye wa SADC ni msimamo mkali wa kupinga unyonyaji na dhuluma, akihoji mikataba kandamizi pamoja na uwekezaji wa kinyonyaji.

Kwa mfano Rais Magufuli, anasimamia mikataba inayolinda maslahi ya haki sawa kwa wote, ndiyo maana alihoji uhalali wa kusafirisha madini ya aina mbalimbali kwa kile kinachoelezwa kuwa ni mchanga wa dhahabu.

Anasimamia ukweli na kuepusha udanganyifu wa kiuwekezaji unaoumiza wananchi kupitia mikataba ambayo inaumiza zaidi Afrika kuliko wageni.

**UCHUMI WA KISASA**

Rais Magufuli ni kiongozi anayetaka vitu vya kisasa kwa maendeleo ya uchumi si kwa Tanzania pekee bali pia SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Anajenga reli ya kisasa (SGR), itakuwa ni muhimili wa kusafirisha watu na shehena katika ukanda huu.

Treni za SGR zitafanya safari kwenye eneo hili hadi Lusaka kupitia reli ya Tazara iliyoboreshwa.

Kupitia Lusaka ni wazi kuwa Tanzania itaunganishwa na Harare, huku usafirishaji wa shehena na watu ukiendelea hadi DRC-Congo na sehemu nyingine za Rwanda na Burundi.

Viongozi wa SADC, hiyo ni fursa ya kuunga mkono juhudi za kimkakati za usafirishaji kwa kuboresha miundombinu ya mataifa yao ili kwenda na kasi ya kuwa na uchumi wa kisasa unaounganishwa na SGR.

**BANDARI KWA PAMOJA**

Rais Magufuli anaingia kuongoza SADC akiwa ameiandaa na kuifanya Bandari ya Dar es Salaam kuwa kiungo muhimu cha kibiashara katika ukanda wa Kusini mwa Afrika.

Angependa kuhakikisha kuwa Afrika Kusini hasa mataifa yasiyo na bahari yanaunganishwa na Tanzania ili kusafirisha mafuta, gesi, chuma, magari na shaba bila kikwazo.

Hivyo wakuu wengine wa SADC wanapotaka kufanikiwa katika sekta ya uchukuzi na usafirishaji ndiyo wakati wa kumuunga mkono Mwenyekiti Magufuli kwa kuitumia kikamilifu bandari ya Dar es Salaam.

Rais Magufuli ana njozi ya kuiunganisha miji ya SADC na Dar es Salaam na kwa nia hiyo, angependa kuwa na usafiri wa anga.

Ameboresha Kampuni ya Ndege ya ATCL na kuhakikisha kuwa watalii na wasafiri kutoka India wanafika kwa wepesi Dar es Salaam na kusambaa maeneo mengine ya ukanda huu wa SADC.

Mwezi uliopita ATCL imeanza kwenda Bombay India na wakati wowote itaanza kwenda China, yote hayo yanafungua milango ya SADC kwenye mataifa mengine duniani.

Ndiyo wakati wa watalii kutoka China na India kuzuru Serengeti lakini kutumia fursa hiyo kwenda Zambia na Zimbabwe kwenye maporomoko ya Victoria, kuona Mto Akosombo, mbuga maarufu za Kalahari na pia kuona uzuri na maajabu ya fukwe za Namibia na mji msafi zaidi barani Afrika wa Windhoek.

Yote hayo yanawezekana kupitia mwenyekiti huyo mpya.





# Wasiokwenda na wenza kliniki wanena

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

BAADHI ya wanawake waliopata ujauzito kabla ya ndoa wameeleza kuwa wanashindwa kupata ushirikiano wa wanaume wanapotakiwa kwenda kliniki kwa vile waliowapa mimba ni waume wa watu.

Walisema wanakosa ushirkiano wa wanaume wanapotakiwa kwenda nao kliniki kwa sababu waliowapa mimba wengine ni wanaume wenye familia zao.

Kinamama hao kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, walisema wanashindwa kupata ushirikiano kutoka kwa wanaume wanapotakiwa kwenda nao kliniki kwa sababu ya kuhofia wenza wao.

Hayo yalisemwa juzi na Diwani wa Viti Maalumu wa Wilaya hiyo, Lucy Ngondo (Chadema), alipokuwa anazungumza na Nipashe kuhusu ushiriki wa wanaume katika kupambana na VVU na Ukimwi, magonjwa mengine na ushauri wa kumlea mtoto unaohusisha kwenda kliniki na wenza wao kwa ajili ya vipimo.

Alisema baadhi ya wanawake waliopewa ujauzito na wanaume wenye wake zao na familia wanashindwa kuambatana na watu ambao si wake zao kliniki wakihofia kuvunja ndoa zao.

Lucy alisema utaratibu wa kuhimizwa wanaume kuambatana kliniki na wenzao wao umekuwa mtihani mgumu licha ya kuwa na faida kwani huchukuliwa vipimo mbalimbali kwa pamoja ili kutambua afya zao na ushauri mwingine wa kitaalamu kuhusu ujauzito.

Alisema kutokana na wanawake hao kupewa ujauzito na waume za watu, huwa wanakosa ushirikiano kwa wanaume wanapoenda kliniki na hivyo kupata wakati mgumu kwenye huduma.

"Tunaomba itungwe sheria ndogo ya kuwabana wanawake wajawazito wasiopima maambukizi ya Virusi vya Ukimwi wanapokuwa wajawazito, kuna wengine wanazaa na waume za watu hivyo na huwa wanafanya kwa kificho hivyo huwa wanapata wakati mgumu kuwashawishi kwenda nao Kiliniki," alisema Ngondo.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Kivuma Msangi alisema kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali wanaendelea kutoa elimu kwa wajawazito pamoja na wenza wao kutambua umuhimu wa kuhudhuria kliniki kwa pamoja.

Aliwashauri wanaume walio ndani ya ndoa kuwa waaminifu ili kuepukana na changamoto za kushirikiana na wanawake wengine na kuwapa ujauzito na kushindwa kwenda nao kliniki.

# Chunya yafungua milango ya dhahabu

**Na Grace Mwakalinga,**
CHUNYA

VIONGOZI wa serikali wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wamewaomba wawekezaji kujitokeza kwenye maeneo mbalimbali ya kiuchumi ikiwamo kilimo na uchimbaji wa dhahabu.

Walisema uwekezaji huo utawanufaisha wananchi kwa kuwapa ajira na kushiriki biashara za aina mbalimbali zinazotokana na rasilimali zilizomo Chunya.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Maryprisca Mahundi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu fursa mbalimbali za kiuchumi zinazopatikana Chunya.

Alisema ili rasilimali za kilimo na madini ziwanufaishe wananchi ni wajibu wa wananchi na wawekezaji kuviboresha na kuviendeleza vitega uchumi vilivyopo ambavyo alisema vitaongeza mapato ya halmashauri pamoja na kuwapatia ajira Wanachunya kwa wakazi.

"Wilaya yetu ina fursa nyingi za uwekezaji ambazo wadau mbalimbali wanaweza wakawekeza, sisi tunawakaribisha ili mradi tu wafuate sheria za nchi, tunapofungua hii hoteli iwe fundisho kwa wengine ambao wanapatamani Chunya kufanya hivi," alisema Mahundi.

Aliongeza kuwa vitega uchumi kama kilimo vinasaidia kuuweka mji katika hali nzuri na ya kupendeza na hivyo akawataka wataalamu wa ardhi na mipango miji wa wilaya kupima maeneo mengi kwa ajili ya watu kujenga vitega uchumi na kuendeleza kilimo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Sophia Kumbuli alisema fursa za uchimbaji madini na kilimo zitaiongezea halmashauri mapato kwa maelezo kuwa watakusanya kodi za ushuru wa mazao na hata kodi ya ardhi.

Aliwatoa hofu wananchi kuhusiana na changamoto ya maji ambapo alisema serikali inajenga mradi mkubwa wa maji katika Kata ya Chalangwa utakaoondoa kadhia hiyo ya muda mrefu kwa wananchi wa Wilaya ya Chunya.




Mkuu wa Huduma za Benki Kidigitali wa Benki ya NBC, Deogratius Mosha (kushoto), akikabidhi cheti kwa mmoja wa mawakala wao Monica Kikoti, baada ya kuhudhuria semina kuhusu elimu ya utoaji wa huduma za kifedha kwa mawakala iliyoandaliwa na benki hiyo jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asasi zaagizwa kujisajili upya

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WIZARA ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeyataka mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyopo Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kujisajili upya kwa mujibu wa Sheria namba 3 ya mwaka 2019, kurahisisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli zinazofanywa na taasisi hizo.

Aidha, yametakiwa yawe yamefanya hivyo ifikapo Agosti 31 mwaka huu, kwa mujibu wa Msemaji wa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Idara ya Maendeleo ya Jamii Erasto Chong'oro.

Alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wanahabari jijini Mbeya na kusema kuwa serikali imetoa miezi miwili kwa ajili ya kusajili mashirika ambayo awali yalisajiliwa kwenye sheria na utaratibu ambao sasa umebadilika.

Alisema kwa sababu wizara imefanya marekebisho ya sheria namba 3 ya mwaka 2019 lazima mashirika hayo yaanze upya usajili.

Alisema kwa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zoezi hilo linafanyika kuanzia Agosti 13 hadi Agosti 17 kwenye ukumbi wa Mkapa ili kutoa fursa kwa wadau wa mashirika kufanya usajili haraka bila malipo.

"Serikali inatambua shughuli za wadau wake wanaohusika na masuala ya kuisaidia jamii kielimu na masuala mengine ikiwa kuzuia ukatili wa kijinsia, na kwamba ni vema asasi hizo kujitokeza mapema, ili kuhuuisha takwimu zao na kuepuka kufungiwa kufanya shughuli zao kwa sababu ya kukosa vigezo," alisema Chong'oro.

Alisisitiza kuwa wizara imeanzisha sheria hiyo mpya ili kuziba mianya ya udanganyifu katika usajili uliokuwa unafanywa na baadhi ya mashirika na kwamba kazi ya usajili ni endelevu na itakuwa na tija kwenye uwajibikaji.



# Mwenge wagomea mradi Mpwapwa

**Na Mwandishi Wetu,** MPWAPWA

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Mzee Mkongea Ally, amegoma kuzindua mradi wa maji wa Mzase wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma, kufuatia kukosekana kwa vielelezo muhimu kutoka maabara ya serikali ikiwamo majibu ya vipimo vya mabomba yaliyotumika.

Aliugomea mradi huo uliogharimu Sh. milioni 432.2 na ujenzi wake kuhusisha kujenga kisima, nyumba ya mashine, tangi la kuhifadhi maji, ofisi ya jumuiya ya watumiaji maji na njia ya umeme.

Kufuatia hali hiyo, kiongozi wa mbio hizo, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, kumpa taarifa za mradi huo, Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(Takukuru) wilayani, ili ajiridhishe na matumizi ya fedha zilizotumiwa.

Hatua hiyo, ilifikiwa juzi na kiongozi huyo baada ya kukagua miundombinu ya mradi huo.

Akizungumza baada ya kukagua, Ally alisema amebaini kuna baadhi ya vitu walivyoomba kwenye mradi huo havipo lakini fedha zinaonyeshwa zilitengwa kwa ajili ya kazi hiyo na zilitumika.

"Kuna baadhi ya vitu vielelezo vyake havipo kama vipimo vya nondo kutoka maabara ya serikali, vipimo vya zege havipo, vya bomba navyo kutoka maabara ya serikali havipo, ubaya wa hapa ni kwamba kazi hazikufanyika lakini kwenye cheti (certificate) fedha zimelipwa," alisema Ally.

Kiongozi huyo alieleza kuwa kutokana na kasoro hizo inaonyesha utaratibu ulikiukwa kwa kufanya malipo hewa hivyo Mwenge wa Uhuru 2019 hauwezi kuzindua mradi huo. "Tunafahamu Mkuu wa Wilaya hili si kosa lako wala la waheshimiwa wabunge, kuna wataalamu ambao wanataaluma ya uhandisi wa kusimamia miradi hii ndiyo wanakiuka utaratibu," alionya.

Aliagiza taarifa ya mradi ikabidhiwe kwa Ofisa Takukuru wa Wilaya ili kila eneo liangaliwe na ajiridhishe na matumizi ya fedha na baada ya wiki mbili taarifa itumwe makao makuu ya Takukuru.

Sambamba na hilo, kiongozi huyo alisema Mwenge uliangalia ubora wa maji kwa mujibu wa vipimo vya maabara na imeonekana kwamba maji ni salama kwa matumizi hivyo wananchi waendelee kuyatumia.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene , alisema kitendo hicho kimekuwa ni fundisho kwao na kitafanya miradi inayotekelezwa kufanywa kwa umakini mkubwa.

Simbachawene ambaye ni Mbunge wa Kibakwe alitumia nafasi hiyo kusisitiza wananchi kutunza vyanzo vya maji kwa kuheshimu sheria iliyopo ya kutofanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 kutoka katika vyanzo vya maji.

Akizungumza baada ya maelekezo hayo, Mkuu wa Wilaya Shekimweri alisema wamepokea taarifa ya ukaguzi na watazingatia maelekezo yaliyotolewa na kiongozi huyo na kuahidi kuyafanyia kazi.

"Tumepokea mapungufu uliyoainisha na kama ulivyoelekeza nimemkabidhi Ofisa wa Takukuru nami namkabidhi hapa ili aanze kazi mara moja na ndani ya wiki mbili taarifa iwasilishwe makao makuu na popote watakapokuwa viongozi wa mbio za Mwenge kitaifa waweze kupewa hatua na maendeleo ya utekelezaji wa maagizo na taarifa hiyo," alisema Shekimweri.

## Jiji latakiwa kutenga maeneo ya makaburi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

BAADHI ya viongozi wa dini mkoani Dodoma wameuomba uongozi wa jiji hilo, kutenga maeneo mapya ya makaburi kwani yaliyopo yanaanza kujaa.

Hayo yalielezwa jana na Mwenyekiti wa Taasisi ya Dodoma General Muslim Association (DGMA), Sheikh Mohamed Thabiti, wakati wa Baraza la Eid El Haji lililofanyika juzi.

Shekhe Thabiti, alisema uongozi wa Jiji la Dodoma unapopima na kutenga maeneo ni vyema kutenga na makaburi, kwa ajili ya kuzikia.

"Kwa sasa maeneo yaliyopo mengi yameanza kujaa tunalazimika kwenda mitaa mingine hali inayoongeza gharama za maziko ,"alisema Thabiti.

Alibainisha kuwa licha ya maeneo hayo kujaa bado wananchi hawajaonyeshwa sehemu nyingine za kuzikia.

Alisema umbali ulipo kwa sasa wa maeneo hayo kuzikia umesababisha gharama za mazishi kuongezeka kutokana na magari yakupeleka miili maeneo hayo kutoza kiasi kikubwa cha fedha. Thabiti aliishukuru serikali na kusema taasisi hiyo imekuwa ikishirikiana na itaendelea kushirikiana na serikali na wadau wengine kuimarisha uhusiano na azaki na wadau wengine bila kujali imani zao katika kutekeleza mikakati ya kuleta maendeleo.




Mwenyekiti wa Taasisi ya Dodoma General Muslim Association (DGMA), Sheikh Mohamed Thabiti (katikati), akizungumza wakati wa Baraza la Eid El Haji, lililofanyika jijini Dodoma juzi jioni. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Jamal Shariff na Katibu, Twalib Twalib. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kupinga rushwa sasa nyumba kwa nyumba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Dodoma, inatarajia kuzindua klabu ya wapinga vitendo vya rushwa, itakayokuwa inatoa elimu kila wakati na popote ndani ya jamii ili kukabiliana na vitendo hivyo.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alipozungumza na gazeti hili kuhusu mikakati waliyojiwekea katika kudhibiti rushwa nchini.

Kibwengo alisema wamejipanga kuzindua klabu hiyo, ambayo itakuwa ikitembelea maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma kwa ajili ya kuwapa elimu wananchi jinsi ya kuepuka kutoa rushwa wanapofuatilia haki zao za msingi popote iwe ndani au nje ya ofisi za serikali.

"Klabu hii pia itaambatana na wananchi kwenye mbio za Mwenge wa Uhuru jijini Dodoma ili kufanikisha lengo la kutoa elimu kwa wananchi," alisema Mkuu wa Takukuru.

Aliongeza kuwa watatumia mikutano ya hadhara ambayo itafanyika katika maeneo mbalimbali kuwafundisha wananchi kwamba rushwa si lazima wala hakuna sababu ya kutoa rushwa.

Alieleza kuwa elimu ni muhimu kutokana na ukweli kwamba wengi hawaelewi na kulazimika kutoa rushwa ili kupata haki zao wakati si lazima wala hakuna sababu.

"Kauli mbiu katika utoaji elimu ni 'Longa Nasi' na kwamba Takukuru inamaanisha wananchi kutoa taarifa pale unapoona kuna viashiria vya ukweli vya rushwa katika eneo lolote ambalo unalifahamu," aliongeza Kibwengo.

Alifafanua kuwa mbio hizo za Mwenge zitasaidia kwa kiasi kubwa wananchi wengi kupata elimu hiyo vijijini na mijini ambako rushwa imekithiri kutokana na wananchi kutokuwa na uelewa.

"Tutakuwa tunatumia vipeperushi kuwapa wakazi wa maeneo mbalimbali ambavyo navyo vitachangia kwa kiasi kikubwa kuielimisha jamii kuhusiana na upingaji rushwa," alisema.

Kibwengo aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa taasisi hiyo ili iwe rahisi kudhibiti vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

"Suala la rushwa si la Takukuru pekee bali ni la watu wote. Kila mmoja anapaswa kuwa ni sehemu ya klabu ya kupinga rushwa. Leo tutapokea Mwenge wa Uhuru Jiji la Dodoma wananchi wanapata elimu ya kutosha," alisema Kibwengo.





# Matokeo ya mitihani yamkera Shein

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kufanya utafiti zaidi kujua chanzo cha baadhi ya shule za Zanzibar kufanya vibaya na kushika nafasi za mwisho katika mitihani ya kitaifa.

Akilihutubia Baraza la Eid el Hajj juzi, lililofanyika Dole Kizimbani, Rais Shein alisema hajaridhika na matokeo mabaya ya baadhi ya shule za Zanzibar ambazo wanafunzi wake walishika nafasi za mwisho kitaifa bila kuwapo kwa sababu za msingi.

Dk. Shein alisema haoni sababu kwa nini wanafunzi wa shule za Zanzibar kushika nafasi za mwisho, huku elimu ikitolewa bure pamoja na kupatikana kwa vifaa vyote vya maabara kwa wanafunzi na michango ya ada kufutwa.

"Nauagiza uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya utafiti wa kina na kuja sababu za msingi zilizofanya wanafunzi wa shule za Zanzibar kufanya vibaya katika mitihani ya kidato cha sita," alisema.

Pia alisema katika kujenga mazingira mazuri kwa wanafunzi wa shule za sekondari kufanya vizuri mitihani ya taifa, serikali imefuta michango ya ada yote ya shule waliyokuwa wakichangishwa wazazi.

Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha kuanzia 2018-2019 Wizara ya Elimu imetenga bajeti ya Sh. bilioni 130 kwa ajili ya ada za wanafunzi kulipia vifaa mbalimbali vikiwamo madaftari na vitabu vya masomo ya sayansi.

Ofisa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali anayeshughulikia elimu kwa wanafunzi wa sekondari, ambaye hakutaka jina lake litajwe, alisema wamelipokea agizo hilo na wanatarajia kukaa kama kamati kulijadili na kulifanyia kazi.

"Tumeisikia hotuba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ambayo ni sawa na agizo la kututaka kufanya utafiti zaidi kujua chanzo cha baadhi ya shule za Zanzibar wanafunzi wake kufanya vibaya mitihani ya taifa," alisema.

Hivi karibuni Baraza la Mitihani la Taifa (Necta) lilitangaza matokeo ya kidato cha sita na katika matokeo hayo, Zanzibar ilitoa shule tano za mwisho zinazoshika mkia.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Mhandisi Hamad Masauni (kushoto), akimwelekeza dereva bodaboda jinsi ya kufunga kofia ngumu, wakati wa utoaji wa elimu kwa madereva na watumiaji wa barabara, zoezi lililofanyika Visiwani Zanzibar jana, kwa lengo la kuwaepusha na ajali zinazoweza kuzuilika. **PICHA: WMNN**

## DC ashadadia unyonyeshaji

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Rajab Ali Rajab, amewaomba wanawake kuzingatia taratibu za unyonyeshaji wa watoto ili kuwawezesha kukua vizuri wakiwa na afya njema.

Rajab alisema hayo Bumbwini Kiongwe Mkoa wa Kaskazini B katika Wiki ya Juma la Unyonyeshaji ambalo lengo lake lilikuwa kuongeza hamasa kwa wanawake kuwanyonyesha watoto kwa kutumia maziwa ya mama.

Alisema wako kinamama hawatumii fursa ya kuwanyonyesha watoto bila ya sababu za msingi, hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kudorora kwa afya ya mtoto.

Hata hivyo alizipongeza baadhi ya taasisi na asasi za kiraia kwa kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu unyonyeshaji wa mtoto na faida zake.

"Mtoto ndiye taifa la kesho kwa hivyo kinamama mnatakiwa kuwanyonyesha kwani maziwa ya mama yamekamilika kwa kuwa na kila aina ya virutubisho," alisema.

Akizungumza katika Wiki ya Unyonyeshaji, Ofisa Miradi wa Taasisi ya Milele Foundation, Eshe Haji Ramadhan, alisema wataelekeza juhudi zao kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na halmashauri za wilaya kuona huduma za afya na elimu inayafikia makundi yote.

"Tumejipanga vizuri kuona elimu kwa kinamama ikiwamo unyonyeshaji kwa kutumia ziwa la mama inawafikia walengwa ili kuona afya ya mtoto inakuwa bora," alisema. Naye Ofisa Lishe kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Said Salum Othman, alisema takwimu zinaonyesha kwamba hali ya unyonyeshaji Zanzibar iko kwa asilimia 30.

"Kiwango cha unyonyeshaji kwa kinamama kwa watoto kinapungua na kipo kwa asilimia 30, huku wakiwamo kinamama wengine hawafikishi miaka miwili ya kuwanyonyesha watoto," alisema.

# Mil. 200/- zatumika kuhudumia wazee

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inatumia Sh. milioni 22 kila mwezi kwa ajili ya pensheni ya jamii ya wazee waliofikia umri wa miaka 70 ikiwa njia mojawapo ya kutambua mchango wao kwa taifa.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, wakati akitoa zawadi ya Sikukuu ya Eid el Hajj katika nyumba za kulelea wazee Sebleni, Unguja na kituo cha kulelea watoto yatima cha SOS kilichoko Mombasa, Zanzibar.

Alisema baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, Serikali ya Rais (hayati) Abeid Amani Karume, ilijenga nyumba za makazi za wazee wasiojiweza wakiwamo wasio na uangalizi wa ndugu na watoto ili kuwahifadhi.

Castico alisema kazi ya kuwatunza wazee inaendelezwa na serikali za awamu mbalimbali na katika serikali ya sasa chini ya Dk. Ali Mohamed Shein, imeanzishwa pensheni jamii.

"Tutaendelea na kazi ya kuwatunza na kuwaenzi wazee wetu ambao wamefanya kazi kubwa katika mchango wa taifa hili. Tunatumia kwa mwezi Sh. milioni 200 kulipa pensheni jamii ya wazee," alisema.

Aidha, alisema kwa upande wa watoto, sheria kali za kuwalinda na kupambana na vitendo vya udhalilishaji zimekuwa zikitungwa ili kuona watoto wanakuwa salama.

Waziri Castico alizitaja sheria zilizopitishwa hivi karibuni ikiwamo ya udhalilishaji na makosa ya jinai, zinatoa adhabu kali kwa watu watakaotiwa hatiani kwa matukio ya ubakaji hadi miaka 30 jela.

"Tumedhamiria kuwalinda watoto wetu dhidi ya matukio ya ukatili wa kijinsia ndiyo maana tumetunga sheria kali kuona wanakuwa salama," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Kituo SOS, Asha Salum, aliwapongeza viongozi wa serikali ya Zanzibar kwa juhudi zao za kuwatembelea watoto na kujua hali zao mara kwa mara.

Alisema watoto hao wamekuwa wakifarijika sana na kujiona kwamba wako katika ulinzi na matunzo salama ya wazazi wao.

"Uongozi wa kijiji cha SOS unafarajika sana kuona viongozi wa serikali wanawatembelea watoto mara kwa mara na kujua matatizo yanayowakabili," alisema.

# Polisi walivyotibua njama za majambazi kuteka basi

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limetibua njama za majambazi kutaka kuliteka basi la kampuni ya Zuberi.

Kutokana na kitendo hicho, jeshi hilo linaendelea kulinda usalama wa wananchi na mali zao kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama likiwamo jeshi la jadi (Sungusungu) katika kipindi chote.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani humo, Richard Abwao, amevihakikishia vyombo vya usafiri ambavyo vinafanya safari zake nyakati za usiku kuelekea katika mikoa ya Kanda ya Ziwa Kigoma, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Geita bila wasiwasi wowote.

Abwao aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe baada ya gazeti hili kupata taarifa kuwa basi la Zuberi linalofanya safari zake Mwanza-Geita na Dar es Salaam lilitekwa na majambazi nyakati za usiku eneo la Lunguya, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama.

Abwao alikiri basi hilo kunusurika kutekwa na majambazi, huku akikanusha askari polisi waliokuwa doria katika maeneo hayo kupambana nao kwa kurushiana risasi.

Alisema askari wa doria walikuwa katika eneo hilo baada ya kupata taarifa za kiintelijensia ndipo majambazi hao walitoroka na kwenda kusikojulikana.

"Ni kweli eneo la barabara ya Lunguya Halmashauri ya Msalala nyakati za usiku majambazi walipanga magogo barabarani kwa kuashiria kuwa na lengo baya la kuteka basi la Zuberi, lakini hawakufanikiwa kutokana na askari waliokuwa doria katika maeneo hayo walifika kabla ya basi kufika eneo la tukio," alisema na kuongeza:

"Hata hivyo, majambazi hayo yalikimbia kwa kuhofia kupambana na askari wangu walioshirikiana na wananchi waliofurika ghafla katika eneo hilo."

Alisema basi hilo namba T640 DLE lilikuwa likiendeshwa na dereva anayejulikana kwa jina moja Abdallah.

Alisema baada ya kuona hali ya kupangwa magogo barabarani askari polisi, sungusungu na wananchi walijipanga imara kukabiliana nao, hali ambayo ilisababisha majambazi hayo kushindwa kutekeleza matukio waliyokuwa wamedhamiria.

Aliwataka wananchi wa mkoa wake kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kupambana na matukio ya kihalifu na mara tu wanapohisi kuna hatari yoyote, watoe haraka taarifa katika vituo vya polisi vilivyo karibu yao.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akimsikiliza Meneja wa Mauzo ya Nje wa Kampuni ya Tanzania Distillers Ltd (TDL), Maleke Hans Mringo, wakati alipotembelea banda la kampuni hiyo, kwenye Maonyesho ya Viwanda ya SADC yaliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GGM yapongezwa maendeleo Geita

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameipongeza Kampuni ya Uchimbaji Dhahabu ya Geita Gold Mining (GGM) kutokana na mchango wake katika maendeleo ya Halmashauri ya Mji wa Geita.

Amesema hatua kubwa za kimaendeleo zilizofikiwa katika halmashauri hiyo zimetokana na mchango mkubwa wa kampuni hiyo kulikoifanya Geita kuwa miongoni mwa miji inayokuwa kwa kasi barani Afrika.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na wananchi wa Jimbo la Geita Mjini ambalo yeye ni mbunge wake, akiwaeleza ahadi mbalimbali alizozitekeleza katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake.

Alisema halmashauri hiyo kwa sasa ina uwezo wa kupanga na kuitekeleza mipango yake kimaendeleo bila kikwazo chochote kutokana na kuwa na nguvu ya kipesa.

Alisema licha ya kasoro kadhaa za GGM, huwezi kuyazungumzia maendeleo ya Geita Mjini pasipo kuitaja kampuni hiyo.

Kanyasu alisema GGM wametoa mchango mkubwa katika ujenzi wa Shule ya Wasichana Nyankumbu ambayo ni moja ya shule zinazofanya vizuri katika mitihani ya kidato cha nne na sita mkoani Geita.

Alisema mbali na hiyo, GGM wametoa mchango mkubwa kupitia fedha za ujirani mwema kwa kujenga madarasa 120, shule za msingi sita na shule za kidato cha tano na sita iliyojengwa katika Kata ya Kasamwa.

Kanyasu pia alisema hadi sasa, halmashauri hiyo imetoa mkopo wenye thamani ya Sh. bilioni 1.7 kwa wanawake, walemavu na vijana (asilimia 10 ya mapato ya halmashauri).

"Tumekopesha ili waweze kujikwamua kiuchumi kwa kujiingiza kwenye biashara mbalimbali," Kanyasu alisema.

Kuhusu sekta ya afya, Kanyasu alisema halmashauri hiyo imefanikiwa kujenga vituo vya afya sita, huku ujenzi wa hospitali ya mkoa ukiendelea mjini humo.

Alisema GGM wametoa mchango mkubwa kwenye ujenzi wa soko la madini ambalo tangu kukamilika kwake na kuanza kufanya kazi, halmashauri hiyo imekuwa na uwezo wa kukusanya Sh. milioni tano kila siku ambazo nazo zimeendelea kuchagiza maendeleo ya halmashauri.

Kuhusu sekta ya maji, Kanyasu alisema halmashauri hiyo imepata Sh. bilioni 100 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji utakaokuwa na uwezo wa kuwahudumia wakazi wote wa Mji wa Geita.

Alisema tayari wataalamu wameanza kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kufanikisha mradi huo na visima sita vimeshachimbwa ili kuwahudumia wananchi wakati wakisubiri kukamilika kwa mradi huo.

Kanyasu alisema halmashauri hiyo pia inaendelea kufanya vizuri katika uimarishaji wa miundombinu ya barabara, michezo na umeme.

# Ujumbe SADC wapongeza teknolojia viwanda Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya wajumbe wa Mkutano wa Wakuu wa Jumuiya ya Maendeleo Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), imeeleza kuridhishwa kwao na teknolojia ya hali ya juu inayotumiwa na viwanda vya Tanzania, hatua inayosaidia uzalishaji bora wa bidhaa zenye kumudu ushindani sokoni. Hayo yamejitokeza wakati wajumbe hao walipofanya ziara kwenye kiwanda cha kutengenezea vifungashio cha Global Packaging (T) Limited kilichopo Kibaha mkoani Pwani, kinachomilikiwa kwa ubia baina ya kampuni ya Wande Printing and Packaging (T) Ltd na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).

Mkurugenzi Mtendaji wa Global Packaging Tanzania Limited, Benno Mwitumba, amesema teknolojia inayotumiwa na kiwanda hicho ni mpya na inatoa bidhaa bora huku idadi ya vifungashio vinavyotengezwa ikiwa ni kubwa ndani ya muda mfupi. "Sisi tumeanza kazi mwaka 2017 na moja kwa moja tukaanza na teknolojia hii mnayoiona sasa ambayo bado ni mpya na ya hali ya juu ambapo kusudio letu lilikuwa ni kutoa bidhaa bora na shehena kubwa kuzalishwa ndani ya muda mfupi," alisema Mwitumba.

Aliongeza: "Waandaaji wa mkutano huu hawajakosea kukiteua kiwanda chetu kwa ajili ya ziara hii na tunataka mfikishe ujumbe kuwa bidhaa zetu ni bora na hivi karibuni tunataka kuingia rasmi kwenye masoko ya nchi za SADC, na tuna hakika wanunuzi watazipenda bidhaa zetu hizi." Mwitumba alishukuru ujumbe wa SADC kutembelea kiwanda hicho, na kusema kuwa uongozi utafanyia kazi ushauri wa wajumbe hao kutaka bidhaa zinazotoka kiwandani hapo kupelekwa pia kwenye masoko ya nchi za SADC ambapo wakulima wanahitaji vifungashio vyenye ubora wa hali ya juu.

"Tumejipanga kutanua kiwanda ili kuongeza uzalishaji kwani mahitaji ya soko la ndani ni makubwa hivyo kupitia ziara hii imetuongezea hamasa katika kufanya utanuzi wa kiwanda tukilenga kutengeneza bidhaa bora zaidi na kuingia rasmi kwenye soko la SADC," alisema Mwitumba. Kuhusu ajira, alisema kiwanda chake kimetengeneza ajira ya moja kwa moja kwa vijana zaidi ya 160, na kwamba baada ya awamu ya tatu ya upanuzi kukamilika, ajira zitaongezeka zaidi ya ilivyo hivi sasa.

Kiongozi wa timu hiyo ya wajumbe wa SADC waliopo nchini, Gastom Kaziri, alisema teknolojia inayotumika na kiwanda hicho ni ya hali ya juu, na kuviasa viwanda vingine nchini kuboresha teknolojia zao, hatua itakayosaidia kuongeza pia ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kuweza kushindana sokoni kikamilifu.

HABARI KIMATAIFA

# Trump awageukia wahamiaji maskini

**WASHINGTON, Marekani**

UONGOZI wa Rais wa Marekani, Donald Trump una mpango wa kuhakikisha unazidisha ugumu kwa wahamiaji maskini ambao wanatakiwa kuongezewa muda wa viza zao ama kupata kadi ya kudumu ya makazi.

Mpango huo unawalenga wahamiaji ambao wanategemea misaada kama ya chakula na makazi kwa zaidi ya mwaka mzima.

Maombi hayo yanaweza kukataliwa ikiwa serikali itaamua kuwa wanaweza kuwa mzigo wa kutegemea misaada katika miaka ijayo.

Maofisa wa Marekani walieleza kuwa mabadiliko hayo yatachangia kujikimu wenyewe na sio kuwa tegemezi.

Utaratibu mpya unaojulikana kama namna ya kujitegemea ulichapishwa katika mpango wa serikali siku ya Jumatatu, na utaanza kufanya kazi oktoba 15, mwaka huu.

Wamesema kuwa wahamiaji ambao tayari ni wakazi wa kudumu wa Marekani wao hawatoathiriwa na mpango huu.

Pia hauwahusu wakimbizi na wanaoomba hifadhi. Lakini wale wanaoomba kuongezewa muda wa viza zao pamoja na kadi ya kijani ama uraia wa Marekani watakumbwa na mabadiliko hayo.

Maofisa hao walieleza kuwa wananchi ambao hawajafikia kiwango cha kipato kinachotakiwa na wanaweza kuegemea kwenye huduma ya bure ya afya ama nyumba, watatakiwa wasiingie nchini Marekani, na wale ambao tayari wapo nchini wanaweza wakakataliwa maombi yao ya kuongeza muda wa kuishi.

Inakadiriwa zaidi ya watu milioni 22 ni wakazi halali wa Marekani lakini hawana uraia na wengi wao wataathiriwa na mpango huu.

Wanaharakati wa haki za kiraia wamesema kuwa mpango huu unalengo la kuwafikia wahamiaji wa kipato cha chini.

Kituo cha Sheria cha Wahamiaji (NILC) kimesema kuwa watamshtaki Rais Trump ili mpango huo usifanye kazi.

Lakini Ikulu ya Marekani imesema kuwa mfumo huo unawasaidia wahamiaji wenye ndugu kuliko wale ambao wanaojitegemea wenyewe.

**BBC**

# Dawa za kupambana na ebola zaonyesha ufanisi

**KINSHASA, Congo**

UGONJWA wa ebola huenda ukadhibitiwa na kutibika baada ya majaribio ya dawa aina mbili zilizokuwa kwenye majaribio kuanza kuonyesha ufanisi katika Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC).

Dawa aina nne zilijaribiwa kwa wagonjwa nchini humo, ambako kuna mlipuko mkubwa wa virusi hivyo.

Dawa aina mbili kati ya nne zimeonekana kufanya kazi vilivyo katika kutibu ugonjwa, utafiti umeeleza.

Dawa hizo sasa zitatumika kutibu wagonjwa wote wa ebola nchini humo, kwa mujibu wa maofisa wa afya wa nchi hiyo.

Taasisi ya Taifa ya Utafiti kuhusu uzio na maradhi ya kuambukiza ya nchini Marekani (NIAID), ambao ilidhamini majaribio hayo, imesema matokeo hayo ni habari njema katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Dawa hizo ziitwazo REGN-EB3 na MAb114, zinafanya kazi ya kuvishambulia virusi vya ebola kwa kuzipa nguvu chembe chembe za kinga za mwili zinazopambana na maradhi.

Mkurugenzi wa NIAID, Dk. Anthony Fauci, alisema ni dawa ambazo kisayansi zimeonyesha kuwa muhimu katika kupunguza vifo vya wagonjwa wa ebola.

Alisema dawa nyingine mbili aina ya ZMapp na Remdesivir, zilishindwa kufanya vizuri kwenye majaribio hayo.

Majaribio yaliyofanywa na taasisi ya utafiti na kuratibiwa na Shirika la Afya Duniani, (WHO), yalianza Novemba mwaka jana.

Tangu wakati huo, dawa aina nne zilijaribiwa kwa wagonjwa 700, huku matokeo ya awali kutoka kwa watu 499 wa kwanza yakifahamika hivi sasa.

Kwa wagonjwa waliopewa dawa aina mbili zilizoonyesha kufanya kazi kwa asilimia 29, waliopewa dawa aina ya REGN-EB3 walipoteza maisha na asilimia 34 waliopewa dawa aina ya mAb114 walipoteza maisha, NIAID ilieleza.

Tofauti na asilimia 49 ya waliopewa dawa ya ZMapp na asilimia 53 waliopewa dawa aina ya Remdesivir walipoteza maisha taasisi hiyo ilieleza.

Mtafiti wa magonjwa ya kuambukiza, Sabue Mulangu, alisema matokeo hayo yanamaanisha kuwa mamlaka za afya zinaweza kuutangazia umma kuwa zaidi ya asilimia 90 ya watu wanaweza kupona ikiwa watapata matibabu mapema.

Akisifu mafanikio ya utafiti, Mkurugenzi wa Mfuko wa Msaada wa masuala ya huduma za kiafya, Jeremy Farrar, alisema bila shaka dawa hizo zinaokoa maisha.

Farrar alisema yanaonyesha kuwa wanasayansi wako mbioni kuufanya ugonjwa wa ebola kuzuilika na kutibika.

"Hatuwezi kutokomeza ugonjwa wa ebola kabisa, lakini tuwe na uwezo wa kuzuia ugonjwa huu kuwa mkubwa katika taifa na ukanda," alisema Farrar.

Hisia kuwa ebola haitibiki, halikadhalika hali ya kutoaminiwa kwa watoa huduma za afya chini DR Congo, kumeathiri juhudi za kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo. Kuna matumaini kuwa ufanisi wa dawa hizo zilizotengenezwa na kampuni ya kimarekani, zitafanya wagonjwa wajihisi kujiamini wanapotafuta huduma mapema", alisema Dk. Fauci.

Alisema njia nzuri ya kumaliza mlipuko huo ni kwa kupata chanjo inayofaa. Chanjo ni aina ya dawa inayoboresha kinga.

Mlipuko wa ugonjwa wa ebola Mashariki mwa DRC ulianza Agosti mwaka jana na ni mkubwa kati ya 10 iliyowahi kuikumba nchi hiyo tangu mwaka 1976, virusi vilipogundulika kwa mara ya kwanza.

Julai, mwaka huu WHO ilitangaza janga la ebola kuwa la dharura duniani.

Ugonjwa huu pia uliathiri watu 28,616, hasa Guinea, Liberia na Sierra Leone. watu 11,310 walipoteza maisha kutokana na mlipuko mkubwa kabisa kuwahi kuripotiwa

Hata hivyo, majaribio ya kupambana na mlipuko wa sasa yamekuwa magumu, kutokana na kuwapo kwa makundi ya wanamgambo na mashaka kuhusu msaada wa tiba kutoka nchi za kigeni.

***BBC***



Wapiganaji wa jeshi lililojitenga linalosaidiwa na Umoja wa Falme za Kiarabu wakiwa mjini Aden baada ya mapambano na vikosi vya serikali. **PICHA: REUTERS**

# DRC yasubiri uamuzi wa mwisho kuunda serikali

**KINSHASA, Congo**

MUDA na wakati wowote kuanzia sasa serikali mpya ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) itatangazwa.

Waziri Mkuu, Sylvester Ilunga Ilunkamba, anatarajia kukabidhi majina ya watu alioteuwa kushiriki katika serikali ijayo kwa Rais Felix Tshisekedi, kabla ya uteuzi rasmi.

Orodha ya watu watakaoteuliwa kwenye nafasi ya mawaziri iko mikononi mwa Waziri Mkuu tangu mwishoni mwa wiki iliyopita.

Orodha hiyo, iliyopendekezwa na muungano wa vyama vya siasa, FCC, unaoongozwa na Joseph Kabila na CACH wa Rais Tshisekedi, itapelekwa kwa Félix Tshisekedi kwa kuisahihisha.

Katika saa 48 zilizopita, Waziri Mkuu Sylvestre Ilunga Ilunkamba aliteuwa majina hayo kwa vigezo vilivyokubaliwa na Rais wa Jamhuri na Mwenyekiti mwenye mamlaka wa FCC, Joseph Kabila.

Majina zaidi ya 100 yataangaliwa na kupitiwa upya, lakini majina 65 pekee ndio yanatakiwa na rais, ambaye ana mamlaka ya kuteua serikali.

"FCC, tuna uhakika tumetoa majina ya watu, wanawake kwa wanaume wenye uwezo wa kufanya kazi. Joseph Kabila amepata wakati wa kupitisha orodha hii na kwa hiyo hakuna mazungumzo yoyote yanayotarajiwa," alisema ofisa mwandamizi wa FCC, ambaye hakutaja jina lake.

Kwa mujibu wa matokeo ya uchaguzi uliofanyika Desemba mwaka jana, Muungano wa CACH utapata nafasi 23, na FCC itapata nafasi 43.

***RFI***

## Mabalozi wa Tanzania nje waja mkutano wa SADC

**Na Beatrice Moses**

MABALOZI 42 wa Tanzania katika nchi mbalimbali wamewasili tayari kushuhudia Rais John Magufuli anavyokabidhiwa Uenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Pia watatembelea miradi kadhaa mikubwa inayotekelezwa nchini.

Msemaji mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, alisema jana kuwa mabalozi hao wamepewa wito rasmi kushiriki mikutano ya SADC inayoendelea nchini.

Alisema leo watatembelea mradi wa ufuaji umeme wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) uliopo Rufiji mkoani Pwani.

"Ni muda tangu wameondoka nchini hivyo watakwenda huko kujionea mradi huo unaotekelezwa na serikali kwa fedha za ndani, ili watumie fursa ya kuwahamasisha wawekezaji.

Dk. Abbasi alisema pia mabalozi waliopo kwenye nchi za SADC nao watakabidhiwa uenyeviti kama ilivyofanywa kwa Prof. Palamagamba Kabudi kupokea uenyekiti wa baraza la mawaziri wa SADC.

Wakati huo huo, Dk. Abbasi alisema, leo Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini atawasili nchini kwa matukio makubwa mawili.

Rais Ramaphosa anakuwa ni Rais wa kwanza kutoka nchi wanachama wa SADC kuwasili kwa ziara ya kitaifa kwa siku tatu.

"Atatembelea kituo cha wapigania uhuru kilichopo Mazimbu mkoani Morogoro, baada ya kumaliza ziara hiyo Agosti 16, ataungana na wakuu wa nchi serikali katika mkutano mkuu utakaofanyika Agosti 17 na 18 mwaka huu," alisema Dk. Abbasi

Alisema Agosti 15 mwaka huu, Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, ataongoza mhadhara wa wazi ambapo ataeleza uzoefu wake juu ya SADC.

"Mhadhara huo ni wa wazi, na kila mmoja anaweza kushiriki ili kupata uzoefu kutoka kwa mzee Mkapa," alisema.

Mkutano huo wa wakuu wa nchi, viongozi wa serikali na wafalme unaanza Agosti 17 hadi 18, mwaka huu.

Dk. Abbasi alisema nchi 16 tayari zimethibitisha kushiriki.

**"Atatembelea kituo cha wapigania uhuru kilichopo Mazimbu mkoani Morogoro, baada ya kumaliza ziara hiyo Agosti 16, ataungana na wakuu wa nchi serikali katika mkutano mkuu utakaofanyika Agosti 17 na 18 mwaka huu," alisema Dk. Abbasi**

# Mgaya ataja sababu vyama vya wafanyakazi sasa kukosa meno

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu mstaafu wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (Tucta), Nicholaus Mgaya, amesema vyama vya kutetea wafanyakazi havina nguvu nchini kwa sababu viongozi walioingia madarakani wapo kwa ajili ya maslahi yao binafsi.

Mgaya ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa Tucta tangu mwaka 2009 hadi alipostaafu mwaka 2016, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu hali ya vyama vya kutetea wafanyakazi nchini, akisema havina meno kama vilivyokuwa zamani.

Alisema udhaifu upo kwa viongozi wengi walioingia katika vyama hivyo kwa dhana ya kujipatia mali badala ya kuwatetea wafanyakazi.

"Vyama vingi vya wafanyakazi havina nguvu, havina nguvu kwa sababu viongozi wengi wameingia si kwa nia ya kuongoza, wameingia wakidhani huko kuna fedha nyingi ambazo hazina wenyewe, kwa hiyo waingia kula fedha," alisema Mgaya na kuongeza:

"We mwenyewe unaona vyama vingi havisikiki kwa sababu viko 'weak' (dhaifu) hata Shirikisho lenyewe la Wafanyakazi (Tucta) liko weak (dhaifu)."

Alisema udhaifu huo unajidhihirisha kutokana na ukimya uliopo, na viongozi kutokuwa tayari kuzungumzia migogoro inayoibuka ndani ya vyama.

Alitolea mfano Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu (CWT), Christopher Banda, kuwa ni Ofisa Elimu, hivyo kwa mujibu wa sheria za ajira nchini, hawezi kuitisha migomo wala kuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya walimu.

Alisema chama hicho kinapaswa kuwa huru, kujiendesha kwa ajili ya kudai maslahi yao, badala ya kusimamiwa na watu ambao ni sehemu ya serikali.

Mgaya alisema baadhi ya wanachama wa CWT walilalamikia suala hilo kwa muda mrefu, jambo ambalo halijafanyiwa kazi. Alisema kutokana na udhaifu uliopo kwenye vyama vya kutetea maslahi ya wafanyakazi, kunasababisha vyama vingine kuanzishwa kikiwamo Chama cha Kutetea Maslahi ya Walimu (Chakamwata).

Alisema hali hiyo imesababisha kuwapo kwa migogoro ndani ya CWT ambayo haijapatiwa ufumbuzi.

Alisema CWT imekuwa ikikata asilimia mbili ya mshahara ya walimu, lakini Chakamwata inakata asilimia moja, jambo ambalo litasababisha walimu kukimbilia huko. Alisema chama hicho kipya kinaweza kuwa mkombozi kwa walimu kama viongozi wake watakuwa imara kusimama kidete kutetea maslahi ya walimu wake.

"Sielewi kama kina uongozi mzuri, kinaweza kuwa kina katiba nzuri, lakini uongozi ukawa dhaifu, wakawa ni waoga, kinaweza kuwa mbadala wa CWT. Kikubwa ni kuwa na viongozi wasiyoogopa na wanaoweza kutumia vizuri sheria za kazi kudai maslahi ya walimu," Mgaya alisema.

Mapema mwezi huu, Mwenyekiti wa Chakamwata, Japhet Joseph, alisema chama hicho kimekuwa kikipigwa vita hadi kuzuiliwa kufanya mkutano mkuu wake wa dharura kwa sababu ya kutetea maslahi ya walimu.

Alidai chama hicho kimekuwa kikikata asilimia moja ya mshahara wa mwalimu fedha ambayo mwalimu anapostaafu hurudishiwa asilimia 50 ya ada alizolipa wakati wa utumishi wake wakati CWT wao wanakata asilimia mbili ambazo huwa hazirudishwi.

Alisema pia kwa mujibu wa katiba yao, mwanachama anapoamua kusitisha hurudishiwa asilimia 50 ya fedha alizochangia katika mfuko huo, tofauti na CWT ambao hawarejeshi fedha kwa mwanachama anayekoma.

Chama hicho kilichoanzishwa mwaka 2015, kina wanachama 12,000 nchi nzima na kati ya hao, 9,000 ni walimu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambao awali walikuwa wanachama wa CWT.

Nipashe ilimtafuta Rais wa CWT, Leah Ulaya, kutaka kufahamu kuhusu yayoendelea ndani ya chama hicho, lakini alidai yupo kikaoni atafutwe baadaye.



Wananchi wakiangalia gari aina ya Canter lililotumbukia kwenye mtaro wa maji ya mvua, baada ya kumshinda dereva katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mabula ashangaa ukosefu wazee wa baraza la ardhi

**Na Munir Shemweta, TABORA**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ametoa siku tatu kabla ya kumaliza ziara yake mkoani Tabora, kukabidhiwa majina ya wazee wa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Tabora kufuatia muda wa wale wa awali kumalizika tangu Desemba, mwaka jana.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na viongozi wa mkoa wa Tabora wakati wa mwanzo wa ziara yake mkoani hapa.

Mabula katika ziara yake, atatembelea wilaya za mkoa wa Tabora kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi na kukagua masijala za ardhi kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa hati za ardhi.

Alisema haiwezekani tangu Desemba, mwaka jana Wazee wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Tabora hawajateuliwa jambo linalosababisha mashauri ya ardhi kushindwa kusikilizwa kwa wakati.

Alisema kuchelewa kuteuliwa wajumbe hao, kunachangia kwa kiasi kikubwa kukwama kusikilizwa mashauri, hivyo kusababisha wananchi kushindwa kutatuliwa matatizo yao. Pia alisema hatua hiyo inasababisha mrundikano wa mashauri mengi na kusababisha Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi wa Wilaya kushindwa kutimiza lengo la kusikiliza mashauri 30 kwa mwezi.

"Haikubaliki kabisa tangu Desemba, mwaka jana Wazee wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tabora hawajateuliwa. Nataka kabla sijamaliza ziara yangu hapa nipatiwe majina ya wajumbe hao niondoke nayo," alisema.

Kuhusu Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Mabula alishangazwa na mkoa mzima kuwa na mabaraza 412 hai kati ya 696 na kufafanua kuwa hali hiyo inachangia wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba Wilaya kuelemewa na mzigo wa mashauri ya ardhi. Aliutaka mkoa kuhuisha mabaraza hayo haraka.

Kwa mujibu wa Mabula, mabaraza ya ardhi ya vijiji ndiyo msingi wa mabaraza ya ardhi na yanasaidia kupunguza mrundikano wa mashauri kwenye wilaya kwa kuwa baadhi ya mashauri yanaweza kumalizwa katika ngazi ya vijiji badala ya kufikishwa katika mabaraza ya wilaya.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, alimweleza Naibu Waziri kuwa pamoja na ofisi yake kutaka kupatiwa majina ya wazee wa Baraza la Ardhi la Wilaya, jitihada hizo zilikwama kwa maelezo kuwa majina ya wateuliwa yapo katika upekuzi.

Hata hivyo, Mwanri alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Komanya Kitwala, kuhakikisha anampatia majina ya wazee hao kabla Naibu Waziri hajamaliza ziara yake mkoani Tabora ili amkabidhi kama alivyoagiza.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MCHANGANYIKO

**WATEJA WA JUMLA,** KIWANDA CHA KUTENGENEZA MIFUKO YA KARATASI KINATAFUTA WATEJA WA ( JUMLA) MIKOA YOTE TANZANIA KATONI YA KG 16 TSH 65,000 KWA MAWASILIANO +255 782 999 061 , +255 712 985 805

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**

Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA VYETI




Hellena Mabula anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo: cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0630-0025 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Nyegina na cheti cha kaidato cha sita chenye index namba S0281-0606 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shulea ya Sekondari Chief Ihunyo.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa:SMT/RB/4781/2018**

115371402

## KUPOTEA KWA VYETI



**Mohamed Yusuph** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo: Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0666-0067** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2009 katika shule ya Sekondari Badri, cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S0101-0573** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012,Shule ya Sekondari Azania na cheti cha Chuo kikuu chenye namba BCOM(A)0004035 kilichotolewa na Chuo kikuu Dar es Salaam mwaka 2015.

**Yeyite atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Control Namba: 991089192921**

115371502

## KUPOTEA KWA CHETI




**Michael Aloyce** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato nne chenye index namba S101/147 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la |Taifa mwaka 1989 katika Shule ya Sekondari Azania.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: WMB/RB/13730/2018**

115370802

## KUPOTEA KWA VYETI



**Saidi Kitambala Saidi** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index **namba S1374/0110** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Kichangachui.

Yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/STA/RB/197753/2019**

115370602

## KUPOTEA KWA CHETI



**Rehema Mohamed Gohage** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2631-0044 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Mukilima.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: MKB/RB/3135/2019**

115372102

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI.

**EMMANUEL ATHONY JIDOLA** MKAZI WA MWASELE MANISPAA YA SHINYANGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA PIKIPIKI AMBAYO ALIINUNUA WORLD VISSION TANZANIA MWAKA 2010 YENYE NAMBA ZA USAJILI T. 183 ACN HONDA XL 125 AMBAYO ILIPOTEA MWEZI WA 3, 2019 MAENEO YA SHINYANGA.

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA EMMANUEL ATHONY JIDOLA KWA SIMU NAMBA 0763077258

**RB NAMBA SHY/RB/ TR/129/ 2019**

215371002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;158/2019**

Ombi la **ERASTO ELECK RITE** kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **AIKA RUBEN URONU**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/09/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 13/08/2019

215370902

## KADI YA TRECTA IMEPOTEA

**JOSEPH S.PANGANI**

anatangaza kupotelewa na kadi ya TRECTA yenye namba za usajili T 909 CRA.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi,

Taarifa ya Polisi:
**MLA/RB/1166/2019**

215371102

**RE: THE LAND ACT NO. 4 OF 1999**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER**
**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFR OF:**
**ATHUMANI MFAUME**

REF: NO. LD135429 OF 26/11/1990
REGISTERED OWNER: ATHUMANI MFAUME
LAND: PLOT NO. 81 BLOCK 'S' TABATA DAR ES SALAAM

**APPLICANT: NEMES TABU MAKEMBE**

TAKE NOTICE that the original letter of OFFER to the land described above is said to be lost and that intend to issue a **REPLACEMENT OF ORIGINAL LETTER OF OFFER** in lieu therefore unless cause to the contrary is shown within thirty days from the date of this publication.

The **ORIGINAL LETTER OF OFFER** if found should be delivered to the office of the ILALA Municipal Director, P.O.BOX 20950 DAR ES SALAAM

**ISSUED BY**
**MUNICIPAL DIRECOR**

215371702

## TANGAZO LA GARI

**SAID MAKUBEL MBARAK** WA ARUSHA ANATANGAZA KUMUUZIA NDUGU DOMINIC MUNGA MATHIAS GARI AINA YA NISSAN YENYE RANGI YA SILVER . IMESAJILIWA KWA NAMBA T 322 AXP, ENGINE NAMBA 990 CHASSES NAMBA K11821642.

KWA MAWASILIANO
**ZAIDI PIGA 0713229510.**

215372002

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI.

**WUZHUO INVESTMENT COMPANY** anatangaza kupotelewa na Kadi ya pikipiki aina ya SANLG yenye namba za usajili MC 848 BKM na Chassis No. LBRSPJBS2G9031397

Taarifa ya Polisi
**KAH/ TR/RB/ 583/2019**

215371902


NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# STERLING

## APATA DILI LA PAUNI MIL. 100

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Mancheser City, Raheem Sterling anatarajia kusaini mkataba binafsi mnono wa pauni milioni 100 ili kuvaa viatu vya AirJordan.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 yupo kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake na kampuni ya Nike.

Lakini gazeti la Telegraph limeripoti kwamba, Raheem atavaa viatu vya kampuni hiyo ya AirJordan kutoka nchini Marekani na kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji atakayelipwa fedha nyingi zaidi.

AirJordan ambayo ilizinduliwa mwaka 1984 kwa ushirikiano na nyota wa zamani wa mpira wa kikapu wa Ligi ya Marekani, NBA, Michael Jordan, imekuwa ikiwavalisha nyota wa mchezo wa magongo.

Sterling pia ana kataba mwingine na kampuni ya Microsoft kwa ajili ya kupromoti Xbox pamoja na EA Sports, ambayo ndio inamiliki 'gemu' za video za shirikisho la soka la Kimataifa, Fifa.

Dili hilo litamfanya Sterling kuvuta mkwanja mrefu na kumweka kwenye orodha ya wanasoka wanaingia fedha ndefu zaidi kutokana na matangazo binafsi na kampuni mbalimbali.

Na yeye atakuwa mchezaji wa kwanza wa klabu ya Man City kuvivaa viatu hivyo katika Ligi Kuu ya England.

# CHELSEA KUMRUDISHA DIMBANI RUDIGER

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea sasa inapanga kumrudisha haraka, Antonio Rudiger tofauti na ilivyopangwa kutoka majeruhi ya goti baada ya kufungwa mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Manchester United.

Beki huyo wa kimataifa wa Ujerumani alifanyiwa upasuaji wa goti mapema mwaka huu na kumfanya kuwa nje ya uwanja katika mechi za mwisho za msimu uliopita.

Mchezaji huyo mwa zamani wa AS Roma ameanza kufanya mazoezi kivyake katika kituo cha mazoezi cha Cobham ili aweze kurudi uwanjani akiwa fiti kwa asilimia 100.

Na sasa kocha, Lampard ameamua kumtupia jicho Rudiger baada ya beki yake kupwaya Jumapili wakichezea kichapo kutoka kwa Man United pale kwenye dimba la Old Trafford.

Kabla ya kuanza kwa msimu huu, Lampard alikutana na Rudiger na kufanya naye mazungumzo binafsi ili kujua maendeleo ya hali yake kabla hajarudi uwanjani.

Bosi huyo wa Blues anataka kuhakikisha beki huyo anarudi uwanjani mapema ili kuweza kuimarisha safu yake ya ulinzi.

Beki Kurt Zouma amekuwa akishutumiwa zaidi baada ya kufungwa na United, kuwa alipwaya.



# ALISSON AIPA PIGO LIVERPOOL

**LONDON, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amethibitisha kwamba, golikipa Alisson atakaa nje ya dimba kwa wiki chache zijazo baada ya kuumia kigimbi.

Kipa huyo wa kimataifa wa Brazil alitolewa nje dakika ya 39 wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Norwich kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu Ijumaa iliyopita.


"Sio nzuri. Ameumia kigimbi ambacho kitamfanya kukaa nje kwa muda kidogo," alisema Klopp akinukuliwa na tovuti ya Klabu hiyo.

"Siwezi kusema kwa sasa ni muda gani atakuwa nje, lakini naamini atakuwa nje ya dimba kwa wiki chache zijazo.

"Nilishawahi kuona mchezaji akikaa wiki sita kwa majeruhi kama haya, lakini sidhani kama anaweza kukaa kwa muda zaidi ya mwezi. Lakini nina uhaika atakaa nje kwa wiki kadhaa."

Alisson nafasi yake ilichukuliwa na Adrian, ambaye amejiunga na klabu hiyo akiwa huru kutoka West Ham na sasa atabeba jukumu la Mbrazil huyo wakati akiwa nje.

Klopp sasa amethibitisha kwamba, klabu itamsaini Andy Lonergan kwa muda mfupi ili kuweza kumsaidia Adrian.



## HABARI MICHEZO




JOSHUA RUIZ

# JOSHUA KURUDIANA NA RUIZ DESEMBA

**LONDON, England**

PAMBANO la masumbwi la marudiano kati ya bondia, Andy Ruiz Jr na Anthony Joshua litafanyika Desemba nchini Saudi Arabia, promota, Eddie Hearn amethibitisha.

Kumekuwa na tetesi kuwa Ruiz Jr hayupo tayari kwa pambano hilo, lakini Hearn amesema kuwa mabondia wote wawili wamesaini mkataba wa mpambano huo Desemba 7, mwaka huu.

Ruiz aliushangaza ulimwengu wa masumbwi kwa kumchakaza Joshua Juni mwaka huu kutawazwa kuwa bingwa wa dunia wa uzito wa juu.

Bingwa huyo hadi sasa hajawaarifu chochote mashabiki wake kupitia mitandao ya kijamii kuhusiana na mpambano huo wa marejeano toka ulipotangazwa siku ya Ijumaa.

Kocha wake, Manny Robles amesema, "Kuna sababu inayomfanya" Ruiz kukaa kimya.

"Mabondia wote wawili wameshatia saini. Vyombo vya usimamizi (wa ndondi) vimeshaarifiwa," amesisitiza Hearn.

Katika mkutano na wanahabari, ambao hata hivyo si Joshua wala Ruiz ambaye alihudhuria, Hearn alitangaza kuwa mpambano huo utafanyika katika uwanja wa wazi katika kitongoji cha Diriyah, nje kidogo ya jiji la Riyadh.

Omar Khalil, ambaye anafanya kazi na serikali ya Saudia katika kuandaa pambano hilo pia ametangaza kuwa wote watakaonunua tiketi za mpambano huo moja kwa moja watakuwa wamepewa viza ya kuingia nchini humo.

Upande wa Ruiz uliweka wazi kuwa usingekubali kucheza pambano la marejeano nchini Uingereza, huku upande wa Joshua ukitaka pambano hilo lichezwe nje ya Marekani.

"Tulipata ofa kutoka Saudi Arabia, Abu Dhabi, Dubai na Qatar," aliongezea Hearn. "Tulitaka kwenda sehemu ambayo wana maono ya mbali na mchezo wa masumbwi. Tulijua Saudia inamaanisha na imewekeza kwenye mchezo huu."

"Inabidi tutambue kuna ulimwengu mwingine nje ya Uwanja wa Cardiff na Madison Square Garden. Tunalazimika kukuza mchezo huu katika maeneo mengine duniani.

Ruiz, alimpoka Joshua mikanda ya IBF, WBA na WBO Juni Mosi baada ya kumuangusha mara nne kabla ya mpambano huo kukatishwa na mwamuzi.

Mkataba unamlazimisha kucheza pambano la marudiano, na awali inadhaniwa kwa ukimya wake labda hajasaini pambano hilo.

Kuna wanaodhani kuwa ukimya wa Ruiz unatokana na kudai kitita kikubwa zaidi ya alichopewa awali.

Pambano hilo linatarajiwa kuingiza fedha nyingi, mpaka sasa inaarifiwa kuwa waandaaji nchini Saudia wametoa dola milioni 40, na bado hapo kuna kitita cha watakaolipia watazamaji kwenye runinga hakijajumuishwa.

Waandaaji nchini Saudia wanasema nchini mwao kuna hamu kubwa ya matukio kama hayo kutokana na uhalisia kuwa 70% ya wananchi milioni 40 ni vijana chini ya miaka 24.

Hata hivyo, makundi ya kutetea haki za binaadamu yanapinga vikali kuandaliwa kwa mapando ya ukubwa wa kiasi hicho nchini humo.

Wanadai kuwa matamasha ya michezo na burudani yanatumika na serikali ya kifalme kuonesha kuwa nchi hiyo imebadilika na kuwa ya kisasa ilhali haki za binaadamu zinaendelea kuvunjwa kila uchao.

# Wachezaji Real Madrid wamvuta Neymar

**MADRID, Hispania**

WACHEZAJI wa Real Madrid wamekuwa wakizungumza na Neymar ili kumshawishi nyota huyo wa Paris Saint-Germain kujiunga nao pale Bernabeu, kwa mujibu wa ESPN FC.

Mkurugenzi wa soka wa PSG, Leonardo amethibitisha kwamba klabu hiyo itamuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kipindi hiki cha majira ya joto na maofisa wa klabu mbili za Madrid na Barcelona wanajaribu kufikia makubaliano.

Wakati huo huo, mashabiki wanaompinga Neymar waliingia uwanjani na mabango wakati mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa wakishinda mabao 3-0 dhidi ya Nimes wikendi iliyopita.

Kurudi Barca ndio jambo linaloonekana kuwa linawezekana kwa Neymar, lakini Madrid nao wameingia kwenye mbio za kutaka kumsajili mchezaji huyo.

Beki wa Barca, Gerard Pique wiki iliyopita alimwambia mchezaji mwenzake huyo wa zamani kuzungumza hadharani kama anataka kurudi pale Camp Nou.

Hata hivyo, Madrid wanaweza wasifikie bei ya kumnunulia mchezaji huyo ya euro milioni 222 ambayo ndiyo bei wanayoitaka PSG na ndio waliyomnunulia miaka miwili iliyopita.

Neymar ni mchezaji ambaye anawaniwa kwa muda mrefu na Rais wa Madrid, Florentino Perez.



## Spurs yapanga kumbakisha Eriksen

**LONDON, England**

KLABU ya Tottenham ipo tayari kuongeza mara mbili zaidi mshahara wa Christian Eriksen ili kumbakisha mchezaji huyo klabuni hapo, gazeti la Daily Mail limeandika.

Lakini taarifa nyingine zinasema kwamba, bado hiyo haitoshi kumshawishi mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark kusaini mkataba mpya baada ya kuainisha wazi kuwa maamuzi yake hayabadilishwi na fedha.

Spurs wanataka kuongeza mkataba wa Eriksen na wapo tayari kumlipa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki ambao ni zaidi ya mara mbili wa ule anaolipwa sasa wa pauni 80,000.

Lakini Eriksen amebainisha kwamba hana mpango wa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo kwa sababu anataka kuichezea klabu kubwa Ulaya.

Klabu za Real Madrid na Juventus zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili mchezaji huyo kipindi hiki cha majira ya joto.

Spurs wanahofia Eriksen ambaye anatajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 100 akaondoka kipindi kijacho cha majira ya joto akiwa huru baada ya mkataba wake kumalizika.

Mwenyekiti wa Totenham, Daniel Levy bado anaweza kumuuza Eriksen kipindi hiki cha majira ya joto kwa sababu dirisha la usajili kwa ligi nyingine Ulaya bado halijafungwa hadi Septemba 2.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AFUNGUKA UPENDO WA ZIDANE

Mara zote alikuwa mwaminifu kwangu, aliniambia Cris furahia na cheza mchezo wako, wewe ndiye...

**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo amemmwagia sifa Zinedine Zidane kwa kumfanya kuwa wa kipekee wakati akiwa na miamba hiyo ya La Liga wakati akimchambua mahusiano yake ya karibu na kocha huyo wa Real Madrid.

Ronaldo aliondoka Madrid kuelekea msimu wa 2018-19, na kujiunga na Juventus kwa dau la euro milioni 112 baada ya kuibebesha ubingwa wa Ulaya mara tatu akiwa chini ya Zidane.

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ('Ballon d'Or'), alifurahia mafanikio makubwa wakati akiwa chini ya Zidane katika kikosi cha Santiago Bernabeu, pia alitwaa ubingwa wa La Liga msimu wa 2016-17.

Ronaldo amemwagia sifa Zidane - ambaye yupo katika kipindi chake cha pili akiiongoza Madrid - wakati akijadili uhusiano wao. "Kujiamini anakohitaji mchezaji hakutoki kwake bali pia hutoka kwa wachezaji wanaomzunguka na kocha," Ronaldo aliiambia DAZN.

"Unahitaji kujisikia kama wewe ni sehemu muhimu ya kundi na Zidane alinifanya kuwa wa kipekee.

"Amenisaidia sana. Tayari nilikuwa na heshima kubwa sana kwake lakini kufanya kazi naye kulinifanya kumpenda zaidi.

"Hiyo ni kwa sababu ya kile anachokipenda kama binadamu, namna anavyozungumza, namna anavyoiongoza timu na namna alivyonitendea.

"Aliniambia, 'Cris, furahia na cheza mchezo wako - wewe ni ndiye pekee unayekwenda kubadili mambo.'

"Mara zote alikuwa mwaminifu kwangu na ndiyo maana nitakuwa na upendo wa kweli kwake."

Ronaldo alifunga mabao 21 Serie A katika msimu wake wa kwanza akiwa na mabingwa wa Italia, Juventus, ambayo ilitwaa ubingwa wa Scudetto kwa mara ya nane mfululizo.

## KWA UFUPI

**NEYMAR AANZA KUNUKIA BARCA**

WAWAKILISHI wa kisheria wa mshambuliaji wa Paris St-Germain na Brazil, Neymar, 27, wamepigwa picha wakiingia ofisi za klabu ya zamani ya mchezaji huyo, Barcelona. ***(Gol TV, via AS)***

**BAYERN YAJITOSA KWA COUTINHO**

Bayern Munich ipo katika mazungumzo na Barcelona kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo Mbrazil Philippe Coutinho, 27, kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu ambao unajumuisha dau la kununua jumla mwishoni mwa msimu. ***(RAC1, via AS)***

**STURRIDGE KUAMUA WIKI HII**

STRAIKA wa zamani wa Liverpool, Daniel Sturridge, 29, atafanya uamuzi mwishoni mwa wiki hii kuhusu mustakabali wake wakati akizingatia ofa 13 kutoka klabu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mkataba utakaomuwezesha kupokea pauni 60,000 kwa wiki kutoka Fenerbahce ya Uturuki. ***(Telegraph)***

**ZAHA AKUBALI YAISHE PALACE**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, 26, amekubali kuweka kando tofauti zake na uongozi wa Crystal Palace, baada ya mchezaji mwenza, Mamadou Sakho kumtaka kujitoa kwa kila kitu katika mkutano na wachezaji. ***(Sun)***

**PERISIC APIMWA AFYA BAYERN**

WINGA wa Inter Milan na Croatia Ivan Perisic, 30, amefanyiwa vipimo vya afya Bayern Munich na anajiandaa kukamilisha uhamisho wake wa mkopo wa muda mrefu wa pauni milioni 4.64, ambao unajumuisha kipengele cha kumnunua kwa pauni milioni 18.6 mwaka ujao. ***(Bild - in German)***

**NEYMAR MBADALA WA POGBA**

REAL Madrid bado inavutiwa kuinasa saini ya Neymar na itahitimisha mchakato wa kumsajili kiungo wa Ufaransa na Manchester United, Paul Pogba, 26, endapo itampata Mbrazil huyo. ***(Sun)***

**BALE ASIKILIZIA ZIDANE ATIMULIWE**

MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale, 30, anajiandaa kuendelea kuvuta muda Real Madrid hadi dirisha jipya la usajili Ligi Kuu China litakapofunguliwa tena Novemba mwaka huu ama kusikilizia kama Zinedine Zidane atatimuliwa. ***(Mail)***

**BECKHAM KUMSAJILI CAVANI**

TIMU ya David Beckham inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, Inter Miami itamsajili straika wa Uruguay, Edinson Cavani, 32, wakati mkataba wake na PSG utakapomalizika Juni 2020. ***(Fox Deportes - in Spanish)***

**LOVREN AWEKWA SOKONI LIVER**

Liverpool itakubali ofa ya pauni milioni 13.9 pamoja na bonasi kwa beki wao wa kulia Mcroatia Dejan Lovren, 30, wakati huu akiivutia AC Milan na Roma. ***(Liverpool Echo)***

**SABABU PEPE KUTUA ARSENAL**

WINGA wa kimataifa wa Ivory Coast, Nicolas Pepe, 24, amejiunga na Arsenal akitokea Lille kwa sababu alitaka kutua klabu ambayo anaweza kuonyesha makubwa, amesema rais wa klabu hiyo ya Ufaransa. ***(Sky Sports)***

**ERIKSEN ATEGWA BURE JUVE**

MABINGWA wa Italia, Juventus wanavutiwa na kuinasa saini ya kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 27, kwa uhamisho huru wakati mkataba wake na Tottenham utakapomalizika mwishoni mwa msimu. ***(Metro)***

**UTD YASHANGAA TETESI POGBA**

Manchester United wameshangazwa na madai kwamba Paul Pogba anaweza kuondoka majira haya ya joto. ***(Mirror)***

# KAKOLANYA ASHUSHA PRESHA YA AUSSEMS KWA MANULA

**Na Mwandishi Wetu**

UWEZO unaoonyeshwa na kipa mpya wa Simba, Beno Kakolanya, umezidi kumshawishi Kocha Mkuu wa mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara, Mbelgiji Patrick Aussems, jambo ambalo limemfanya kueleza anaona changamoto kubwa kwa mlinda mlango namba moja, Aishi Manula.

Manula ambaye hajaichezea Simba tangu aiache kambini Afrika Kusini na kurejea kujiunga na Taifa Stars, kukosekana kwake kumetoa nafasi kwa Kakolanya kuweza kuonyesha ubora wake ambao sasa umemshawishi Aussems.

Mbali na mechi za kirafiki Kakolanya alizosimama langoni wakiwa kambini Afrika Kusini na kufanya vizuri, ameidakia Simba pia katika mechi ya kirafiki dhidi ya Power Dynamos ya Zambia iliyopigwa Uwanja wa Taifa kwenye kilele cha Simba Day na kumalizika kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara kushinda 3-1.

Katika mechi ya kimashindano ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya UD Songo iliyomalizika kwa sare tasa ugenini Beira nchini Msumbiji, pia Kakolanya ndiye aliyesimama langoni na kuonyesha uwezo mkubwa kwa kufuta makosa kadhaa yaliyofanywa na safu ya ulinzi.

Kutokana na kiwango hicho, Aussems amemsifu Kakolanya kwa kufanya vizuri, na kueleza kuwa kwa sasa hana wasiwasi tena kama ilivyokuwa msimu uliopita wakati Manula alipoumia.

"Katika mechi zote alizocheza, amefanya vizuri, hivyo ni matumaini yangu kadiri siku zinavyoenda atakuwa bora zaidi na natarajia atatoa changamoto kubwa kwa Manula," alisema Aussems alipoulizwa kuhusu kiwango cha Kakolanya.



Baadhi ya wachezaji wa zamani wa klabu za Simba na Yanga wakiwa katika picha ya pamoja, kabla ya mchezo wao utakaopigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi. Kutoka kushoto ni Mohamed Hussein 'Mmachinga', Ramadhan Kampira, Dua Said, Edibilly Lunyamila na Thomas Kipese. **MPIGAPICHA WETU**

# Wakongwe Simba, Yanga kukinukisha mkoani Lindi

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa zamani wa vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga wanatarajiwa kumenyana katika mechi inayotarajiwa kuwa kali na ya kusisimua wakati wa kilele cha tamasha la Mtaa kwa Mtaa litakalofanyika Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi Jumamosi wiki hii.

Tamasha hilo la aina yake linatarajiwa kuwakutanisha wakongwe hao wa 'kukinukisha', Jumamosi kabla ya Jumapili kupigwa fainali ya tamasha hilo iliyozishirikisha timu zaidi ya 100.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, mchezaji wa zamani wa Simba, Thomas Kipese, aliwataka mashabiki wa soka hususan vijana kujitokeza kwa wingi siku hiyo ili waweze kupata vitu vizuri kutoka kwa wakongwe hao.

Alisema katika mchezo huo, Yanga lazima wafe kama walivyokufa Songea katika tamasha la Majimaji, na kukiri kuwa kikosi chao kimejipanga vya kutosha kwa ajili ya mchezo huo. "Mimi mnanijua vizuri wadau wa mpira mje kwa wingi sana siku hiyo mpate burudani ya aina yake, iliyoandaliwa na Mashujaa FM iliyopo Lindi, ni nafasi ya kipekee kwa wakazi wa mkoa huo kujionea burudani ya aina yake," alisema.

Kwa upande wake Ramadhan Kampira, ambaye ni mchezaji wa zamani ya Yanga, aliwataka Simba kujiandaa kisaikolojia kwenda kupokea kipigo kwani Yanga iko vizuri na wanamorali ya hali ya juu kwa ajili ya mchezo huo.

Aliwataja baadhi ya wachezaji watakaolitandaza soka siku hiyo kuwa ni yeye mwenyewe, Mohamed Hussein, Edibilly Lunyamila, Bakari Malima, Said Maulid na wengine kibao.

Naye Maximilian Luhanga, ambaye ni Mkuu wa Masoko wa Kampuni ya Mashujaa, alisema katika hitimisho la tamasha lao lililoanza mwaka jana, wameamua kuwaita wakongwe hao wa soka ili kulinogesha.

Alisema, siku ya hitimisho timu mbili zitamenyana katika mchezo huo wa fainali ambapo bingwa atazawadiwa gari aina ya Noah ambayo kwa imani yao itawasaidia katika kujiongezea kipato au timu kuitumia katika safari zao mbalimbali.

"Tumeona tutoe zawadi ya gari kwa maana itawasaidia katika mambo mbalimbali tofauti na zawadi ya pesa zinatumika na kumalizika, lakini gari litawasaidia katika mambo mengi," alisema.

## Matola kuiongezea kasi Yanga Ijumaa

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuipa tabu Yanga wakati akiinoa Lipuli FC ya Iringa, Kocha wa Polisi Tanzania, Seleman Matola, Ijumaa atakipima ubavu kikosi chake hicho kwa kucheza na vijana hao wa Mwinyi Zahera katika mechi ya kirafiki itakayopigwa Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

Yanga jana imeelekea mkoani Kilimanjaro kuweka kambi ya kujiandaa na mechi yao ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Township Rollers itakayopigwa Agosti 24, mwaka huu mjini Gaborone, Botswana.

Uongozi wa Yanga juzi, ulieleza kuwa umeamua kuweka kambi Kilimanjaro ili kuweza kuzoea hali ya baridi ambayo inaelezwa kufanana na ile ya Botswana kwa sasa, na ikiwa huko itacheza mechi ya kirafiki dhidi ya Polisi Tanzania ili kutafuta kasi ya kukivaa Township Rollers ambayo walipelekana mchakamchaka kwenye mechi ya awali Uwanja wa Taifa na kutoka sare ya bao 1-1.

**Aidha, Polisi Tanzania nayo imesema itautumia mchezo huo utakaopigwa majira saa 10 alasiri kwa kutambulisha wachezaji wake wa msimu huu, kutambulisha jezi na benchi zima la ufundi.**

Msimu uliopita wakati akiinoa Lipuli, Matola alikubali kipigo cha bao 1-0 katika mechi ya Ligi Kuu raundi ya kwanza iliyopigwa Uwanja wa Taifa kabla ya kuigeuzia kibao raundi ya pili kwa kupata ushindi kama huo kwenye dimba la Kumbukumbu ya Sokoine mjini Iringa.

Kisha Matola aliiwezesha Lipuli kuitupa Yanga nje kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho nchini (FA Cup) kwa kuichapa mabao 2-0 katika mchezo uliopigwa Uwanja wao wa Kumbukumbu ya Sokoine.

Akizungumzia maendeleo ya kikosi chake kilichokuwa kimeweka kambi jijini Dar es Salaam kujiandaa na Ligi Kuu inayotarajiwa kuanza Agosti 23, Matola alisema wamefanya maandalizi mazuri na ana imani kubwa ya kutoa upinzani kwa timu zote ikiwamo kwa vigogo wa soka nchini Simba, Yanga na Azam FC.

"Tumejiandaa vizuri, wachezaji wana ari ya kutosha kabla ya ligi kuanza, hivyo tunaamini tutafanya makubwa msimu utakapoanza hasa ukizingatia ni kikosi kipya, lazima wachezaji wawe na mambo mapya.

"Kwa ujumla hatuna hofu hata dhidi ya Simba, Yanga, Azam tunaweza kupambana na kupata matokeo," alisema.

Michezo
Jumatano Agosti 14, 2019
Nipashe



Ronaldo afunguka upendo wa Zidane

HABARI UK 30



Zahera

Aussems

# SIMBA SC NA SIRI CAF, REKODI SHIDA YANGA

## ●●●Kila mtu na ashinde kwao yazidi kuwabeba Wekundu wa Msimbazi, rekodi mechi za ugenini kwa Wanajangwani tatizo kubwa, makocha wafunguka...

**Na Isaac Kijoti**

WAKATI miamba ya soka nchini kwa sasa ikiwa katika maandalizi makubwa kuelekea mechi zao za marudiano za Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kulazimishwa sare kwenye mechi za awali, rekodi ya Simba kushinda nyumbani inaibeba huku watani zao, Yanga rekodi ya kupoteza ugenini ikionekana kufifisha matumaini yao ya kusonga mbele.

Simba itakuwa nyumbani Uwanja wa Taifa, Agosti 25 kuikaribisha UD Songo ya Msumbiji baada ya timu hizo kutoka sare tasa katika mechi ya awali iliyopigwa mjini Beira nchini humo, wakati Yanga iliyolazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani dhidi ya Township Rollers, Agosti 24 itakuwa mjini Gaborone kurudiana na mabingwa hao wa Botswana.

Hata hivyo, Yanga ambayo ipo mkoani Kilimanjaro ikijiwinda na mechi hiyo ya marudiano, hofu imetanda kwa mashabiki wake kutokana na rekodi zake katika mechi za kimataifa hususan ikiwa ugenini.

**YANGA KIMATAIFA**

Kwa mujibu wa takwimu za Nipashe ambazo zinalandana kabisa na zile za Shirikisho la Soka Afrika (Caf), mwaka jana kabla ya michuano hiyo kuanza kuchezwa kwa mfumo wa msimu, kwenye michuano ya kimataifa ambayo Yanga iliiwakilisha nchi katika Ligi ya Mabingwa kabla ya kutolewa na kuangukia Kombe la Shirikisho, ilicheza jumla ya mechi sita ugenini na haikushinda hata moja, huku ikipoteza nne na kuambulia sare mbili tu.

Msimu huo katika hatua ya awali kabisa ya Ligi ya Mabingwa Februari 10, mwaka jana ilianzia nyumbani dhidi ya Saint Louis Suns United ya Shelisheli na kushinda bao 1-0 kabla ya siku 11 baadaye kupata sare ya bao 1-1 ugenini.

Mechi ya raundi ya kwanza Machi 6, mwaka jana ikaikaribisha Township Rollers katika Uwanja wa Taifa na kukubali kipigo cha mabao 2-1 kabla ya siku 11 baadaye kuifuata Botswana na kulazimisha sare ya bao 1-1, hivyo mabingwa hao wa Botswana kufuzu hatua ya makundi na Wanajangwani kuangukia mechi ya mchujo kusaka nafasi ya kucheza hatua ya makundi Kombe la Shirikisho.

Katika mechi ya mchujo, Yanga ilipangwa na Welayta Dicha ya Ethiopia ambapo ikiwa Uwanja wa Taifa Aprili 7, mwaka jana ilishinda 2-0 kabla ya siku 11 baadaye kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini.

Matokeo hayo yaliipeleka Yanga hatua ya makundi kwenye Kombe la Shirikisho ambapo iliangukia Kundi D ikipangwa sambamba na USM Alger ya Algeria, Rayon Sports ya Rwanda na Gor Mahia ya Kenya.

Katika hatua hii, Yanga ilianza kwa kipigo cha mabao 4-0 ugenini Algeria dhidi ya USM Alger Mei 5, kabla ya siku 11 baadaye kutoka sare tasa dhidi ya Rayon Sports Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Julai 18, mwaka jana ikaifuata Gor Mahia nchini Kenya na kulala 4-0 kabla ya siku 11 baadaye kurudiana Uwanja wa Taifa na kupigwa tena 3-2. Baada ya mchezo huo, Yanga iliialika USM Alger Uwanja wa Taifa na kushinda 2-1 Agosti 18, kabla ya siku 11 kwenda kulala kwa bao 1-0 ugenini Rwanda dhidi ya Rayon Sports.

Matokeo hayo yaliifanya Yanga kumaliza mkiani mwa kundi bila kushinda mechi hata moja ugenini huku ikiwa na pointi nne tu, wakati UMS Alger iliyomaliza nafasi ya kwanza na Royon Sports ikimaliza nafasi ya pili zikifuzu hatua ya robo fainali.

Hata hivyo, Yanga haikuwa chini ya kocha wake mkuu wa sasa, Mwinyi Zahera ambaye tangu atue amekuwa lulu kwa mashabiki huku akijaribu kuisuka upya, hivyo anaweza kuwa mbeleko mpya kwa Wanajangwani hao katika mechi za ugenini.

Tayari Zahera amesema: "Kuna mambo yakufanyia marekebisho hususan safu ya ushambuliaji kutokuwa na muunganiko mzuri, katika mechi hizi za Caf ni muhimu sana kupata matokeo nyumbani.

"Lakini bado tunaweza kuingiza bao ugenini na hata kupata matokeo ya 2-1, hivyo tunajipanga kucheza kwa kasi mechi ya marudiano ugenini."

**SIMBA KIMATAIFA**

Mwaka jana Caf ilibadili mfumo wake wa michuano hiyo na kuanza kuandaliwa kwa mtindo wa msimu, ambapo msimu wa 2018/19, Simba waliipeperusha bendera nchi kwenye Ligi ya Mabingwa na kufanikiwa kutinga robo fainali.

Simba ambayo ilikuwa ikitamba na kaulimbiu yake "Kila mtu ashinde nyumbani", ilifanya vizuri kiasi ugenini kwenye mechi za awali na raundi ya kwanza, lakini hatua ya makundi ilikuwa na rekodi mbaya.

Simba ilianza hatua ya awali kwa kushinda mabao 4-1 nyumbani dhidi ya Mbabane Swallows ya Eswatini (zamani Sawaziland) kabla ya kuifuata kwao na kuichapa 4-0.

Mechi iliyofuata ikachapwa 2-1 ugenini Zambia dhidi ya Nkana FC, kabla ya kuifumua mabao 3-1 kweye Uwanja wa Taifa na kufanikiwa kutinga hatua ya makundi ambapo changamoto ya kupoteza ugenini ilianzia hapo.

Hatua ya makundi ilianzia nyumbani kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya JS Saoura ya Algeria kabla ya kwenda DR Congo na kunyukwa mabao 5-0 dhidi ya AS Vita kipigo kama hicho ikikipata pia ilipoifuata Al Ahly nchini Misri, lakini pia ilipoifuata JS Saoura ikatandikwa 2-0, hivyo kujikuta ikishindwa hata kupata sare ikiwa nje ya Uwanja wa Taifa katika hatua hii.

Hata hivyo, ilifanikiwa kushinda bao 1-0 Uwanja wa Taifa dhidi ya Al Ahly na 2-1 dhidi ya AS Vita na kuweka rekodi ya kushinda mechi zake zote za nyumbani hatua ya awali, raundi ya kwanza na hatua ya makundi.

Hatua ya robo fainali Simba ikalazimishwa sare tasa dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo, ikiwa ni mara yake ya kwanza kukosa ushindi katika Uwanja wa Taifa kwa msimu huo, kabla ya kwenda kutolewa ugenini kwa mabao 4-1.

Hivyo, matokeo ya sare tasa kwa Simba ugenini yanaipa matumaini makubwa ya kushinda nyumbani ambapo imekuwa ikipata support kubwa kutoka kwa mashabiki wake.

Tayari Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema ana uhakika wa kufanya vizuri nyumbani dhidi ya UD Songo na kusonga mbele.

"Kikubwa tumeweza kuzuia na kutoruhusu bao ugenini, nina uhakika tunaweza kufanya vizuri mechi ya marudiano nyumbani na kusonga mbele," alisema Aussems.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >